

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

BUNGE LA KUMI NA MOJA

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 20 Juni, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali Ofisi ya Rais - TAMISEMI, tunaanza na Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 416

**Mkakati wa Kuhakikisha Manispaa ya
Mpanda Inakuwa Safi**

MHE. RHODA E. KUNCHELA aliuliza:-

Pamoja na lengo la Serikali kuhakikisha Manispaa zinakuwa safi na kuzuia magonjwa ya mlipuko, Manispaa ya Mpanda ina changamoto ya ukosefu wa vifaa kama magari ya taka.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Manispaa zinakuwa safi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Manispaa ya Mpanda ina maroli mawili kati ya manne yanayohitajika kwa ajili ya kuzolea taka ngumu. Kutokana na changamoto hiyo, uongozi wa Manispaa umejiwekea mikakati ifuatayo:-

(i) Manispaa ya Mpanda imebinafsisha (*outsource*) shughuli ya uzoaji na udhibiti wa taka kwa mzabuni anayelipwa kuitia mapato ya ndani ya Halmashauri, mMzabuni huyu ana magari mawili na hivyo kufanya jumla ya magari kuwa manne.

(ii) Manispaa ya Mpanda imeanzisha mpango shirikishi jamii wenye jumla ya vikundi vya uzoaji na udhibiti wa taka ngumu katika mitaa 17, vimejengwa vizimba vitano kwa ajili ya kuhifadhi taka na vitakabidhiwa mikokoteni 17 tarehe 21/06/2017 siku ya uzinduzi.

(iii) Kila siku ya Jumamosi kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi wananchi wote hushiriki kufanya usafi katika maeneo ya makazi, biashara na maeneo mbalimbali ya kufanya kazi.

(iv) Kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi usafi wa kina hufanyika ambapo wananchi pamoja na viongozi mbalimbali hushiriki kufanya usafi katika maeneo yao.

(v) Siku hiyo ya Ijumaa kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi

saa 3:30 asubuhi watumishi wa Manispaa hushiriki kufanya usafi katika maeneo ya Ofisi ya Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhamasisha usafi nchini ili kuepuka mlipuko wa magonjwa na kuongeza unadhifu wa miji yetu.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Majibu ya Mheshimiwa Waziri nadhani hayana uhalisia na mazingira ya Manispaa ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2014 Halmashauri ya Mpanda ilitenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ununuzi wa gari la kukusanya taka, gari la kisasa na siyo haya malori mawili ambayo umeyasema.

Kutokana na ubadhirifu ambao umefanyika kwenye Manispaa hii, Serikali inachukua hatua gani kwa huyu mzabuni aliyetumia fedha hizi na mpaka sasa hajarudisha na baadhi ya hao watendaji ambao wamekula pesa hii, wananchi wa Manispaa ya Mpanda hivi tunavyoongea wanashinda na takataka ndani, wanashindwa kuzitoa na Manispaa imeshindwa kukusanya hizi taka kwa wakati. Serikali inamchukulia hatua gani huyu Ndugu Kisira pamoja na watendaji waliokula pesa hizi katika Manispaa ya Mpanda? (*Makofi*)

Swali la pili, imekuwa ni tabia ya Serikali kuendelea kuhamasisha wananchi kufanya usafi kwenye maeneo yao, lakini kitu kibaya zaidi ni kwamba wananchi hawa wanalaizimishwa kufunga maduka, kila siku ya Jumamosi kuanzia saa 1:00 asubuhi mpaka saa 4:00 aasubuhi na siyo Mkoa wa Katavi peke yake au Manispaa ya Mpanda peke yake ni nchi nzima, ikiwepo na maduka ya Dar es Salaam, Kigoma, Mbeya, Mwanza pamoja na Katavi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali umeshaelewka.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tabia hii ya kuendelea kufunga maduka, je, Serikali

hamuoni kwamba mnapoteza uchumi wa wananchi wao kuendelea kufunga maduka na huku wakiendelea kufanya usafi? (Makof)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Rhoda tutende haki, swali lako ulilouliza halafu una ajenda, inawezekana swali lako *ungeli-frame* vizuri lingepata majibu mazuri sana. Kwa sababu swali lako ilikuwa linajenga suala la ubadhirifu wa fedha zilizotengwa, ungelitengeneza vizuri halafu tungeweza kupata majibu mazuri sana katika hilo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimesema kwamba pale kuna magari ya taka mawili, kama kuna suala la ubadhilifu hiyo ni ajenda nyingine, tunachotakiwa kukifanya ni kwamba hatuvumilli ubadhirifu wa aina yoyote, na kama ubadhirifu huo upo, tutaenda kuufanya kazi tutaenda kufuatilia nini kilichojiri katika Manispaa ya Mpanda kama fedha zilizitengwa lakini hazikutumika vizuri katika suala hilo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la ajenda kwamba siku ya Jumamosi wananchi wanafunga maduka, kumbukumbu yangu Waziri Mkuu hapa aliulizwa na Mheshimiwa Ulega, Mbunge wa Mkuranga katika suala ya siku ya Jumamosi utaratibu wa kufanya, lengo kubwa ilikuwa usafi ufanyike lakini usizue shughuli za wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo hili limeishatolewa kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya katika maeneo yao tunapofanya utaratibu wa usafi tuangalie *modality* nzuri usafi ufanyike, lakini kama kuna mambo mengine ambayo saa nydingine yanahusu shughuli mahsusini zinaweza kufanya. Hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo naomba tufanye rejea ile vizuri tusitoe majibu mawili itakuwa ni *sub-standard* siyo vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niichukue kwamba hoja yako ya usafi ni ajenda yetu ya Kitaifa, lazima kama Wabunge, lazima kama Viongozi tusimame pamoja katika jambo hili. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje na baadaye Mheshimiwa Selasini.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa magari ya kunyonya maji machafu na kuzoa taka siyo lazima tu iwe kwenye Manispaa au Majiji, hata Wilaya zetu tunahitaji magari ya kunyonya maji machafu na magari ya kuzoa taka. Je, Serikali ina mpango gani kupeleka gari la kunyonya maji machafu pamoja na kuzoa taka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI naomba kujibu swali la Mzee wangu Lubeleje, mimi namuita greda la zamani makali yale yale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mzee Lubeleje naomba tuiweke katika vipaumbele vyetu vya Halmashauri, naomba nikusihii Mheshimiwa Lubeleje katika mpango wenu wa Halmashauri hilo jambo mkiliainisha, na sisi katika kupidisha bajeti tutalipa kipaumbele. Ninajua kwamba kweli ni jambo la msingi kufanya usafi na kuwa na mitambo hii ya kuzolea taka na kunyonyea maji, kwa hiyo mkiweka katika kipaumbele, mchakato wa bajeti ujao kama Mpwapwa mtaweka kipaumbele basi sisi hatutasisi kuhakikisha jambo hilo tunaliwekea kipaumbele hilo ili Mpwapwa mpate gari la kunyonyea maji taka.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Takataka zinaweza zikasababisha uchumi mkubwa sana kwa wananchi wetu kwa sababu taka

zinaweza zikatengeneza matofali, zinaweza zikazalisha umeme, zinaweza zikatengeneza mbolea nzuri sana na sasa hivi kwa sababu maeneo ya kutupa taka yanaendelea kupungua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali isifanye uamuzi wa makusudi, kabisa ikaleta hii teknolojia nchini, ikaanza na majiji yetu ili kuwafanya wananchi wakapata kipato kwa kukusanya takataka na kuzipeleka kwenye maeneo hayo ambayo yanaweza yakazi-process na kuzalisha vitu vingine kwa faida ya Taifa kwa ujumla? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selasini jambo lako ni zuri sana, ndiyo maana katika ofisi yetu tuna mradi mmoja unaitwa *Strategic City Project*, katika miji mbalimbali tumetenga utaratibu wa kutengeneza haya madampo ya kisasa, ambapo ukienda Mbeya utayakuta, hapa Dodoma tunajenga na maeneo mbalimbali tunatengeneza madampo kama yale. Lengo letu kubwa ni kwamba taka zitakazozolewa baadaye ziingizwe katika system maalum kuweza ku-convert katika shughuli zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sasa hivi tunakaribisha wawekezaji mbalimbali ambao katika njia moja au nyingine watasaidia ukusanyaji wa hizi taka kuweka katika malighafi nyingine, ikiwemo suala zima la utengenezaji wa mkaa.

Kwa hiyo, ni hilo ni jambo zuri Serikali na wadau mbalimbali tushirikiane kwa mustakabali wa nchi yetu ambao mwisho wa siku taka hizi baada ya kuwa uchafu inaweza ikawa malighafi na zitasaidia kujenga uchumi katika nchi yetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo, sasa aulize swalii lake.

Na. 417

Risiti za *EFD* Kutodumu kwa Muda Mrefu

MHE. RICHARD P. MBOGO aliuliza:-

Electronic Fiscal Device (EFD) risiti hazidumu kwa muda mrefu kwani zinafutika maandishi ndani ya muda mfupi.

Je, *TRA* wataridhika na maelezo ya mlipakodi bila ushahidi wa risiti?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali kulikuwa na tatizo la matumizi ya risiti za *EFD* bila maelekezo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hali hiyo ilisababisha baadhi ya wafanyabiashara kutumia risiti ambazo zinafutika au zinadumu kwa muda mfupi. Hata hivyo, baada ya kubaini tatizo hilo, *TRA* ilitoa maelekezo kwa watumiaji wote wa mashine za *EFD* kununua na kutumia karatasi zilizoidhinishwa na Mamlaka ambazo hudumu kwa muda mrefu, takribani miaka mitano. Pili, *TRA* imeidhinisha waagizaji wa karatasi zenye sifa ili kuondokana na tatizo la karatasi zisizo na kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto tunayokabiliiana nayo ya baadhi ya wafanyabiashara kutumia karatasi zinazofutika au kudumu kwa muda mfupi, *TRA* inaweza kufuatilia na kubaini kumbukumbu za mteja kutoka kwenye *server* iliyopo *TRA* na hivyo kurahisisha uhakiki wa stakabadhi, ama iliyofutika au kupotea. Hivyo basi, endapo risiti ya mtumiaji wa mashine za *EFD* itafutika au kupotea, ushahidi wa muamala uliofanywa na mteja kwa kutumia mashine za *EFD* utapatikana kwenye *server* kuu iliyopo *TRA*.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia wafanyabiashara nchini iliweza kuahidi kugawa hizi mashine bure ili kurahisisha ufanyaji wa hii miamala. Je, zoezi hili limefanyika kwa kiwango gani na Serikali ina mpango gani wa kukamilisha? (*Makof*)

Swali la pili dogo, sasa hivi tunafanya miamala kielektroniki kwa mfano kulipa gharama mbalimbali kama vile umeme, muda wa maongezi wa simu, ving'amuzi, kupitia kampuni za simu. Serikali itakubaliana na maelezo ya wafanyabiashara wanaoandaa mahesabu kwamba tulifanya malipo hayo kwa njia ya kimiamala?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la kwanza ni kweli Serikali iliahidi kugawa mashine hizi na kwa sasa tumefikia hatua nzuri, maana yake tulisitisha zoezi ili tufanye tathmini ya zile mashine tulizozigawa ili sasa kuweza kugundua changamoto na fursa nyingine katika utekelezaji wa suala hili na uthamini huu unakaribia kukamilika na muda siyo mrefu tutaendelea kuzigawa mashine hizi kwa wafanyabiashara wote ambao wako *registered* kwa ajili ya VAT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malipo ya kielektroniki ni sahihi yanafanyika katika miamala ya simu kulipia malipo mbalimbali na sisi tunashirikiana na tayari tumeisha saini *Memorandum of Understanding at TCRA* ili malipo yote yanayofanyika kupitia simu au *e-payment* yoyote ile tuweze kui-truck na kuhakikisha *document* zote na kumbukumbu zote zinaweza kupatikana kwa ajili ya kufanya uthamini kwa ajili ya kodi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hongoli, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wadogowadogo wa miti ambayo inazalisha mbao na kuni wa Mkoa wa Njombe na maeneo mengine ya Mkoa wa Iringa wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa sana wanapovuna mbao zao na kutaka kupeleka sokoni. Wakifika Iringa wanakutana na kodi nyingine au wanakutana na utaratibu mwingine kwamba lazima wawe na risiti za *EFD* wakati hao wakulima wamevuna mazao haya kwenye shamba lao, na wamepata kibali cha kuvuna na kodi nyingine wameishatoa, lakini wanaambiwa wawe na risiti ya *EFD* na hawana mashine. Wasipokuwa na risiti ya *EFD* wanaambiwa watoe faini ya shilingi milioni moja. (*Makofii*)

Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu mzuri wa kuweza kuondoa hii kero ambayo imekuwa tatizo kubwa sana kwa wakulima wetu hususani wa Lupembe na maeneo mengine wanaosafirisha mbao zao kwenda sokoni Dar es Salaam? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi na Mheshimiwa Mbunge kama atakumbuka nimekaa naye kujadili tatizo hili na tayari nimeshaelekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kufuatilia jambo hili, ni risiti za aina gani zinazodaiwa Iringa tu.

Kwa hiyo, naahidi kwamba hili linafanyiwa kazi, nami nilimuahidi Mheshimiwa Mbunge nikimaliza kipindi hiki cha bajeti nitakwenda Iringa kushughulikia tatizo hili. (*Makofii*)

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba *EFD* ni mashine ya kukusanya kodi na kutoa risiti, kwa maana nyingine ni *device* ya *TRA* ya kukusanya kodi, sasa kwa nini Serikali isiwapo wafanyabiashara *EFD* mashine bure?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *EFD* ni sahihi ni kwa ajili ya matumizi ya kikodi pia kwa matumizi ya wafanyabiashara wetu ili waweze kujua kumbukumbu sahihi katika kufanya biashara zao. Katika hili ndio maana Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwamba *EFD* zigawiwe bure, lakini tuangalie mfumo mzuri wa kuweza *ku-share* gharama hizi za kupata mashine hizi za *EFD*. Kwa hiyo, Serikali inawekeza lakini na wafanyabiashara wetu nao wanawekeza kwa pamoja ili tuweze kujenga Taifa letu.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imejidhatiti kukusanya mapato kwa kupitia mashine hizi za *EFD*, lakini kuna matatizo makubwa ya kutokuwepo kwa mtandao au mawasiliano tunapoenda kwenye vituo vya manunuzi, vinavyosababisha wanunuzi kukaa kwenye vituo kwa muda mrefu wakisubiri risiti au wakati mwingine tunakata tamaa tunaondoka bila kuwepo na risiti.

Je, Serikali ina mpango gani makini kuhakikisha kwamba inaboresha mfumo wa kukusanya kodi pamoja na kupata huduma kwa muda unaotakiwa ili kuhakikisha kwamba kile walichokikusudia kinaliletea Taifa mapato kwa maendeleo yetu? Ahsante. (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba lipo hili tatizo kwa baadhi ya wauzaji na wafanyabiashara ndani ya nchi yetu. Tatizo la kimtandao halipo kwa kiwango ambacho wafanyabiashara wanakisema, nitoe wito kwa Wabunge kama viongozi kwenye maeneo yetu tushikamane na Serikali yetu kwa sababu hakuna maendeleo bila kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushirikiane katika kuhakikisha wafanyabiashara wanatumia mashine hizi kwa pamoja, lakini *TRA* wanafanya jitihada kubwa za kupita maeneo ya wafanyabiashara wetu kuhakikisha kwamba

mashine hizi zinatumika na zinafanya kazi. Ni wito wangu kwenu Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuhakikisha hili linaweza kufanyika ndani ya nchi yetu.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 418

**Vyombo vyta Habari kuajiri Wakalimani wa
Lugha za Alama Nchini**

MHE. AMINA S. MOLLEL aliuliza:-

Haki ya kupata taarifa ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania na vyombo vyetu vyta habari havina wakalimani wa lugha ya alama kwa ajili ya kuwawezesha viziwi kupata habari kwa uelewa uliotimilifu kama raia wengine.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa vyombo vyta habari hasa *tvvinaajiri* wakalimani hasa katika taarifa za habari ili waweze kufuatilia matukio yanayooneeshwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA
MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Amina Saleh Mollel (Mbunge), kwa kuona umuhimu wa suala hili pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote hasa Mheshimiwa Stella Alex Ikupa (Mbunge) ambaye naye aliuliza swali hili tarehe 08/05/2017 katika mjadala wa bajeti ya Wizara yetu.

Napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa baada ya swali la Mheshimiwa Stella Alex Ikupa Mbunge, Wizara iilitisha kikao cha wadau mbalimbali wakiwepo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Chama cha Viziwi Tanzania (*CHAVITA*), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *VETA*, Chama cha Wakalimani wa Lugha za Alama (*TASLI*), *TBC* na wadau wengine ili kutafakari namna ya kutekeleza kwa haraka azma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, tulikubaliana kwamba *VETA* watoe mafunzo hayo kwa kushirikiana na *CHAVITA* na *TASLI*, kutokana na mtandao mkubwa ambao *VETA* wanao na *VETA* wamekubali. *TASLI* wamepewa kazi ya kuandaa kanzi data za wakalimani wa lugha ya alama kwa viziwi, na *TCRA* wanaandaa kalenda yaani *road map* ya utekelezaji wa matumizi ya huduma za wakalimani wa lugha ya alama katika vituo vyta televisheni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hatua hizo *TBC* inaendelea na mawasiliano yake na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa - Taasisi ya Elimu ya Juu, inayofundisha wataalamu wa lugha ya alama kuona ni namna gani shirika linavyoweza kuwatumia wataalamu, wahitimu na wanafunzi wa chuo hicho kutoa kwa muda huduma ya lugha ya alama kupitia *TBC*.

Aidha, Serikali imeandaa kutekeleza suala hili kwa kuweka wakalimani wa lugha ya alama katika matukio ya Kitaifa kama maadhimisho ya miaka 53 ya Muungano yaliyofanyika 26 Aprili, 2017. Vilevile *TBC*iko kwenye mchakato wa kuajiri wakalimani wachache kwa kuanzia wa lugha za alama kwa taarifa zake za habari na katika matangazo machache yanayorushwa na televisheni hiyo ya *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa wito kwa wamiliki wa vyombo vyta habari binafsi nchini nao kuanza mchakato wa kuwaajiri wakalimani wa lugha ya alama ili waweze kuwawezesha watu wa kundi hili kupata taarifa kupitia vyombo vyao habari.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina Mollel swali la nyongeza kama unalo.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali ya nyongeza ninayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, awali ya yote ninalipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pongezi ziende kwa Spika wa Bunge kwa kuwa tayari wamekwishaanza kutoa huduma hii katika matangazo haya, wakalimani wamekwishaanza kutafsiri na kuwawezesha wenzetu viziwi kupata taarifa.

Kwa kuwa kilio cha haki ya kupata taarifa ni cha muda mrefu katika mjadala pia wa bajeti ya Wizara tulilizungumzia hili. Ningependa kupata *commitment* ya Serikali; je, ni lini sasa utekelezaji huu utaanza na kwa kuwa *TBC* ni televisheni ya umma, *commitment* ya Serikali kwamba Shirika hili litaaajiri lini wakalimani wa lugha ya alama ili basi wenzetu viziwi waweze kupata taarifa?

Swali langu la pili, kwa kuwa haki ya kupata habari ni haki ya Kikatiba, je, Serikali inatoa muda gani kwa wamiliki wa vyombo binafsi vya habari ili na wao basi waone umuhimu na kutekeleza haki hii ya Kikatiba ambayo ni ya lbara ya 18(d)? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa pongezi ambazo ametoa na tunazipokea, tunasema ahsante sana. (*Makof*)

Katika swali lake la kwanza ambalo anahitaji kujua sasa ni lini *TBC* itaaajiri, nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Amina Mollel kwa jinsi ambavyo amekuwa amepambania haki za walemvu, na kwa kweli nakumbuka kabisa kwamba hata katika mjadala wa bajeti ya Wizara yetu alichangia suala hili na alitaka kujua ni lini hasa vyombo vya utangazaji vitakuwa vikituo ukalimani wa lugha ya alama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ni kwamba, katika kikao ambacho kilifanyika wadau wale walijipangia majukumu mbalimbali. Kwa upande wetu Wizara tulipangia *TBC* iwe ni chombo cha mfano, ianze mara moja kutoa ukalimani wa lugha ya alama, na kwa kuanzia *TBC* tayari imeishatuma maombi ya kupata kibali cha kuajiri wakalimani wawili, hivyo wakati wowote kibali kitakapotoka basi *TBC* itaajiri ili iweze kuwa chombo cha mfano kwa vyombo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwamba ni muda gani tumeweka kwa vyombo vya habari. Kama mlivyosikia katika jibu la msingi ni kwamba, *TCRA* imepewa jukumu la kuchukua kanzi data kutoka *TASL* ambayo ni orodha ya wale wakalimani ambao wana uwezo wa kutoa ukalimani katika vyombo vya habari, wakiishachukua taarifa hizi watakuwa wakipeleka kwa vyombo vya habari.

Sasa tatizo ambalo tunalo ni kwamba vyombo vya habari ni vingi, vyombo vya habari vya utangazaji televisheni, ni vingi takribani 32, lakini kwa mujibu wa *TASL* wapo wakalimani 70 na kati ya hao wakalimani 15 tu ndiyo ambao wanaonekana kwamba wana ujuzi na uwezo wa kufanya ukalimani katika vyombo vya habari au utangazaji wa televisheni. Ndiyo maana sasa *VETA* na *CHAVITA* wamepewa jukumu la kutoa mafunzo kwa hawa wakalimani wengine waliobaki ili na wao waweze kufikia uwezo wa kutangaza katika vituo vya televisheni. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni muda mrefu sasa wananchi wa Wilaya ya Lushoto hawapati mawasiliano hasa ya redio ya Taifa na hili swali nimekuwa nikiliuliza mara kwa mara.

Je, ni lini Serikali itajenga mitambo hiyo ili wananchi wa Wilaya ya Lushoto waweze kupata taarifa kama ilivyokuwa kwa wananchi wengine waishio mjini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Habari majibu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira swali linalokuja linaongelea masuala ya usikivu wa redio katika nchi ya Tanzania.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, sasa aulize swali lake.

Na. 419

Kuboresha usikivu wa *TBC* na Televisheni huko Amani

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya *TBC Radio* kwenye maeneo ya Tarafa ya Amani Muheza ni hafifu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mawasiliano ya redio na televisheni ya Kituo cha Taifa cha *TBC*?

(b) Je, ni lini Serikali itaboresha mawasiliano kwenye maeneo hayo ya milima ya Amani ya Vituo vya Taifa Redio na *TBC* ili wananchi waweze kunufaika na vipindi hivyo?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa mawasiliano ya Redio na Televisheni ya Taifa (*TBC*) yanaimarishwa na kuwafikia wananchi katika

maeneo yote ya nchi. Katika kutekeleza dhamira hiyo, Serikali kila mwaka imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu na usikivu wa redio na televisheni ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuboresha usikivu wa redio za Shirika katika maeneo ya mipakani mwa nchi ambayo ni Kakonko, Tarime, Rombo, Longido na Nyasa, na utekelezaji wa mradi huo unaendelea. Aidha, katika hatua ya kuhakikisha changamoto ya usikivu wa redio za Shirika inapatiwa ufumbuzi kwa kiwango kikubwa, Serikali imeendelea kuimarisha bajeti ya upanuzi wa usikivu wa *TBC*, ambapo katika mwaka 2017/2018 shilingi bilioni tatu zimetengwa ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni mbili ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2016/2017, ambapo kiasi cha shilingi bilioni moja zilitengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa usikivu wa Redio na Televisheni ya Taifa ni wa hatua kwa hatua, hivyo Serikali itaendelea kutekeleza azma hii katika maeneo ambayo kuna usikivu hafifu kwa kuendelea kutenga fedha kila mwaka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi Adadi swali la nyongeza.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Tarafa ya Amani tunaitegemea sana pale Muheza kwa mambo ya uchumi, kukosekana kusikilizwa kwa redio kwenye maeneo hayo pamoja na televisheni hususan kwenye Kata za Mbomole, Zirai, Misarai, Amani kwenyewe na Kwezitu kunawafanya wananchi hao kukosa uzoefu ili kuweza kujifunza sehemu nyingine. Swali langu la kwanza ni kama ifuatavyo:-

Kufuatana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 zimetengwa

bilioni tatu, nataka uwahakikishie wananchi wa Amani kwamba nao wako kwenye mpango huu ili waweze kupata uzoefu wa kuona televisheni yao na redio yao ya Taifa?

Swali langu la pili; utaratibu wa *TBC* wanapoweka minara kwenye vijiji kuwalipa fidia wananchi wa vijiji hivyo vyta karibu ili kuimarisha ulinzi na pia kuhakikisha kwamba usalama wa minara hiyo inakuwepo. Kata yangu moja ya Potwe ina mnara wa *TBC*, lakini hawajapata fidia na ninaomba kama kwenye mpango huu wa sasa hivi, kwenye hii Tarafa ya Amani patakuwepo na mipango ya kuongeza usikivu, basi wananchi hao waweze kulipwa fidia.

Naomba uwahakikishie wananchi hao mambo hayo, nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ametaka kujua hizo shilingi bilioni tatu kama wao nao wako kwenye mpango huu wa kuimarisha usikivu. Labda tu nitoe maelezo kama tulivyosema nadhani sote tuliskia hotuba ya Mheshimiwa Waziri akisoma katika bajeti yetu ni kwamba ziko Wilaya nyingi sana ambazo hazina usikivu. Ziko Wilaya takribani 84 usikivu wake ni hafifu sana. Tulipoanza kujaribu kuboresha usikivu katika Wilaya zetu tano tulianzia kwanza kwa mwaka huu wa fedha katika Wilaya ya Geita na tulipoweka mitambo ile ya *FM* katika Mkoa wa Geita tumegundua kwamba katika utafiti wetu ni kwamba masafa yale usikivu uko katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Geita na maeneo mengine.

Kwa mfano; usikivu umekwenda mpaka Geita Mjini, umekwenda Bukombe, umekwenda Chato, umekwenda Kahama, kwa hiyo, ni imani yangu kwamba tunapoboresha meneo ya Longido na maeneo ya Rombo pengine usikivu unaweza ukaboreka katika maeneo mengine. Kwa hiyo, siyo rahisi sasa hivi kuamua kwamba hizi shilingi bilioni tatu tunaweza kuzipeleka wapi, tunatarajia tuone kwamba effect inaweza au usikivu huu katika maeneo haya tutakayoboresha yanaweza yakaenda mpaka maeneo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tuna mpango mwininge wa kufufua ile mitambo ya zamani, mitambo ya *AM* ambayo yenye we inakwenda mbali zaidi. Mwanzoni tulikuwa na mitambo minne tu ambapo mmoja ulikuwa Dodoma, mwininge Mwanza, mwininge Dare es Salaam na mmoja ulikuwepo Nachingwea, ambapo yote hii ilikuwa inapelekea usikivu katika nchi nzima. Kwa hiyo, tumeshakubaliana na wadau wa maendeleo kwamba watatusaidia kufufua mitambo hii, ili kusudi tuweze kuboresha usikivu katika nchi nzima. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulembo.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa kama alivyosema muuliza swali wa kwanza *TBC* wameweza kupata shilingi billioni tatu, naomba kumuuliza Mheshimiwa mjibu swali.

Ni lini Serikali itaweza kununua vifaa vidogo *TVU* au *AVIWEST* vifaa vile tukio linapotokea wanaweka pale pale tunakwenda kwenye *breaking news*, lakini *TBC* leo kwenye *breaking news* wanakodi vifaa, kifaa kimoja kinanunuliwa kama shilingi milioni 50 au shilingi milioni 60, hii ni aibu katika Serikali yetu.

Serikali waniambie ni lini wataweza kununua vifaa hivyo na kuvisambaza Tanzania kwa sababu masafa marefu hayasikiki. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa swali la Kibunge, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana, kama nimempata vizuri Mheshimiwa Mbunge hii *TVU*ni kwa upande wa televisheni na ambapo tayari *TBC* imeshanunua vifaa hivi, ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndassa, halafu Mheshimiwa Bilago.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *TBC 1* na *TBC Redio* ni visemeo vya Taifa, ndiyo spika ya Serikali. Je, kwa sababu matatizo ni mengi, usikivu karibu nchi nzima hawasikii vizuri, Je, Mheshimiwa Waziri hivi unatambua kwamba *TBC 1* na *Redio TBC 1*, televisheni ni kisemeo cha Taifa. Kwa nini sasa Serikali isiwekeze ili kuondoa kutokusikia vizuri katika maeneo mbalimbali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Habari.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba njibuu swali la nyongeza la Mheshimiwa Seneta Ndassa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa *TBC* katika nchi hii na ndiyo maana umeona uwekezaji ukiongezeka kila mwaka. Sasa hivi tupo katika kuboresha usikivu katika Wilaya tano kwa pesa tulioongezewa tuna uwezo kuongeza usikivu katika Wilaya zingine 15. Kwa hiyo, tunapoongeza hizo Wilaya 15 tunaenda kuangalia sehemu ipi ambayo ina hali mbaya zaidi tutaendelea kuboresha hii bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na matatizo ya kifedha, sasa hivi tumeanza kuangalia pia mifumo yetu ya ndani ambayo imekuwa ikitunyima kupata kipato zaidi. Tuna mikataba ambayo mmekuwa mkiipigia kelele hapa kama *StarTimes*, tumeanza kuchunguza, ninaku hakikishia kwamba katika zoezi tunalolifanya sasa hivi kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais tutafika mahali pazuri. Kwa taarifa tu kwa Bunge hili lako Tukufu Mheshimiwa Rais wa *StarTimes Group* kutoka China imebidi naye afunge safari kama mwenzetu wa makinikia kuja kutuona kwa ajili ya suala hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii nyeti. Wilaya ya Kakonko ni mionganini mwa Wilaya zenyeye matatizo ya usikivu wa *TBC*. Kule tunasikiliza Redio Burundi, ndugu yangu Mheshimiwa Mwamoto ni shahidi amekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kibondo kule. Maeneo ya Kibondo na Kokonko hakuna usikivu wa *TBC*. Katika swali la msingi imetajwa Wilaya ya Kakonko. Naomba kujua na nipewe *time frame* na Serikali ni lini, ni tarehe ngapi *TBC* itaanza kusikika Kakonko?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kwamba Kakonko ni moja ya zile Wilaya tano za mipakani ambazo zimetengewa fedha katika bajeti ya mwaka huu 2016/2017, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwamba amekuwa akipambania usikivu katika Wilaya yake na ni kweli kwamba matangazo mengi wanayapata kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu ambao tumeanza, tulianza na kufanya tathmini kwamba ni wapi minara iwekwe tayari tulishaomba masafa kutoka *TCRA* na tumepata, tayari mzabuni ameshapata zabuni ya kufanya kazi hii, lakini *time frame* tuliyopanga ni mwisho wa mwaka huu wa fedha usikivu utakuwa umeimarika katika Wilaya ya Kakonko na maeneo mengine ambayo ameyataja. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hussein Nassor na Mheshimiwa Sugu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matatizo ya usikivu pia *TBC* kuna matatizo ya weledi kwa watangazaji. Mfano, kuna watangazaji wa *TBC* walitangaza uongo

kwamba Donald Trump alimpongeza *President Magufuli*, upambe uliopitiliza mpaka tajiri anashtuka. Sasa wale watu walismamishwa lakini hivi karibuni nimeanza kuwaona kwenye tv. Walipewa adhabu gani ili wasirudie tena upambe? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Habari.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA

MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichukua hatua za kinidhamu kwa kosa ambalo ni la kiufundi tu ambalo mtu yejote duniani hapa anaweza kulifanya. Yametokea matatizo kama hayo hayo Kenya yalifanyika na watangazaji wamerudi, tulichokifanya ni kuchukua tu hatua ya muda mfupi. Wazungu wanasema *it's a deterrent* kwamba uwe muangalifu zaidi. Ni kitu kinafanyika kila siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nikikuletea, tuchukulie tu mfano wa magazeti yote yanayochapishwa kila siku, ninakuuhakikishia asilimia 60 utakuta kuna matatizo/makosa ndani, ni kitu cha ubinadamu. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Ni Mheshimiwa Hussein Nassor au uko mbali kidogo? Huyo hapo, ni huyo uliyesimama, sawasawa. Ni Mheshimiwa nani?

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mipata.

MWENYEKITI: Aaah, Mheshimiwa Mipata, *okay*.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi usikivu kwa ujumla hasa mwambao mwa Ziwa Tanganyika katika Tarafa ya Wampembe, Kata ya Kala, Wampembe, Kizumbi pamoja na Ninde hazina kabisa usikivu wa Redio Tanzania, bahati mbaya sana maeneo haya hayana mawasiliano ya barabara ya uhakika. Viongozi ni mara chache wanatembelea maeneo haya ukiacha *DC*, Mkoo wa Mkoa na viongozi wengine wa

Chama. Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha usikivu katika eneo hili ili wananchi wa Ziwa Tanganyika mpakani kule wawe na usikivu wa kutosha kusikiliza matangazo mbalimbali ya nchi yao? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kama nilivyotangulia kusema mwanzoni, tuna mpango wa kufanya suluhisho la kudumu ambalo tunaweza kukarabati ile mitambo michache ambayo inaweza ikafika eneo la nchi nzima. Kwa mfano, mtambo ule wa Mwanza unaweza ukaenda mpaka maeneo hayo na tayari tumeshaandika andiko kupeleka kwa mbia wetu wa maendeleo ambaye tayari amekubali kufanya ukarabati wa mitambo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa, kuliko kusubiri hizi fedha kidogo kidogo za kila mwaka ni bora tukaifufua ile mitambo ya *AM* ambayo haina matatizo kabisa na sifa zake ni kwamba inakwenda mbali sana na haipati pingamizi la milima.

Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira ili kusudi tuweze kupata majibu kutoka kwa mbia wetu wa maendeleo na kuweza kufufua mitambo yetu ambapo maeneo hayo aliyoyataja yatapata usikivu pamoja na nchi nzima.

MWENYEKITI: Ahsanteni sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri, *TBC* imetosha. Sasa tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 420

**Kufungwa Gerezani wa Mama wenyе Watoto Wadogo/
Wachanga**

MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA aliuliza:-

Wapo wanawake ambao wamefungwa kwenye magerezani wakiwa na watoto wachanga/wadogo ambao bado wanahitaji uangalizi au huduma za mama zao.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuwanusuru watoto hao ambao hawana hatia?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inavunja haki za binadamu kwa kuwaweka gerezani watoto hao wasio na makosa?

(c) Je, Serikali inaweza kulipa Bunge takwimu za wanawake waliokinzana na sheria na wamefungwa kwa miaka mitano iliyopita?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yapo mazingira ambayo watoto wadogo na watoto wachanga huingia gerezani wakiwa wameambatana na mama zao kutokana na mama zao kufungwa gerezani au kuingia mahabusu, ama mama zao kuingia wakiwa wajawazito na baadae kujifungua gerezani. Watoto hao hupokelewa na kuruhusiwa kuwepo gerezani na mama zao kwa mujibu wa Kifungu cha 144(1) cha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 na Kanuni 728 ya Kanuni za Kudumu za Jeshi la Magereza za mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kuruhusu watoto kuwa na mama zao magerezani unatokana na kuzingatia

maslahi ya mtoto kama inavyohimizwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto (*The Convention of Rights of the Child*) na mikataba mbalimbali ya kikanda inayohusiana na haki za mtoto. Kwa kuwa mtoto mchanga huwa bado ananyonya, hivyo himaya stahiki ya malezi na makuzi ya awali huwa ni ya mama yake. Hata hivyo Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 imetoa nafasi kwa mtoto ambae mzazi wake wake yuko katika ukinzani wa sheria kuweza kupata malezi mbadala ambayo yanazingatia mahitaji yote ya mtoto kama ilivyo kwa mtoto ye yole yule chini ya uangalizi wa uongozi wa magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2016, idadi ya wanawake waliofungwa magerezani kutokana na kukinzana na sheria ili kuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 ni 364, mwaka 2013 ni 321, mwaka 2014 ni 373, mwaka 2015 walikuwa ni 334 na mwaka 2016 ni 616. Hivyo kufanya jumla yake wote kuwa ni 2008.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Raisa swali la nyongeza.

MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida wafungwa wanawake au kisheria wanatakiwa walindwe au wasimamiwe na askari magereza wanawake na tunaamini kwamba magereza wale ambao wamefungwa kule wako katika mikono salama. Inakuwaje akina mama wale wanapata ujauzito wakiwa katika magereza? (*Makofii*)

Swali la pili ni kwamba, je, Waziri haoni kwamba iko haja ya akina mama hawa kupewa vifungo vya nje ili kutoa haki kwa watoto wale wasiwemo ndani ya magereza kama walivyo mama zao? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa mujibu wa utaratibu na ndivyo hali ilivyo kwamba wafungwa wanawake wanasmamiwa na askari magereza wa kike. Sasa hoja kwamba wafungwa wale wanapata mimba wakiwa gerezani hiyo inahitaji uthibitisho, kwa sababu katika hali ya kawaida huwezi kujua mimba ile ameipata vipi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kimsingi mazingira hayaruhusu hali hiyo kutokea katika Magereza. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba inawezekana pengine waliingga pale hali ya kuwa walikuwa na mimba changa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na vifungo vyanya kwa akina mama hawa. Tunao utaratibu ambao haubagui jinsia ya kuweza kuwapatia vifungo vyanya kwa mujibu wa taratibu. Tuna utaratibu wa huduma za jamii, tuna utaratibu vilevile wa msamaha na wanawake wanafaidika katika taratibu zote mbili. Kwa hiyo, utaratibu huo upo lakini inategemea na makosa. Kwa wanawake ambao makosa yao hayakidhi vigezo vyanya kuweza kupata fursa hiyo wataendelea kutumikia vifungo vyao kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, itabidi sasa Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri mfuatilie ili kama ni kweli wanafanya jambo hili, hawa akina mama tujue inakuwaje. Nimeona Mheshimiwa Anna Gidarya, Mheshimiwa Waziri anataka kuongea. Haya, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Waheshimiwa Wabunge wamesimama wengi sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimezunguka takriban Magereza ya Mikoa yote na katika zunguka ile hakuna eneo hata moja ambako nimefika nikaelezewa kwamba mama ama mwanamke aliyejewa amefungwa kifungo cha muda

mrefu amegundulika amepata mtoto akiwa katika kifungo cha muda mrefu. Ni kweli unaweza ukakuta wale waliokuwa wana vifungo vyta muda mfupi wakajifungua wakiwa gerezani, lakini kujifungua wakiwa gerezani haina maana kwamba mimba kaipatia gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge niwaambie tu vyombo vyetu hivi ni vyombo vinavyofanya kazi kwa sheria kali sana. Haingewezekana mwanamke apatie mimba ndani halafu ijifice isijulikane kwamba kapatia mimba pale. Kwa hiyo, hatua zingeshachukuliwa na wale watu ni wachukuaji wa hatua kweli kweli. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ahsante kwa kututhibitishia. Jicho langu limemuona Mheshimiwa Anna Gidarya na Mheshimiwa Ikupa.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu ya Waziri na swali la msingi kumekuwa na msongamano mkubwa katika magereza ya wanawake, pia inaonekana kuna matatizo makubwa sana ya kisaikolojia kwa wale watoto wanaokulia pale gerezani kwa sababu mazingira siyo rafiki. Je, ni lini sasa Serikali itatenga kituo maalum kwa ajili ya wale wanawake wanaofungwa wakiwa na mimba na wakiwa na watoto wachanga? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mazingira ya magereza ya wanawake, Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha mazingira ya magereza yetu kila mwaka kadri hali ya uwezo wa bajeti inavyoruhusu ikiwemo maeneo ambayo magereza ya wanawake yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo

Mheshimiwa Waziri amezungumza, tumekuwa tuna utaratibu wa kufanya ziara kwenye magereza haya. Naomba nikiri hapa kama kuna maeneo ambayo yana mazingira mazuri ni magereza ya wanawake kuliko wanaume.

Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuwapongeza sana akina mama inaonekana siyo tu katika hali ya maisha ya kawaida lakini hata hali ya gerezani maeneo yao yanakuwa ni maeneo ambayo yanakuwa safi na mazuri zaidi kimazingira pia Serikali inafanya jitihada kwa kutoa kipaumbele maalum katika maeneo ambayo magereza ya akina mama wenye watoto yapo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ikupa.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita Mkoani Dar es Salaam lilitokea tukio la kusikitisha dhidi ya watu wenye ulemavu ambao ni waendesha bajaji ambapo walifanyiwa vitendo vya udhalilishaji pamoja na vitendo vya kinyama, walipigwa sana na baadae kuburuzwa chini. Pamoja na makosa ambayo walidaiwa kuwa nayo lakini *approach* ambayo ilitumika na askari wetu haikuwa nzuri kabisa. Je, nini kauli ya Serikali kwa hili? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Ikupa kwa kuleta swali hilo na yeye ni Mbunge anayewakilisha kundi hilo, kwa sababu yupo ni-*apologize* kwa niaba yake awafikishie salamu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema kwamba pamoja na utaratibu kuwepo ama ukiukwaji wa utaratibu, kwa kuzingatia hali yao ni nguvu kubwa imetumika. Serikali tumeshajadiliana na wenzetu wa

TAMISEMI, watakatana na Wizara ya TAMISEMI pamoja na wenzao wa ngazi ya Mkoa ili kuweka utaratibu ambao utakuwa una taswira nzuri na kufanya jambo hilo ili lisiweze kujirudia kuweka utaratibu ulio wa kudumu ili liweze kufanya utaratibu huo wa kudumu. Kwa hiyo, tumepokea *concern* hiyo na linafanyiwa kazi ili jambo la aina hiyo lisijirudie. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 421

**Mauaji ya Wazee na Watu Wenye Ulemavu wa
Ngozi – Ushetu**

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA aliuliza:-

Miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na mauaji ya wazee na walemvu wa ngozi kutokana na sababu mbalimbali.

(a) Je, ni idadi ya watu wangapi waliopoteza maisha katika Jimbo la Ushetu kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015?

(b) Je, mauaji ya makundi haya yanapungua au yanaongezeka katika Jimbo la Ushetu?

(c) Je, Serikali imeshirikisha vipi jamii kupiga vita mauaji haya, vikiwemo vikundi vya dini, walinzi wa jadi (sungusungu) na uongozi wa kimila Jimboni Ushetu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2010 wazee waliouawa walikuwa wawili, mwaka 2011 wazee wanee, mwaka 2013 wazee watano, mwaka 2014 wazee waliouawa walifikia sita, mwaka 2015 walikuwa wawili, mwaka 2016 wawili na mwaka 2017 alikuwa ni mzee moja. Kwa hiyo, jumla ya wazee ambao wamepoteza maisha katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwaka 2010 hadi 2017 ni wazee 22 katika Jimbo la Ushetu. Kwa upande wa walemaru wa ngozi, katika kipindi hicho hakuna mlemavu aliyeuawa wala kujeruhija Jimboni Ushetu ila kwa nchi nzima kwa kipindi cha miaka 2010 mpaka 2017 walemaru wa ngozi waliouawa walikuwa ni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa mauaji ya makundi haya katika miaka ya karibuni yanapungua kutokana na misako iliyofanywa ya kuwakamata waganga wa kienyeji ambao wanapiga ramli chonganishi na kuchochea imani za kishirikina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukomesha mauaji haya, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwemo kushirikiana na taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali ndani na nje ya Jimbo hilo katika kutoa elimu ya ukatili huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikishirikiana na jamii na taasisi za kidini, vikundi vya ulinzi jamii ndani na nje ya Jimbo la Ushetu kwa kuwapa elimu wananchi ili kudhibiti maujai hayo ya kikatili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kwandikwa kama una swali la nyongeza.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali.

Kwa kuwa tuna kituo cha polisi chenye hadhi ya Wilaya, hiki ni kituo kipyaa na bado kina changamoto, tunao askari wachache 38 tu, lakini askari hawa wanafanya kazi nzuri kwa kushirikiana na wananchi, Madiwani na Halmashauri.

Pia kwa kuwa hakuna vifaa/vitendea kazi yakiwemo magari, kwa sasa Hal mashauri ya Ushetu tumewapa Polisi jengo pamoja na gari. Tunahitaji kuwa na vituo vidogo kandokando kwa sababu Jimbo la Ushetu ni kubwa, linapakana na majimbo nane na tumedhamiria kutokomeza kabisa mauaji ya wazee na walemaavu.

Je, ni lini Serikali itatupatia vifaa ikiwemo magari pamoja na askari ili angalau tufikishe askari 100. Hii itasaidia sana pia kupunguza makosa katika majimbo nane ambayo napakana nayo. Ni lini sasa Serikali itatusaidia?

Swali la pili, kwa kuwa tunazo jitihada za kujenga vituo vidogo kando kando katika maeneo ya Kata ya Chambo, Kata ya Ulowa, Kata ya Ubagwe na kata Idahina na kwa kuanzia katika Kata ya Idahina tuna jengo ambalo tumetumia nguvu za wananchi, Mbunge pamoja na wachimbaji wadogo, na litaweza kuwa *accommodate* ofisi pamoja na askari wapatao watano.

Je, Serikali iko tayari sasa kutusaidia kukamilisha jengo hili ili tuweze kupata askari tuweze kuimarisha masuala ya usalama katika eneo hili ambalo linakuwa kwa kasi? Ahsante. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri naona maswali marefu naomba ujibu kwa ufupi tu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake kubwa alizonazo za kuhakikisha kwamba hali ya usalama katika Jimbo lake inaimarika, amekuwa akifuatilia kwa karibu sana maendeleo ya vyombo vyetu vya usalama katika Jimbo lake naomba nimpongeze sana kwa niaba ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kuongeza idadi ya askari na vitendea kazi vingine ikiwemo magari, naomba nilichukue hilo nikitambua kwamba katika

bajeti ya mwaka huu wa fedha tuna matarajio ya kuongeza na kuajiri vijana wapya japokuwa ni kweli tuna uchache wa askari siyo tu katika Jimbo lake, ni katika maeneo mengi nchi nzima. Kwa hiyo, tutazingatia kulingana na mahitaji ya nchi nzima ili tuone jinsi gani tunaweza kufanya kusaidia jitihada za askari wetu pale katika Jimbo lake pamoja na usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na jengo lake ambalo amezungumzia vilevile kama nilivyokuwa nikijibu mara nyingi hapa, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba majengo ya hivi vituo vyetu vya vyombo vya usalama vyote ni malengo ya Serikali kuhakikisha kwamba vinaimarika, tuna upungufu huo vilevile katika maeneo mengi nchini. Nichukue fursa hii kumhakikishia kwamba jitihada zinafanyika hata nije ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumekuwa na utaratibu wa kutumia taasisi yetu ya Jeshi la Magereza kuweza kuanza ujenzi kwa kutumia rasilimali za maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge kulitumia Jeshi la Magereza katika eneo lake kwa ajili ya kuanza harakati za ujenzi wa kituo hicho na baadaye pale itakapofikia katika hatua nzuri tunaweza kulikamilisha kwani katika mwaka huu wa fedha tumetenga bajeti fedha za kutosha kuhakikisha kwamba tunamaliza maboma yote ambayo yamejengwea kwa nguvu za wananchi pamoja na nguvu na vyombo vyetu vya usalama kwa kutumia rasilimali za maeneo yale. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Waziri, muda naona unakwenda zaidi tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swalii lake.

Na. 422

Kupunguza mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi

MHE. DKT. DAVID M. DAVID aliuliza:-

Mkomazi Game Reserve (sasa Hifadhi ya Taifa Mkomazi) ilianzishwa kabla ya Uhuru wakati tukiwa na idadi ndogo ya watu na mifugo.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kusogeza mipaka ya Hifadhi ya Taifa Mkomazi ili wananchi wa Kata za Visiwani, Mji Mdogo wa Same na Vumari wapate maeneo ya kuishi, kilimo na ufugaji?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa Mkomazi imetokana na kupandishwa hadhi kwa Pori la Akiba la Mkomazi – Umba kuititia Tangazo la Serikali Namba 27 la mwaka 2008. Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ilirithi mipaka ya lililokuwa Pori la Akiba la Mkomazi – Umba mipaka ambayo ilitambulika kisheria kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 275 la mwaka 1974.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ni sehemu muhimu ya mfumo wa kikolojia na toshelezi kwa idadi ya wanyamapor waliopo hifadhini kujipatia mahitaji yao ikiwemo malisho, maji na maeneo ya mazalia hivyo kufanya hatua za kupunguzwa kwa eneo kusababisha athari hasi ikiwemo baadhi ya wanyamapor kutoka nje ya hifadhi kwa ajili ya kujitafutia mahitaji yao muhimu na hatimaye kusababaisha kuongezeka kwa migogoro kati ya binadamu na wanyama pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya mwaka 2009 hairuhusu kufanyika kwa shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi ikiwepo kilimo, ufugaji na uchimbaji madini. Hivyo, kutokana na sababu hizi za msingi za kiuhifadhi, kwa sasa Serikali haioni haja ya kusogezza mipaka ya hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, isipokuwa kwamba Serikali itaendelea kupokea kutoka kwa wananchi na wadau wengine maoni yatakayozingatia matakwa ya sheria na taaluma ya uhifadhi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa David Mathayo swalii la nyongeza.

MHE. DKT. DAVID M. DAVID: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niulize maswali mawwili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wangu wa Kata za Kisiwani, Vumari na Mji Mdogo wa Same wamebanwa sana na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi; na kwa kuwa Mwenyezi Mungu wakati anaumba dunia alimuumba binadamu akamwambia atawale viumbi vyote viishivyo kwenye maji na kwenye nchi kavu; na kwa kuwa wakati wa uhuru tulikuwa na idadi ya watu milioni 10.3 na sasa hivi tuko takribani milioni 50, tulikuwa na ng'ombe milioni nane sasa hivi milioni 28; tulikuwa na mbuzi milioni 4.4 sasa hivi ni milioni 16.6; tulikuwa na kondoo milioni tatu na sasa hivi ni milioni tano, tulikuwa na nguruwe 22,000 sasa hivi ni milioni mbili, *astaghfillillah* nimetaja nguruwe wakati ni mwezi wa Ramadhan, mnisamehe sana. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba uulize swalii tafadhali.

MHE. DKT. DAVID M. DAVID: Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza je, Wizara ya Maliasili na Utalii iko tayari kushirikiana na Wizara ya Kilimo, TAMISEMI pamoja Ardhi ili waweze kutathmini eneo na idadi ya watu pamoja na mifugo wanayofuga ili kusudi kama kuna uwezekano maeneo ya hifadhi za misitu pamoja na Hifadhi za Wanyamapori

zipunguzwe ili binadamu waweze kupata maeneo ya makazi pamoja na mifugo na kilimo?

Swali la pili, kwa kuwa Botswana, Afrika ya Kusini na Namibia wameweza kuzuia wanyamapori kutoka kwenye mapori kwenda kwa binadamu ama kwenye wanyama wanaofugwa, je, Serikali iko tayari sasa kuandaa mpango rasmi wa kuweka *fence* ili wanyamapori wasiweze kwenda kwenye makazi ya watu kuwasumbua na kuwalettea madhara ikiwa ni pamoja na vifo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza Mheshimiwa Mbunge anazungumzia upungufu wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya kibinadamu hasa kwa ajili ya faida ya kiuchumi na kijamii, akihusisha na uhaba au upungufu wa rasilimali ardhi kwa ajili ya shughuli hizo zinazotokana na ongezeko la binadamu na wanyama kama ambavyo amewataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi Serikali inatambua na kwa kweli ni dhamira ya Serikali kuwafanya wananchi waweze kufanya kazi za kuzalisha mali kwa sababu ni kwa kufanya hivyo tu peke yake ndiyo hata madhumuni makubwa kabisa ya Serikali ya kuiondoa nchi kutoka katika uchumi wa chini kwenda uchumi wa kati yatafanikiwa, ni kwa kufanya kazi tu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi waweze kufanya kazi lazima waweze kuwa na ardhi au wawe na maeneo ya kufanya kazi. Kabla hatujaanza kusema kwamba maeneo tunayoyatumia hayatoshi ni lazima kwanza tuone maeneo hayao yanatumikaje hivi sasa, kwa hiyo, hapa ndipo ambapo tunazungumzia juu ya suala la mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Kuhusu swali lake tutashirikiana vipi na Wizara nne zile alizozitaja ukweli ni kwamba Mheshimiwa Mbunge

anafahamu kwamba tayari tunayo Kamati ya Kitaifa ya Wizara alizozitaja ambayo iko kazini inashughulikia suala hilo na baada ya utafiti wa kitaalam, baada ya kujiridhisha kitaalam tutapitia upya sheria na kuona katika kila eneo kama kweli suluhihisho pekee la kuweza kuwafanya wananchi kupata eneo la kufanya shughuli za kibinadamu kama suluhihisho pekee ni kugawa maeneo ambayo yamehifadhiwa kwa faida ambazo tunazifahamu ziko lukuki, basi Serikali itazingatia mwelekeo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kutajitokeza ukweli kwamba bado maeneo tulionayo tunaweza kuyatumia vizuri zaidi bila kuathiri maeneo yaliyohifadhiwa basi hatutakuwa na haja ya kupunguza maeneo ya hifadhi isipokuwa tutajiimarisha zaidi katika kutumia vizuri zaidi maeneo ambayo hayajahifadhiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili juu ya kuweka *fence*, kuweka uzio kwa ajili ya kuzuia wanyamaporii kwenda kwenye maeneo ambayo ni ya binadamu, kwa ajili ya maeneo ya makazi ya binadamu na maeneo ambayo binadamu wanafanya shughuli za kibinadamu za kiuchumi na kijamii; napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba huko ambako anazungumzia kwamba udhibiti umefanikiwa njia iliyotumika siyo hii tu peke yake ya kuweka *fence*, njia ya kuweka *fence* ni mojawapo na inatumika tu pale ambapo ni lazima kuweka *fence* kwa sababu njia hii ni ya gharama kubwa na si rafiki pia kwa mazingira hata kwa wanyama wenyewe na hata kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kwa sasa hivi ni kwamba Serikali inalichukua suala hili na kwa kweli tumekuwa tukilifanyia kazi muda mrefu kuweza kuona ni namna gani tunaweza kudhibiti kiwango na kasi ya Wanyamaporii kutoka kwenye maeneo yao na kwenda kwenye maeneo ambayo ni ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi hapa vilevile na binadamu na wenyewe tusiendelee na utaratibu ule wa

kwenda kukaa kwenye maeneo ambayo aidha ni njia za wanyapori au ni maeneo ya mtawanyiko ya wanyamaporii.

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wetu hauruhusu kwa hiyo nitawapa watu wawili tu nitampa Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Shangazi.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la hifadhi ya Mlima Kilimanjaro una eneo la *Half Mile* au 0.8 ya kilometa, huduma za jamii kwa mfano uvunaji wa majani, uvunaji wa kuni kusafisha vyanzo vya asili vya maji, kwa mfano mifereji, inahusu vijiji 42 vya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi. Wakati huu hakuna mahusiano mazuri kati ya wananchi wa vijiji hivi 42 pamoja na Hifadhi chini ya *KINAPA* hasa wale askari. Serikali haionti ni vema pande zote zinazohusika yaani wawakilishi wa vijiji pamoja na *KINAPA* ikisimamiwa na Serikali kuweka taratibu na kanuni endelevu zinazoaminika za mazingira ya kisasa ili mahusiano mema kati vijiji 42 na Hifadhi ya Mlima Kilimajora viweze vikawa vya mazingira ya kisasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri naomba majibu kwa kifupi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi kabisa Serikali inazingatia ukweli kwamba ili uhifadhi uwe endelevu ni sharti wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi husika, wanaopakana nazo waweze kuona kwamba wao ni sehemu ya huo uhifadhi kwenye hayo maeneo yanayohusika.

Kwa hiyo, njia zote zinazotumika katika kukamilisha malengo ya uhifadhi ni lazima ziwe rafiki kwa wananchi ambao wanazunguka kwenye maeneo hayo. Kwa sasa Serikali inachokifanya ni kuanzisha taratibu za kuwasogelea wananchi kwa ukaribu kabisa na kuwashirikisha, kuwapa elimu kwanza ya manufaa ya uhifadhi wenyewe, pia kuona

namna gani wanaweza kushiriki kwenye jitihada za Serikali za kuhifadhi, muhimu zaidi mwishoni kabisa ni kuona namna ambavyo wananchi hawa wanaweza wakanufaika na uhifadhi moja kwa moja ukiacha ule utaratibu wa kunufaika na uhifadhi kwa njia na taratibu za kawaida za Kiserikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi swali fupi la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati anajibu suala la Mbuga ya Mkomazi na Mbuga ya Mkomazi kwa Mkoa wa Tanga kuna Wilaya ya Lushoto, Korogwe na Mkinga. Tatizo la mipaka hata kule linatuathiri na kuna timu sasa inapita kutathmini hilo tatizo, nataka nitambue, je, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili imeshirikiana na hawa watalaamu ambao wanapita kutathmini ile mipaka, hasa katika eneo la Mwakijembe Wilaya ya Mkinga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi naomba urudie swali Mheshimiwa Naibu Waziri hajaelewa vizuri, kwa ufupi tafadhali.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mbuga ya Mkomazi kwa Mkoa wa Tanga iko katika Wilaya za Lushoto, Korogwe na Mkinga na hili tatizo la mipaka sasa hivi kuna timu ya ambayo iko chini ya *RAS* kwa kule Tanga inafuatilia haya maeneo yenye migogoro ambayo wananchi na mbuga wanakinzana hasa eneo la Mwakijembe katika Halmashauri ya Mkinga, je, Wizara ya Maliasili na Utalii inatambua uwepo wa hii timu ambayo inakagua mipaka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri umelielewa naona swali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa timu hiyo inayokagua mipaka.

Lakini Mheshimiwa Mbatia nafikiri wakati nikiwa namjibu swalí alikuwa anasisitiza lini nilimuona wakati anataoka alikuwa anaendelea kuongea anauliza lini, sasa Mheshimiwa Mbatia tukimaliza kikao hiki cha Bunge (Kamati ya Fedha hivi) mimi na wewe tuambatane tukaangalie uhalisia ulivyo halafu tuweke ratiba ya kushughulikia suala hilo.

MWENYEKITI: Ahsante muda siyo rafiki tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla, Mbunge wa Makete sasa aulize swalí lake, kwa niaba anauliza nani?

Na. 423

Mabweni kwenye Chuo cha VETA cha Wilaya ya Makete

MHE. EDWARD F. MWALONGO (K.n.y MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING) aliuliza:-

Chuo cha Ufundı Stadi (VETA) katika Wilaya ya Makete hakina mabweni hivyo kunufaisha kata moja tu wakati watoto wanaotoka Tarafa za Matamba, Ikuwo, Magoma, Bulongwa, Ukwama na Kata za Lupila na Tandala hawawezi kunufaika na Chuo hicho kwa sababu ya umbali uliopo.

Je, ni lini Serikali itakipa chuo kipaumbele cha kujengewa mabweni?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swalí la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla King, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi

250,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha VETA cha Makete. Mkandarasi Tanzania *Building Agency (TBA)* anategemewa kuanza ujenzi kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2017 baada ya kukamilisha hatua za kusaini mkataba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalongo swali la nyongeza kama unalo.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza ninalo. Je, Serikali ina mpango gani ya kuwasaidia vijana wanaohitimu mafunzo ya ufundi kama hao wa Makete kupata angalau vifaa tu vya kuanzia kazil?

Swali la pili, Halmashauri ya Mji Njombe ina shule za sekondari 22 na zoezi hili la kujenga Vyuo vya Ufundii linaonekana sasa kwa Serikali limekuwa gumu sana na linakwenda pole pole sana.

Je, Serikali ipo tayari kupokea ushauri, sasa ianze kuzibadilisha baadhi ya shule za sekondari kuwa shule za ufundi ili kusudi vijana wetu walio wengi watakaokuwa wanahitimu Kidato cha Nne waweze kuwa mafundi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kimsingi ni kwamba VETA imekuwa ikifanya hivyo baada ya kumaliza mafunzo ya ufundi kwa baadhi ya wanafunzi wanaohitimu wamekuwa wakipewa vifaa kwa ajili ya kuanzia shughuli zao za kiufundi, pia kusaidia kutengeneza *clusters* za hao wanaokuwa wamehitimu pamoja na wengine ambao wamekuwa wamehitimu mafunzo ya ufundi siyo tu kuititia VETA hata kuititia kwa wananchi wa kawaida, tunawatambua na kuweza kuwapa vifaa, vilevile kuwatambua rasmi na kuweza kuwapa yeti.

Swali la pili la kuweza kubadilisha shule ziwe za ufundi, Wizara tayari tumeshalionia hilo na tunafikiria kubadilisha baadhi ya shule za sekondari hasa zilizokuwa shule za ufundi kama Ifunda, Mtwara, Tanga, Bwiru na shule ya Musoma ili ziweze kuwa vyuo vitakavyoweza kutoa mafunzo kwa ajili ya *technicians*.

Kwa hiyo, muda ukikamilika tutafanya hivyo na kwa mwaka huu tunategemea tuanze kujenga shule mbadala kwa sababu shule hizi zinachukua wanafunzi wa sayansi kwa kidato cha tano na sita na *form one* mpaka *form four* tunawajengea shule yao ili hayo majengo ambayo ni muhimu sana kama *workshops* yaweze kutumika kwa Vyuo vya Ufundi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda hauturuhusu na maswali ya nyongeza tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Waitara.

Na. 424

Ufufuaji wa Kiwanda cha Tairi - Arusha

MHE. MWITA M. WAITARA (K. n. y. MHE. SAED A. KUBENEÀ) aliuliza:-

Serikali imetangaza kukabidhi rasmi kazi ya kufufua kiwanda cha kutengeneza tairi cha Arusha kwa Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) baada ya kusitisha rasmi uzalishaji mwaka 2009.

Je, mpaka sasa kazi ya kufufua kiwanda hicho imefikia wapi na inatarajiwa kugharimu fedha kiasi gani?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kiwanda cha kutengeneza matairi cha Arusha kilisimamisha uzalishaji mwaka 2009 kutokana na Serikali kukosa fedha kwa ajili ya kukiendesha na mbia mwenza (Kampuni ya *Continental AG*) hakuwa tayari kuendelea kuwekeza katika kiwanda hicho. Hivyo, Serikali iliweka dhamana ya kukisimamia kiwanda hicho chini ya *NDC*. Dhamira ya Serikali hivi sasa ni kuona kiwanda hicho kinaanza kuzalisha matairi mapema iwezekanavyo.

Mpaka sasa Serikali imenunua asilimia 26 ya hisa zilizokuwa zinamiliikiwa na mbia mwenza na hivyo kukifanya kiwanda hicho kumiliikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Ili uwekezaji mpya katika kiwanda uwe wenyetija, katika mwaka 2016/2017 Serikali imefanya utafiti wa kubainisha aina ya teknolojia itakayotumika, uwezo wa uzalishaji, upatikanaji wa malighafi, upatikanaji wa soko na athari za mradi na teknolojia itakayotumika kwa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya awali imebaini kuwa kwanza, mitambo iliyopo ambayo ilifungwa kwenye miaka ya 1960 ikiwa imetumika haifai kwa uzalishaji wa kiushindani, pili, inatakiwa kufungwa mitambo inayotumika teknolojia ya kisasa itakayowezesha kiwanda kufanya kazi kwa ufanisi na kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Tatu, kiwanda kipanuliwe ili kiweze kuzalisha matairi ya aina mbalimbali na kwa wingi ili kupata faida ya uzalishaji kwa wingi (*economies of scale*). Nne, kiwanda hicho kiundeshwe na sekta binafsi, Serikali ikiwa mbia kwa hisa zinazolingana na rasilimali za kiwanda zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mpango wa Serikali kwa mwaka 2017/2018 kutafuta mbia atakayekidhi vigezo tajwa hapo juu ili uwekezaji uanze.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu yaliyo chini ya kiwango ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Saed Kubenea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza liliuliza kwamba mpaka sasa kasi ya kufufua viwanda imefikia wapi? Kwa hiyo, kwa majibu hayo inahitaji tujue kwamba Waziri yuko tayari kukiriki kwamba kiwanda hiki hana mpango wa kukifufua kwa maelezo aliyotoa hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mpaka sasa anaamini kwamba kauli mbiu ya Serikali ni kuinua viwanda au kuua viwanda? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, majibu kwa ufupi kabisa.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali iliyofanyika imeandikwa kwenye jibu langu ni kufanya utafiti; na mwaka jana nillipewa shillingi milioni 150 kwa ajili kufanya utafiti na umakamilika kwa hiyo kazi niliyopewa nimemaliza. Kazi ya Serikali ni kujenga viwanda na viwanda vitaendeshwa na Sekta binafsi, mwaka unaokuja 2017/2018 nimeomba pesa shillingi milioni 70 tu nitangaze *tendersekta* binafsi ifanye kazi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, muda si rafiki, tunaendelea na tunamalizia na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 425

Pesa Iliyotengwa kwa ajili ya Bwawa la Mkomazi

MHE. MARY P. CHATANDA (K.n. y. MHE. STEPHEN H. NGONYANI) aliuliza:-

Serikali ilitenga shillingi bilioni 13 kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Mkomazi lakini baadaye Serikali ilihamishia fedha hizo Mkoa mwingine.

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha pesa hiyo ili Bwawa lililokusudiwa lijengwe?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2003 na 2004 wananchi wa kijiji cha Manga Mkocheni, kata ya Mkomazi, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe walionesha hitaji la mradi wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa zao la mpunga katika Bonde la Mkomazi. Aidha, mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa wakati huo kupitia Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro ilifanyika upembuzi yakinifu na usanifu wa awali ambapo walibaini kuwa jumla ya shilingi bilioni kumi na tatu zingehitajika kuendeleza Bonde la Mkomazi ikiwemo ujenzi wa bwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Hata hivyo, usanifu huo ulibaini kuwa bwawa hilo lingezamisha Ziwa Manga liliopo katika Kijiji cha Manga, ambalo lina maji ya chumvi ambayo yangeathiri kilimo cha zao la mpunga. Kutokana na changamoto hii mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro ilianza kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu kwa kuepuka kuzamisha Ziwa Manga na kubaini kuwa jumla ya shilingi bilioni 1.5 zingehitajika kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikia azma hii Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2015/2016 ilitenga jumla ya shilingi milioni mia nane kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Mkomazi. Hata hivyo bajeti ya maendeleo kwa fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji ikiwemo Bwawa la Mkomazi haikutolewa na hivyo kusababisha mradi huo kutotekeliza. Sambamba na fedha hizo kutotolewa bado kuna baadhi ya wananchi ambao walikuwa wanaukataa mradi kwa sababu ya maeneo yao kuzamishwa ndani ya maji na hivyo kufanya mazingira ya kutekeleza mradi huo kutokuwa rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi walio wengi wa Kata ya Mkomazi kuitia Mheshimiwa Mbunge bado wanaona umuhimu wa mradi huo na hasa katika hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Wizara yangu kuitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji italiingiza bwawa hili katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza utekelezaji ili hatimaye lengo la Serikali na wananchi wa Mkomazi waweze kuwa na kilimo cha uhakika na hivyo kuwa na usalama wa chakula na kujiongezea kipato kuitia zao la mpunga.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mary Chatanda kama unalo swali la nyongeza.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikubaliani na majibu ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, hayardhishi kabisa. Ukiangalia kwa mtiririko ulioko kwenye majibu haya imesema wazi mwaka 2006/2007 walifanya upembusi na kugundua kwamba shilingi bilioni kumi na tatu ililijika kwa ajili ya mradi huu lakini wakafanya upembusi tena mwaka 2014/2015 ikaonekana shilingi bilioni 1.54 zilitakiwa kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili lakini bado wakafanya mwaka 2015/2016 wakatenga millioni 800.

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba uulize swali.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja naomba utulie. (*Kicheko*)[**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**]

Mheshimiwa Mwenyekiti, walitenga fedha hizi shilingi milioni 800 hazikutoka, halafu mwaka 2016/2017 hawakutenga fedha...

MWENYEKITI: Mheshimiwa imetosha, naomba uulize swali tafadhalii.

MHE. MARY P. CHATANDA: ... 2017/2018 hawakutenga fedha, sasa ni kwa nini wanazungumza uongo? Kwa nini hawakutenga fedha katika miaka miwili hii ambayo imo mpaka bajeti ya safari hii wanazungumza...

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba uulize swalii tafadhalii.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili...Taarifa kwenye swalii?

T A R I F A

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mama Sitta, taarifa.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi naomba kwa heshima na taadhima mpenzi wangu, ndugu yangu Mheshimiwa Mary Chatanda ufute hilo neno la kusema tulia, nakuomba. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwenye maswali imeanza lini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mary.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimeteleza ulimi ni kwa ajili ya hasira, tusameheane.

MBUNGE FULANI: Ametukana kitii huyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mary, umeshauliza swalii?

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili sijaauliza.

MBUNGE FULANI: Hajafuta kauli yake, afute kauli.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nimefuta.

MBUNGE FULANI: Amezoea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mary, naomba umalizie swali kwa ufupi tafadhali.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye amekamilika, ulimi inawezekana umeteleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali haioni sasa kwamba kutokutekeleza mradi hii hawawatendei haki wananchi wa Wilaya ya Korogwe hususan Manga Mkocheni?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya shemeji yangu Mheshimiwa Mary Chatanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeonyesha taratibu mbalimbali zilizofanywa na Serikali na kwamba utendaji lazima tufuate tathmini ya wataalam. Sisi kazi yetu ni kutunga sera na kupitisha bajeti, lakini utekelezaji unazingatia taarifa za wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la msingi nimesema kwamba utafiti wa awali ulionesha kwamba bwawa lingejengwa kwa shilingi bilioni 13; lakini tathmini ya kimazingira ikaonyesha kwamba bwawa hilo lingejengwa lingezamisha baadhi ya maeneo na vijiji vya wananchi wa Manga, tusingeweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, Tume ya Umwagiliaji kupitia Mkoa wa Kilimanjaro wakafanya tathmini nyingine upya ambayo kama ingetekelezwa basi hayo maeneo ambayo yangeathirika na bwawa yasingekuwemo, ndiyo maana bajeti sasa ikaja shilingi bilioni 1.5, hilo ndilo

jibu la msingi. Lakini bado tumetenga shilingi milioni 800 mwaka uliofuata 2014/2015 lakini kwa bahati mbaya bajeti haikutoka ndio maana utekelezaji haukufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba malengo yetu ni kuhakikisha tunajenga hili bwawa na ndio maana Serikali ya Chama cha Mapinduzi...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu tafadhalii tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri anamalizia.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: ...imeunda Tume ya Umwagiliaji ambayo sasa kazi yake itakuwa ni kusimamia moja kwa moja suala la utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi hakuna haja ya hasira kazi hii tutaifanya na wananchi wa Manga watapata huduma wanayoihitaji. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umemalizika na tumeongeza ziada kidogo. Waheshimiwa Wabunge, nawaomba m jitahidi sana kuyafupisha maswali yenu, kwa sababu mnapofupisha maswali yakawa ya Kibunge na majibu pia ya Mawaziri na Naibu Mawaziri tutaweza kupata fursa zaidi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa hiyo, sisi tungependa tuwape nafasi wengi zaidi lakini kwa vile maswali yanakuwa marefu tunashindwa kutoa fursa kwa wingi.

Pia napenda niwaombe sana kuna wageni wengi wanakuja wakati huu wa asubuhi wanaangalia namna gani tunaendesha Bunge letu ikiwa mtafanya vurugu na

kuzungumza kwa wingi wakati watu wanauliza maswali au kujibiwa tunaondoa heshima na hadhi ya Bunge letu. Kwa hiyo, naomba sana muache tabia hiyo ili tuende vizuri. Mimi hapa nimewasamehe kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, lakini naomba msiendelee tena. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nina matangazoo hapa, kwanza tunaanza na wageni ambaao wapo Bungeni asubuhi hii. Tuna wageni ambaao wako kwenye jukwaa la Spika, wageni watano wa Mheshimiwa Spika ambaao ni askari wastaa fu waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1939 – 1945 kutoka *Tanzania Legion Clubs*. Askari hao ni Ndugu Rashid Ngonji - Mwenyekiti, Ndugu Maurusi Waruma, Ndugu Damian R. Mchuka, Ndugu Mwajanga Mwankunda na Ndugu Wambura Manyanya, karibuni sana kwa heshima zote katika Bunge letu. (*Makofii*)

Pia tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Ruangwa Mkoani Lindi. Wageni hao ni Ndugu Omari Haji Chembeja na Ndugu Hassan Seif Mkumbanjile, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 69 wa Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* - Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaao ni walimu wanne na wanachuo 65 kutoka Chuo cha Ualimu Bustani, hawa ni wageni wa Naibu Waziri pamoja na Mheshimiwa Waziri, karibuni sana wageni wetu kutoka chuo hiki cha ualimu Bustani.

Kuna wageni 100 wa Mheshimiwa Anna R. Lupembe ambaao ni watoto wa *Sunday School* wa Kanisa la KKKT Ipagala Mkoani Dodoma, karibuni sana watoto wetu wa *Sunday School*. Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ambaye ni Katibu wa CCM Mkoa wa Geita, karibu sana Katibu wetu. Pia tuna wageni walio tembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambaao ni wanachuo sita kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana katika Bunge letu hili. (*Makofii*)

Pia tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Khatib Said Haji ambao ni yatima 10 pamoja na mama yao ambao ye ye mwenyewe Mheshimiwa Khatib Said Haji anawalea na kuwatunza, karibuni sana; naona walivyopendeza hongera sana Mheshimiwa Khatib na Mungu akujazie yeny e kheri. Tunaendelea, pia tuna wageni wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Makunduchi ambao ni mtoto wake pamoja na ndugu yake, kwa hiyo naomba na wao tuwakaribishe sana katika Bunge letu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo ya wageni, nawakaribisha wote kwa pamoja katika Bunge letu na karibuni tena kwa mara nyingine.

Kuna wageni wa mwisho ni Dkt. Muhajir Kachwamba pamoja na Ndugu Abubakar Muhajir nao pia hao naomba niwakaribishe katika Bunge letu hilli.

Mwisho kabisa kuna tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa imani ya kikristo. Waheshimiwa hawa wanatangaziwa kuhudhuria ibada katika eneo la wazi la *basement* leo Jumanne siku ya tarehe 20 Juni, 2017 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana. Aidha, katika ibada hiyo tutakuwa na Mtumishi wa Mungu, Mchungaji David Mbaga wa Kanisa la Waadventista la Dodoma. Kwa hiyo, naamini mmelisikia hilo tangazo ndugu zangu waumini wakristo. Baada ya kusema hayo sasa naomba nimpishe Mheshimiwa Spika ...

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: ...ili aendeleee.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Namkaribisha sasa Mheshimiwa Spika aendeleee na shughuli inayofuata. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Mwongozo waMwenyekiti.

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Lakini kabla ya kuendelea naomba leo ni siku kidogo ya kipekee, miongozo yote tuifanye kesho. Nina mambo mawili tu madogo, la kwanza jioni kuwahi, kwa sababu ya zoezi la Kikatiba la kupiga kura kwa ajili ya bajeti. Kwa hiyo, tunaomba saa kumi kamili jioni wote tuwepo kwa sababu tunaanza *immediately* saa kumi tunaanza zoezi hilo mara moja, kwa hiyo, nawaomba wote muwepo mapema kabisa kadri inavyowezekana.

Jambo la pili ni kwamba baada ya zoezi hilo la jioni kutakuwa na futari ya Spika, pale mahali petu, na hiyo futari hajapata kutokea, kwa hiyo, matarajio yangu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wote, watumishi wa Bunge na wageni wetu watakaokuwepo jioni hiyo tuungane pamoja pale kwenye futari. (*Makofii*)

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Sasa ni wakati wa kuhitimisha hoja. Waheshimiwa Wabunge tusikilize hoja zetu namna zinavyojibowi na Serikali na nitaanza na Waheshimiwa Mawaziri, halafu baadae nitamuita mtoa hoja.

Waheshimiwa Mawaziri, muda wetu ni mdogo, kwa hiyo ukipata nafasi moja kwa moja itumie vizuri kwa sababu dakika zenyewe ni chache. Tunaanza na Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa dakika tano na atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NIASHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze na mimi kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa waliyofanya, pamoja na Katibu Mkuu. Hata hivyo, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna anavyosimamia rasilimali za nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yako mambo ambayo yamezungumzwa kwa wingi sana katika bajeti hili na yanahu sana kwa kiasi kikubwa Wizara ya Nishati na Madini. Hata hivyo nitajielekeza sana kwenye hoja za nishati kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la *LNG*, suala la kiwanda cha kusindika gesi; Waheshimiwa Wabunge wameuliza kama mradi upo ama haupo.

Mheshimiwa Spika, nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba mradi wa *LNG* wa Lindi bado upo na wala hautahamishwa, hauendi Msumbiji wala sehemu yoyote. Na hapo tulipofika sasa tuko katika utekelezaji na tarehe 24 mwezi huu watalaaam wanaondoka kwenda Trinidad & Tobago kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo na wajenzi; na wajenzi watakaojenga ni makampuni makubwa ya *ExxonMobil*, *BG Shell*, pamoja na *TPDC*. Kwa hiyo, mradi huo upo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lipo suala la ujuzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanga.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kutoa taarifa kwa sababu ni suala la maendeleo, tunajenga viwanda. Utaratibu

wa ujenzi wa bomba hili umeshaanza na sasa nitoe taarifa sahihi kwamba bomba hili litafika katika mikoa minane ya nchi yetu na wilaya 24 na urefu wa kilometa 1,445 kwa kiasi kikubwa katika Tanzania. Hatua inayofuata katikati ya mwezi unaokuja tutasaini, lakini pia tutafanya uzinduzi na ujenzi wa jiwe la msingi huko Tanga katika eneo linaloitwa Chongoleani, Mjini Tanga. Kwa hiyo, ujenzi unaanza na utekelezaji utakamilika mwaka 2025. Kwa hiyo, Ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Makambako Songea; huu ni mradi muhimu sana. Wananchi walio wengi wa maeneo ya Mikoa ya Njombe, Songea na Wilaya zake wanautarajia sana mradi huu, uko katika hatua nzuri. Hata hivyo niseme tu *commitment* ya Serikali, kwa mwaka huu wa fedha tumetenga bilioni kumi na moja kwa ajili ya kwenye mradi huu, na ujenzi umeshaanza kufika katika hatua nzuri na mwezi Oktoba mwakani utakamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini niwaambie tu shughuli kubwa zinazofanyika katika mradi huu, ya kwanza kabisa ni ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vilivyoko Madaba, Njombe pamoja na Songea Mjini na utakamilika hivi karibuni. Mradi mzima utagharimu *Swedish Krona* milioni 620, Dola za Marekani milioni 20 na shilingi bilioni 17 za Tanzania. Kwa hiyo, utekelezaji ukwenda vizuri mwezi Agosti mwakani utakamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mradi huu kazi zitakazofanyika ni pamoja na kujenga *transmission line* ya urefu wa kilometa 250 kutoka Njombe hadi Songea, *transmission* ya kusambaza umeme katika vijiji 120 katika Wilaya nilizozitaja na kuwaunganishia umeme wateja 22,700. Kwa hiyo ni mradi mkubwa na unakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kusambaza Umeme Mjini, maana wako Wabunge wamehoji kwamba tunapeleka umeme vijiji tu lakini mjini hatuendi. Niseme tu kwamba tumepata Dola za Kimarekani milioni 424 kwa ajili ya ujenzi na miundombinu ya mijini ili kuhakikisha kwamba

mijini tunakuwa na umeme wa kutosha ili viwanda vinavyojengwa mijini sasa viwe endelevu na kazi hii inafanyaika vizuri. Kazi zitakazofanyaika, ili nitumie nafasi hii vizuri, sana sana ni ufungaji wa transforma kubwa na ndogo zinazoanzia KVA 50, KVA 100, KVA 200 hadi KVA 315. Hii ni katika kuhakikisha kwamba umeme mijini pia unaimarika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *REA* Awamu ya *Tatu*; ninatambua kwamba muda ni mfupi sana, lakini niwape taarifa Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe 24 Juni (kesho kutwa tu) tunaanza sasa uzinduzi rasmi wa mradi mkubwa wa *REA* Awamu ya *Tatu* katika mikoa yote Tanzania Bara. Tunaanza na Mkoa wa Manyara tarehe 24, tarehe 4 hadi 5 tunakwenda Katavi na Rukwa, tukitoka Katavi na Rukwa tunaenda Mtwara na Lindi halafu tunaenda Kigoma. Kwa hiyo, wananchi wa Kagera Nkanda, Kazumulo pamoja na kule Kagera tutaendelea kuzindua hadi mikoa yote ikamilike kwa muda mfupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda ni mfupi, lakini niendelee kuzungumza kidogo suala la usambazaji wa gesi majumbani.

Mheshimiwa Spika,...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzunguzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini, Dkt. Merdad Matogolo Kalemani. Kama nilivyosema mwanzo, sasa anaafuata Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvubi, Dkt. Charles John Tizeba.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikushukuru sana kwa kunipa nafasi

na mimi kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Hoja ya Bajeti ya Serikali iliyoko mbele yetu.

SPIKA: Dakika tano pia.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kusema tu kwamba naunga mkono hoja na baada ya kuunga mkono hoja niseme pia kwamba bajeti hii imeitendea haki sana sekta ya kilimo nchini. Ninaposema sekta ya kilimo ni kwa maana ya sekta ya kilimo, mazao, mifugo na uvuvi na pia sekta ya ushirika hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la tozo, pamoja na kwamba wako walioonekana kama hawaridhiki na ufutaji wa tozo na kodi mbalimbali katika kilimo, lakini sisi tunaovaa kiatu ndio tunajua kilikuwa kinatubana kiasi gani, na kwa maana hiyo tunatarajia kwamba tozo na kodi mbalimbali ambazo zimeondolewa zitaongeza tija katika kilimo, lakini pia zitaweka mazingira mazuri ya wadau wote wa kilimo *ku-participate* (*kushiriki*) bila kukwazwa na mazingira hayo ya kodi na ushuru mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wakulima wamekuwa wakilalamikia tozo hizo na wafanyabiashara na watu wengine katika minyororo ya thamani na wao pia wamekuwa wanalamikia tozo hizo. Kwa hiyo, tumeziondoa na Serikali imekubali kuziondoa na kuzifuta baadhi yake, nyingine kuzipunguza ili kuhakikisha kwamba wote wananzaika, *win-win situation*; Serikali ibakie na mambo yake ikinanzaika lakini na wananchi pia wapate nafuu na kunanzaika na jitihada wanazofanya katika mashamba na maeneo mengine ya uzalishaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba baada ya hayo tutaona mabadiliko ya bei ya mazao yetu ya biashara, lakini pia tutaona uzalishaji wa mazao ya kilimo ukiongezeko, tutaona ufugaji ukipata nafuu zaidi baada ya kuondoa kodi hizi na tumeweka mazingira yanayovutia uwekezaji sasa katika mifugo. Eneo hili limekuwa halipati

uwekezaji mzuri kwa sababu ya tozo na ada mbalimbali zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba tunaendelea kama Wizara na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba upatikanaji wa pembejeo unakuwa kwa wakati na kwa bei ambayo wakulima wanaweza kumudu. Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kuondoa tozo zilizokuwako katika uingizaji na usambazaji wa mbolea na viuatilifu. Vilevile tunaendelea na mchakato wa uagizaji wa baadhi ya mbolea kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba mwishowe bei tutakayoiweka itakuwa inahimilika, wananchi wanaweza kuimudu na kwa hivyo ituwezeshe kuongeza uzalishaji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*) imekamilika maandalizi yake na tumefanya mambo kadhaa. Pamoja na mambo tulioyoyafanya ni kutoa Mwongozo wa Kilimo, pia Mwongozo wa Ufugaji.

Mheshimiwa Spika, katika programu hii suala la umwagiliaji limepeewa kipaumbele, na safari hii umwagiliaji tunaoufikiria kuuwekea msisitizo mkubwa ni umwagiliaji wa mazao makuu ya chakula. Kwa muda mrefu umwagiliaji umekuwa katika maeneo ya mpunga na mbogamboga, lakini sasa katika awamu hii ya Programu ya Kilimo ya Pili tunataka kwenda kwenye zao kubwa la chakula nchini ambalo ni mahindi. Umwagiliaji ufanyike pia katika uzalishaji wa mahindi ili kujihakikisha usalama wa chakula na uzalishaji wa muda wote ambao hautuletei mashaka.

Mheshimiwa Spika, niombe kutumia nafasi hii kuwatangazia wananchi kwamba sasa hivi maeneo mengi nchini wanavuna, lakini niwaombe sana baada ya kufanya mavuno hayo utumiaji wa chakula chao uwe wa makini kwa sababu hali ya hewa katika nchi zinazotuzunguka haikuwa nzuri na kwa hiyo, kutakuwa na mahitaji makubwa ya kununua chakula kutoka Tanzania kwenda nchi za nje.

Wananchi hawazuiliwi kuuza lakini wanashauriwa wauze na kuiwekea akiba ya kuwatoshha.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa kilimo, Mifugo na Uvubi, Dkt. Charles John Tizeba, sasa anafuata Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Waziri una dakika saba.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAА NA

MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Awali ya yote naunga mkono hoja na napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Fedha kwa bajeti nzuri na vilevile kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuirejeshea nchi yetu sifa na heshima yake ya zamani, sifa na heshima ya kuthubutu, sifa na heshima ya kupigania haki, usawa, na uhuru bila kigugumizi, bila uoga na bila hata kujali aliyeko upande wa pili, je, ana fedha nydingi, ni mkubwa sana au yukoje. Na msimamo huo dunia nzima ilitambua kwamba hiyo ndio Tanzania. Mwalimu alianza kuonesha sifa hii ya Tanzania mara tu baada ya uhuru baada ya kuiweka nchi yetu kama ngome kuu ya upiganiaji uhuru katika Bara la Afrika na dunia yote ilijua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikukumbushe kitu kimoja kwamba katika hali ya kawaida huwa ni tajiri tu ndiye anayeweza kumuwekea vikwazo mtu maskini, lakini kipindi cha Mwalimu nchi masikini ya Tanzania ilikuwa inawawekea vikwazo hata nchi kubwa. Na ukiwekewa vikwazo na Tanzania una hali mbaya, chukulia mfano Uingereza walipoanza kuchezacheza na haki ya uhuru wa watu wa Zimbabwe, tarehe 16 Disemba, 1965 Tanzania tukavunja

uhusiano wa kidiplomasia na Uingereza na dunia ikaona, *just a question of principle! (Makof)*

Mheshimiwa Spika, tulipoungana na Zanzibar mwaka 1964 Ujerumani wakaanza kutumia ile wanaita *the Hallstein Doctrine* ambayo ilikuwa inasema kama wewe ni rafiki wa Ujerumani Magharibi basi vunja urafiki na Ujerumani Mashariki; Mwalimu akasema *I see, hebu acheni kutuchazea hapa, ondokeni Wajerumani wote.* Hiyo, ndiyo Tanzania, Tanzania ya kuthubutu, Tanzania yenye *principles. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, tulifundishwa na Mwalimu kwamba Nchi hii ili iweze kuendelea hatuhitaji *big brother*, hatuhitaji pesa, hiyo ni akili ya kitumwa, pesa ni matokeo. Tunachohitaji ni vitu vinne tu; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora, huo ndio ulikuwa msingi. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, lakini mjadala wa makinikia au mashapo kwa mujibu wa Kamusi tulioizindua tu hapa jana; mjadala huu ambao umeendelea kwa wiki kama mbili hivi, hauakisi Tanzania ya Nyerere. Wakati wananchi wanaunga mkono na kushangilia uthubutu wa Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kutetea rasilimali za nchi na wao wanaelewa mikataba tulioingia, mchanga unachukuliwa yanaachwa mashimo hapa, hakuna hata makubaliano kwamba basi mkishachenjua kule turudishieni mchanga tuzibe haya mashimo au mtatengenezaje?

Mheshimiwa Spika, tuna makampuni hapa kama *Williamson Diamond*, miaka 77 haipati faida lakini ikiwa Botswana inapata faida, wananchi wanalelewa hilo, lakini sisi wasomi sasa tunasema hapana, jamani tuwe waangalifu, tuwe waangalifu sana! Oooh, wazungu hawa, tuwe waangalifu nao; mimi nashangaa.

Mheshimiwa Spika, sasa ili tuendelee tunahitaji vitu vinne watu, ardhi, siasa na uongozi bora, sasa hivi imebadilika imekuwa ili tuendelee tunahitaji fedha na wazungu, maana tunawaogopa wazungu kupita kiasi, imenitisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, leo hii tuna vita ya kiuchumi, kijana msomi, mwanasheria, unasimama hapa unatutishia nyau! Ooh! Tuna *MIGA* na Wanyakyusa kuna watu wanaitwa kina Minga, wananiuliza hivi huyu Minga ametokea wapi? Tuna *MIGA!* *What is MIGA?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mbunge wa Mwibara hapa, alituletea mkataba hapa, kasoma tu kifungu kimoja, Ibara ya 12, lakini namwambia asome na ya 11, hatuwezi kushindwa kesi chini ya sheria hii ndogo ya *MIGA*, ni mkataba wa kawaida tu kama mikataba mingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Profesa Osoro, ya Mruma ni takataka! Huo ni umamluki wa hali ya juu. Tuko kwenye vita! Tuko kwenye vita hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sio tu *MIGA*, lakini sisi tuna mikataba ya kimataifa inayosimamia *good faith* katika mikataba. Tuna *UN Convention on Contrast for International of Sale of Goods*, tuna *UCC* ambayo ni *Unfair Commercial Code* ambayo tunaitumia, yote inasisitiza *good faith* katika mikataba. *Good faith* inatokea wapi, mikataba hii ya madini ambapo mtu anasema nachukua mchanga wako kwenda kuchenjua, tuna-*calculate percentage* kule, kumbe ameshauza siku nyingi. *There is no good faith!* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *MIGA Convention* yenye we inasema nini; *MIGA* inasema ukitaka kutumia *MIGA* faida yake hapa lazima uheshimu sheria za nchi. Sheria za nchi zinasema nini? Zinasema kwamba ukitaka kuingia mkataba lazima kuwepo na *union of minds*, wanasheria wanajua, tunaita *concensus ad idem*, haiwezekani ikawepo *concensus* wakati wewe unamwambia mwenzako naenda kuchenjua halafu nakokotoa, kumbe huwa kabla ya kuchimba umeshauza hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana nasema hatuwezi hata kidogo kushindwa hiyo kesi. Tuliweza kushinda mtihani wa *Devolution Agreements* wakati wa uhuru, tutashindwa *MIGA*? Tutashindwa *MIGA*? Tukishindwa kesi hii basi

tumezungukwa na Mayuda Iskariote wa kutisha, lakini nashukuru wako wachache sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Devolution Agreements* zilikuwa ni nini, niseme kwa kifupi. Tulipokuwa tunapata uhuru Barani Afrika Waingereza walikuwa wanakuja na mikataba inayosema, mimi nakubali mikataba yote alioingia Uingereza inayonibana inibane mimi kama nchi huru. Ni Mwalimu Nyerere peke yake aliyepeleka *note* ya kukataa hiyo Umoja wa Mataifa akisema mimi nilikuwa sijazaliwa kama taifa huru, mikataba hiyo mliingia kwa hiyari yenu hamkuni-*consult*, mlinitawala bila kibali changu, sitaki kuingia kwenye hiyo biashara; na tangu toka hapo ndipo ikazaliwa dhana katika Sheria ya Kimataifa inaitwa *The Nyerere Doctrine of State Succession* ambayo watu wengi wameifanyia mpaka *Degree za Uzamivu*, hii nchi ina historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Mwalimu uliokoa mengi sana nchi hii. Tulikuwa na *Belbase Agreement* alioingia Mwingereza na Ubelgiji. Mwingereza aliitoa Bandari ya Kigoma na Bandari ya Dar es Salaam kuwapa Wabelgiji waimiliki, tukakwepa kutokana na Mwalimu msimamo wake wa kwamba hatukubali. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana. Ahsante sana, kwa sababu ya muda, tungependa zaidi uendelee kuwasilisha.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, nilishaunga mkono hoja.

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa. Tunaungana nawe Mheshimiwa Waziri, na hata mimi kama Spika naona aibu Waheshimiwa Wabunge wangu wanapodiriki kusema kwamba, ripoti zile muhimu zenye faida kubwa katika nchi yetu ni *profesorio rubbish, ouh!* Ahsante sana, lakini ndio hivyo tena. (*Makofi*)

Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles John Mwijage, dakika saba.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na nichukue fursa hii kuunga mkono Bajeti Kuu ya Serikali, lakini kabla ya hapo nichukue fursa hii kwako wewe Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu kuwakaribisha kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba yanayoanza tarehe 28 Juni, 2017 na yatakwenda mpaka mwezi wa saba tarehe 8 Julai, yakishirikisha nchi za Kimataifa kama 30 na makampuni 2,500. Tutaonesha bidhaa ya Tanzania, bidhaa kama nilizovaa, siwezi kutembea, ninacho kiatu kutoka *Karanga Prison* na hizi nguo kutoka *21st Century Morogoro* na mshonaji ana kiwanda kidogo; kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwakaribisha Sabasaba, mje muone bidhaa ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yaliyozungumzwa kwenye Bajeti ya Serikali Kuu. Bajeti hii ni ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Bajeti hii kwa ujumla wake ni ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, si ya ujenzi wa viwanda tu, ni ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Nichukue fursa hii kuwatoa wasiwasi watu waliokuwa na mashaka kwamba hatutajenga viwanda kwa sababu mwaka uliopita Mheshimiwa Mwijage alitengewa shilingi bilioni 40 akapewa saba, lakini viwanda havitajengwa; la hasha angalia upande wa pili nilipopewa shilingi bilioni 40 zikaja shilingi bilioni saba nimetengeneza viwanda vya shilingi trilioni 5.2, kwa hiyo hayo mambo hayahusiani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika kipindi hicho tumetengeneza miundombinu wezeshi na ile miundombinu saidizi itakayopunguza *transaction cost* na *production cost*, ndipo uchumi utakavyoweza kuchangamka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la viwanda kuna watu wana mashaka kwamba hatujui changamoto za viwanda, si kweli tutendeane haki, kama kuna watu wanajua Serikali hii inajua changamoto zote. Tunajua mimi na Wizara yangu tunakutana na wawekezaji kila siku, pia viko vikao vya ubia kati ya mimi na Waziri wa Fedha tunakutana tukiwa wenza kuzungumza na wawekezaji wote, tunajua changamoto zao. Hata hivyo wawekezaji wanaweza kuwa

na matakwa yao Serikali haiwezi kuyatimiza kwa wakati mmoja. Bajeti hii naipongeza imejibu hoja za Wabunge na wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nawasilisha hapa nilikuja na vitabu vingi, nikawaonesha kitabu kimoja cha mawasiliano yangu mimi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na yote yaliyosemwa ambayo yametokana na Dawati la Wepesi wa Kufanya Biashara ambalo nalisimamia mimi mengi mengi yametekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwaomba wananchi wote wakiwemo Wabunge na wafanyabiasha, tunaanza upya, leteni mawazo yenu kwa kile ambacho mnadhani akikutekelezwa au kile ambacho kimeibuka. Kwa sababu biashara ni *dynamic* siyo *static* upepo unabadijika. Kwa hiyo, leteni mawazo yenu nitayapeleka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mawaziri wengine tutawaalika, tutakutana mara nne kwa mwaka ili kuhakikisha kwamba tunaweza kwenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vivutio vikubwa vya uwekezaji ni mazingira bora ya kufanya biashara, *the easy of doing business*. Naomba nieleze sasa hivi wakaguzi wa wepesi wa kufanya shughuli ndio wanapita kuangalia nchi gani ndiyo inafanya vizuri. Msipige kelele msizungumze kama kwamba nchi hii inawaka moto, hapana, sisi ni miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri ila tuna tamaa ya kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wepesi wa kufanya biashara timu ya Serikali kwa kushirikiana na *private sector* imefanya kazi nzuri na ripoti hiyo ndiyo inafanyiwa kazi, yale yote mliyoyasema yataondolewa. Mheshimiwa Tizeba amesema kuna tozo zimeondolewa lakini tunataka ziondoke zaidi. Tutakwenda hatua kwa hatua Idara za Serikali, Wizara zote na wote wawe tayari kuondoa kile ambacho kila Mtanzania ataona kwamba kinamkwamisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lipo suala la bidhaa bandia na bidhaa zisizokidhi viwango. Nilizungumza kwenye bajeti yangu kwamba ndiyo kazi ninayokwenda kuifanya, hii kazi si rahisi, inahusu *change of mind* na kwamba wale wanaokwenda kukamata na wao lazima uwabadijishe. Hata hivyo niwaambie hakuna jiwe litakalobaki bila kugeuzwa. Kama Jemadari Mkuu anapambana na makinikia mimi nitashindwa je kupambana na panya hawa? Nitapambana nao, bidhaa bandia Tanzania hazitaiingia.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la vifaa vyta vitenzi vinakuja bandia, waende majenerali wapambane kule juu na mimi nitapiga hawa panya.

Mheshimiwa Spika, juu ya aina ya viwanda kwamba sisi hatujui aina ya viwanda hakuna, Mheshimiwa Rais amesema Jengeni viwanda ambavyo vinachakata mallasili au mazao ya wananchi, ndivyo tunavyojenga. Kesho kutwa nakwenda Kibaha, Mkuu wa nchi anakwenda kuzindua kiwanda cha kuchakata matunda. Limeni matunda kuna viwanda vimetengenezwa vyta kuweza kuchakata matunda yote.

Mheshimiwa Spika, lakini msiende mbali sana, hapa Dodoma kuna Kiwanda cha Asante kinaweza kuchakata matunda yote yanayoweza kulimwa Ukanda wote wa Kati, kwa hiyo tunajua, lakini tumeelekeza tuwekeze nguvu katika viwanda ambavyo vinaajiri watu wengi. Ila niwaeleze kiwanda cha vifaa vyta ujenzi kama vigae kinachukua muda mfupi kujengwa kuliko kiwanda kinachoajiri watu wengi. Mpaka sasa nina viwanda ambavyo vikianza kazi Morogoro na Kigoma tutaweza kuzalisha sukari zaidi ya mahitaji ya nchi hii, lakini viwanda vyta namna hiyo vinachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mchengerwa nikuambie umesema, umelalamika nimekusikia, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekusikia, Waziri wa Ardhi amekusikia waliochukua ardhi Rufiji lazima niende nilale nao mbele kama nikishindwa nitapimwa kwa hilo. Ardhi ya Rufiji inaweza kuzalisha sukari, Mbunge anasema njoo Waziri anasema njoo,

nani anapinga? Nakwenda kufanyakazi juu ya Rufiji na Mchengerwa usiache kupinga kelele piga kelele na mimi nakusikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari ya Bagamoyo. Tume ya Serikali imeshapokea ripoti ya mwekezaji kuhusu Bagamoyo, Bagamoyo mwekezaji yuko tayari kumaliza kila kitu. Ni juu yetu sisi Serikali kukubaliana naye ili tuweze kumruhusu aendelee.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru karibu Sabasaba, karibu uone bidhaa ya Tanzania. Kwa mara ya tatu tena naomba kuunga mkono hoja bajeti ya Mheshimiwa Mpango na Mama Kachwamba, twende mbele.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Blashara na Uwezekazaji, Mheshimiwa Charles John Mwijage. Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa kutembelea maonyesho ya Sabasaba mwaka huu, Dar es salaam.

Sasa naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Profesa kwa dakika saba.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia bajeti ya Serikali. Kwanza kabisa nianze kusema ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ninaunga mkono hoja kwa sababu bajeti hii imeitendea haki sekta ya elimu, na bajeti hii inalenga katika kuondoa kero ambazo zimekuwa zikiwasumbua Watanzania kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze hatua ya Serikali ya kuanzisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato (*e-government payment gateway*) ambayo kwa kweli inalenga kuondoa upotevu wa mapato ambao unasababisha Serikali isiweze kuwashudumia wananchi wake ipasavyo. Vilevile napongeza kodi ambazo zimeondolea katika sekta ya elimu katika katarasi za kujibia maswali, lakini vilevile napongeza

hatua ya kuondoa kodi kwa ajili ya vifaa vya wanafunzi wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba nijikite katika kujibu hoja ambazo zilishus sekt ya elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kumekuwa na hoja ambayo imejitokeza kuhusu namna ambavyo Serikali imejipanga katika kuhakikisha kwamba inatatua kero za wanafunzi wenyewe mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie tena Bunge lako Tukufu kwamba utatuaji wa kero za wanafunzi wenyewe mahitaji maalum ni kipaumbele namba moja cha Serikali ya Awamu ya Tano, na tayari hatua za kutatua matatizo hayo zimekwisha chukuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyopita tulinunu vifaa ambavyo vimesambazwa katika shule na Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakaangalia katika kitabu changu cha bajeti kielelezo namba 8 hadi 10 kimeonyesha mgao wa vifaa vilivyonunua na kwa Waheshimiwa Wabunge amba hamkuapa katika awamu hii ni wahakikishie kwamba katika bajeti hii ambayo leo tunaipigia kura zimetengwa fedha kwa ajili yakuhakikisha kwamba ile mikoa na shule ambazo hazijapata zitapatiwa vifaa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Ukaguzi. Limezungumziwa hapa suala la kuboresha ukaguzi ili kuwa na ufanisi zaidi. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inatambua kwamba Idara ya Udhibiti Ubora ndio jicho la Serikali katika sekt ya elimu; kwa hiyo kwa namna yoyote ile Serikali itahakikisha kwamba inaboresha. Hatua ambazo tumezichukua ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunanunu vitendea kazi, tunafahamu kwamba mazingira ya Wadhibiti Ubora hayakuwa mazuri. Katika bajeti ya sekt ya elimu tumetenga fedha kwa ajili ya kujenga ofisi 50 pamoja na kununu vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, vifaa peke yake haviwezi kuleta ufanisi inatakiwa pia na watu ambao ni mahiri katika kufanya kazi. Mfumo mzima wa Ukaguzi katika sekta ya elimu tutaungalia kwa kuhakikisha kwamba tunakuwa na ufanisi zaidi. Kwa sababu mfumo wa sasa ambapo Mkaguzi wa Shule za Msingi hawezi kukagua shule za sekondari umepitwa na wakati kwa sababu kila ilipo shule ya msingi jirani yake kuna shule ya sekondari. Kwa hiyo, tunaangalia mfumo mzima na tumetengeza kihunzi cha ukaguzi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na mfumo ambao ni fanisi zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imezungumziwa katika sekta ya elimu ilikuwa inahusiana na mazingira ya miundombinu katika sekta ya elimu. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya awamu ya tano imeweka dhamira ya dhati na katika bajeti hii tumeweka mikakati ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha mazingira katika sekta ya elimu kuanzia vyuo vya ualimu pamoja na vyuo vyetu vikuu. Kama tulivyofanya katika kujenga mabweni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tutaendelea na katika taasisi zetu nyingine za elimu ya juu ili kuhakikisha kwamba vijana wa Kitanzania wanapata elimu yao katika mazingira ambayo ni mazingira tulivu na ni rafiki katika kujifunza.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tutaendelea kuimarisha mazingira katika sekta ya elimu. Niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wanaozungumzia mazingira ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwamba tuna mpango wa kujenga shule maalum ya kisasa katika Chuo chetu cha Walimu cha Patandi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ili chuo kiwe karibu na mahali ambapo mafunzo ya walimu yanatolewa kwa lengo la kuhakikisha kwamba mafunzo ya walimu ambao wanahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum yatolewa kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeongelewa ni suala la kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi. Niseme kwamba jirani yangu hapa Mwijage ambaye

anajenga viwanda hawezi akafanikiwa kama sijampa raslimaliwatu ya kutosha. Wizara yangu inalitambua hilo na tumeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kamba tunakwenda sambamba na dhamira ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyo ongea Chuo cha Ufundji Arusha Kimesha andaa kozi mahususi kuhakikisha kwamba Watanzania wananaufaika na fursa ya kujenga bomba la mafuta ambazo nchi yetu imepata katika mazingira ya ushindani mkali. Kwa hiyo, tunaanda kozi ya kuwezesha vijana wetu kuwamahiri katika ujenzi wa bomba na vilevile katika nyanja nyingine zozote ambazo zinahusiana na viwanda vinavyoanzishwa. Tunafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Viwanda na Biashara wanatupatia mahitaji na Wizara yangu hatulali tunahakikisha kwamba tunaweka mazingira fanisi ya kuweza kuhakikisha kwamba tunatoa mafunzo yanayoendana mahitaji.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa *VETA* katika wilaya na katika maeneo yetu limekuwa likuzungumzwa, sana na niserde kwamba zile *VETA* ambazo ziliikuwa zijengwe kwa ufadhili wa *ADB* tangu mwaka 2015 kulikuwa na changamoto ambazo Wizara yangu ilikuwa inapatia uvumbuzi na niwashakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba zile *VETA* zote ambazo ziko katika mchakato wa kujengwa tutahakikisha kwamba katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 tunazikamilisha ili tuweze kupata fursa ya kuweza kujenga maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa uchache hayo ndijo ambayo yalzungumziwa katika sekta ya elimu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kama nilivyosema ni bajeti nzuri ni bajeti ambayo inaenda kuondoa kero katika sekta ya elimu lakini pia ni bajeti ambayo itawezesha kuimarisha mifumo ya elimu. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sasa nimuite Mheshimwa

Ummu Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa dakika saba.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza na mimi niseme naunga mkono hoja. Lakini pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kusimamia vyema raslimali zetu za nchi.

Mheshimiwa Spika, kadiri tunavyosimamia fedha za nchi maana yake tunawekeza pia katika kuboresha huduma za jamii ikiwemo huduma za afya. Nitoe mfano bajeti ya dawa ya Serikali mwaka 2015 ilikuwa shilingi bilioni 24 mwaka 2016 shilingi bilioni 251, mwaka 2017 tunazungumzia takribani shilingi bilioni 269; kwa hiyo kuna watu wanatakiwa waangalie uhusiano wa hatua ambazo tunachukua katika kusimamia raslimali za nchi, lakini pia katika kuboresha huduma za jamii ikiwemo huduma za afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuititia jitihada za Mheshimiwa Rais tumeona kwamba kwa mara ya kwanza hakuna Mtanzania mgonjwa atakuwa analala chini kwa sababu tu ya ukosefu wa vitanda au magodoro. Endapo mgonjwa atalala chini ni kwa sababu hospitali au kituo hicho hakina sehemu ya kuweka vitanda au magodoro, hizi zote ni juhudzi za Mheshimiwa Rais, Dkt.John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais akisambaza vifaa katika halmashauri zote nchini haijawahi kutokea katika historia ya Tanzania. Tumeona kwa mara ya kwanza *ambulance* zaidi ya 67 Mheshimiwa Rais akizisambaza nchi nzima, haijawahi kutokea katika historia ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Dkt. Mpango na Naibu Waziri, wifi yangu Dkt. Ashatu Kijaji na wataalamu wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri waliyofanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya tutanufaika sana na bajeti hii ambayo inapendekezwa. Kwa mfano Suala la kuendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 katika sukari ya viwandani maana yake ni kwamba tunawekeza katika utengenezaji wa dawa, viwanda vyta dawa vinatumia pia sukari ya viwandani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango tunakupongeza sana kwa sababu asilimia 80 ya mahitaji yetu ya dawa tunayanunua kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, sasa hivi tunataka kuhakikisha kwamba dawa zinatengenezwa ndani ya Tanzania, hii ni hatua nzuri na tunaipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunapongeza bajeti hii kwa sababu imefuta ada ya kuanzisha maduka ya dawa. Tumesema *MSD* haiwezi kuwa na dawa aina zote kwa asilimia 100; kwa hiyo, lazima yawepo maduka binafsi ya dawa. Mheshimiwa Mpango tunakupongeza kwamba umefuta ada ya kuanzisha maduka ya dawa maana yake dawa zitapatikana katika vijiji, katika mitaa yetu na katika makazi yetu. Dawa si biashara, dawa ni huduma tunawapongeza sana Wizara ya Fedha kwa kuliona suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ambalo tunaona sekta ya afya tutanufaika sana na bajeti hii ni suala la kuwatambua rasmi wafanyabiashara wadogo wadogo wamachinga, mama ntilie, maana yake tutakapowatambua ndiyo pia itakuwa rahisi kwetu kuwafikia katika huduma za *social security* (huduma ya hifadhi ya jamii) na hapa nazungumzia bima ya afya. Endapo wafanyabiashara hawa wadogo tutaweza kuwatambua maana yake pia itakuwa rahisi kwetu sisi kuwafikia na kuwahimiza wajijunge na bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya kupata huduma za afya kwa Watanzania ni suala la gharama ya fedha, kwa hiyo tunahimza wananchi wote wajijunge katika mifuko ya bima ya afya ili sasa iwe rahisi kupata dawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nilitaka kupongeza bajeti hii ni suala pia la kufuta tozo katika mabango ambayo yanaonesha zahanati, sehemu za

huduma, vituo vya afya na hospitali, hili ni jambo zuri kwa sababu litakuwa pia ni rahisi kwa wananchi hasa kwa wakati wa dharura kuhakikisha kwamba wanapata huduma za afya kwa wakati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi sasa nijikite katika kujibu hoja tatu ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Hoja ya kwanza imeongelewa na Mheshimiwa Lucy Mayenga, naye alikuwa anazungumzia kuhusu utendaji kazi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, na kwamba kuna kampuni inaitwa *Techno Net Scientific Limited* ambayo inaingiza kemikali bila kufuata sheria. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Lucy Mayenga, tunakuballiana kwamba ndiyo changamoto hii ipo lakini tumeibaini na sasa hivi tayari Mkemia Mkuu wa Serikali anashirikiana na vyombo vingine vya dola kuhakikisha kwamba tunampeleka mahakamani haraka iwezekanavyo Kampuni hii ya *Techno Net Scientific* ambayo inajihuisha na shughuli za kuhifadhi na kuuza kemikali za viwandani na majumbani wakati usajili wake umeisha toka tarehe 30 Aprili, 2016. Kwa hiyo, Mheshimiwa nikuthibitishie kwamba uchunguzi umekamilika na ndani ya muda mchache tutampeleka mahakamani mhusika.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge hili kutoa onyo kwa wote wanaojihuisha na kuingiza kemikali za viwandani na majumbani kuhakikisha kwamba wanazingatia sheria.

Mheshimiwa Spika, mwezi wa tisa tulikuja Bungeni tukaleta sheria ya kuibadilisha Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali iwe Mamlaka (*Authorty*) maana yake ni kutaka kuipa nguvu na uwezo wa kuweza kusimamia shughuli zake mbalimbali ikiwemo kusimamia kemikali za viwandani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lucy Mayenga nikusihi dada yangu kwamba ndugu yangu tusiifute hii ofisi kwa sababu licha ya kusimamia shughuli za kemikali, lakini pia ina majukumu mengine ya kuhakikisha inasimamia Sheria ya Teknolojia ya

Vinasaba, lakini pia inajihuisha na sheria zinazohusika na vilelezo za sampuli katika makosa ya jinai na Mheshimiwa Mwingulu anaitegemea sana katika kukamilisha mashauri mbalimbali ya kijinai ikiwemo Mahakamani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo limeelezwa na Mheshimiwa Mbunge Aeshi Hilaly ni suala la uvutaji shisha, kwamba je shisha ina madhara gani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika,...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

Kabla hatujaendelea kuna wangeni ambao walisaaulika kutangazwa nao ni wachungaji 16wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kutoka Geita, ahsante sana. Wachungaji hawa wanatoka *Pentecostal Assemblies of God, Geita*; wachungaji karibuni sana Dodoma, mtuombee. (*Makof!*)

Tunaendelea na uchangiaji sasa ni Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora; Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki kwa dakika saba.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi naanza moja kwa moja kwa kuunga mkono hoja hii, na kipekee namshukuru sana Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake, Makatibu Wakuu na uongozi mzima wa wizara kwa kuja au kwa kuandaa bajeti hii nzuri sana ya Serikali kwa mwaka 2017/2018. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na wasemaji waliotangulia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amekuwa akisimamia rasilimali zetu,

maliasili na madini katika kuhakikisha kwamba zinatumika kwa manufaa ya taifa letu. Waheshimiwa Wabunge kama tutakumbuka mwaka 2015 wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa akizindua Bunge hili, alieleza vipaumbele kadhaa na nipende tu kupongeza sana bajeti hii ya Serikali kwa kiasi kikubwa imeweza kutimiza vipaumbele vile au imeanza kufanya kazi vipaumbele hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, alieleza namna ambavyo atahakikisha kwamba anakuzu uchumi, alielezea namna ambavyo ataziba mianya ya mapato ya Serikali; na kwa kweli nipongeze sana Wizara ya Fedha, tumeweza kuona *e-government payment system* namna ilivyoanza, tumejionea mifumo ya kielektroniki katika Serikali za Mitaa, lakini pia tumejionea namna *TRA* pamoja na *ZRB* namna ambavyo wameboresha mifumo yao ya malipo. Ni kwa kufanya hivi ndipo tutapata bakaa ya kuweza kupata fedha na kuboresha huduma nyingine za Kiserikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia aliahidi kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya Serikali. Tumeweza kujionea namna ambavyo hata sasa safari za nje ya nchi ni zile tu ambazo ni za lazima. Hata kwa wale ambao wanaenda, ukiangalia ujumbe wao (*delegation*) kidogo kwa kiasi kikubwa imepungua na kwa kweli imekuwa ikileta tija na kutusaidia kupata fedha kwa ajili ya huduma zingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, zaidi tumeona namna utawala bora unavyoendelea kudumishwa, tumeona namna ambavyo mapambano dhidi ya rushwa yanavyoendelea, na mmeona katika wiki kadhaa kesi zinazidi kwenda mahakamani. Nipende tu kusema kwamba kuititia TAKUKURU na Serikali nzima kwa ujumla hatutafumbia macho mtu ye yeyote ambaye atataka kuchezee rasilimali, ambaye atafanya ubadhirifu wa mali za umma akifikiri tu kwamba ataweza kuchezee kwa kuwa Serikali haipo macho.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kusema kwamba TAKUKURU iko macho, itaendelea kufanya hivyo na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunafuatilia miradi yote ya

maendeleo na tunaomba tu Waheshimiwa Wabunge na wananchi watupatie ushirikiano ili kuhakikisha kwamba haya yanafanya.

Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele vingine ilikuwa ni kufanya mabadiliko makubwa ya utendaji Serikalini. Wote mtashuhudia sasa hivi mkienda katika taasisi mbalimbali za umma kwa kiasi kikubwa huduma imeboreka sana. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi muendelee kutupatia ushirikiano, itakapotokea unaenda kupata huduma unaombwa rushwa tafadhalii toa ripoti katika namba 113 ili tuweze kuchukua hatua dhidi ya yejote ambaye anataka kukupatia haki yako mpaka uwe umefanya malipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niombe sasa nielekee katika hoja chache ambazo zillijitokeza kuhusiana na ofisi yangu au masuala ya kiutumishi. Ilikuwepo hoja kwamba katika bajeti hii ya mwaka 2017/2018 nyongeza ya mshahara haijaonekana katika bajeti. Nipende tu kusema kwamba ukiangalia bajeti ya mwaka 2016/2017 ilikuwa ni ya shilingi triliioni 6.6; bajeti ya mwaka huu 2017/2018 ni shilingi triliioni 7.205, kuna nyongeza hapo ya zaidi ya shilingi bilioni 605 ambayo ni sawa na asilimia 9.18. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, fedha hizi tumepanga sasa zitatumika kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi mbalimbali, lakini pia fedha hizi zitatumika katika kulipia malimbikizo ya maslahi mbalimbali ambayo watumishi wanadai, pia tutatumia katika ajira mpya. Kama nilivyoeleza tumepanga kuajiri watumishi 52,436. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wapo ambao wamekuwa wakisema kwamba uhakiki umekuwa ukiendelea muda mrefu. Nipende tu kusema kwamba kama una Serikali makini ni lazima pia uweze kufanya uhakiki ili kujiridhisha kwamba unalipa watumishi wale tu ambao kweli ndio umewakusudia; tumeondoa zaidi ya watumishi hewa 19,708. Endapo watumishi hawa wangeendelea kuwepo katika orodha ya malipo ya Serikali au *payroll*, kila mwezi Serikali

ingepoteza takribani shilingi bilioni 20, si fedha ndogo. Sasa hivi tunatumia shilingi bilioni 18.8 kila mwezi kulipia elimu katika shule za msingi na sekondari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa wewe ujiulize kama mafanikio yote haya yanapatikana kwa fedha hizo halafu upande mwingine kulikuwa kuna zaidi ya shilingi bilioni 20 kila mwezi zilikuwa zinaondoka kwa ajili ya watumishi hewa. Kwa hiyo, nipende tu kusema kwamba watasema tunaendelea na uhakiki, tunaonekana tumekuwa maarufu kwa uhakiki, naomba bora niwe hivyo na nitaendelea kuwa Waziri wa uhakiki ikibidi ili kuhakikisha kwamba hakuna hata fedha moja ya Serikali ambayo inapotea; na kwa kufanya hivi ndipo tunapata walau ahueni ya fedha nyingine ya kuweza kuboresha maslahi ya watumishi pamoja na huduma nyingine mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wapo ambaao wanasema ajira hazijatoka, sio kweli. Tumeshaajiri ajira zaidi ya 9,000. Katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama watumishi mbalimbali wameajiriwa, wapo ambaao walisema hawajaona ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama; wameshaajiriwa wote waliotoka katika mafunzo ya depo wameshaajiriwa, labda aseme kama kuna wengine ambaao wako katika mafunzo ambaao bado hawajaajiriwa.

Mheshimiwa Spika, tumeshaajiri walimu wa sayansi na hesabu, wataalam wa maabara na tutaendelea kufanya hivyo kwa kadri uwezo wa Serikali unavyoruhusu. Niwatoe tu hofu wahitimu wetu kwamba ajira wakati wowote zitaendelea kutolewa kwa awamu kwa mujibu wa sekta husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba katika sekta ya elimu zaidi ya watumishi 16,516 tutawaajiri mwaka huu, lakini pia katika sekta ya afya zaidi ya watumishi 14,102 tutaweza pia kuwaajiri na hii pia ni pamoja na kuongeza na nyongeza nyingine ya ku-replace wale ambaao waliondoka kwa mujibu wa zoezi la uhakiki wa vyeti *fake* ambalo liiliwa likiendeshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine, nadhani ni ya Mheshimiwa Nsanzugwanko; kwamba Serikali baada ya kumaliza uhakiki wa vyeti feki ifanye *performance audit*. Nipende tu kumueleza kwamba ufanisi katika utoaji wa huduma unapimwa kwa kutumia vigezo vingi ikiwemo uwezo wa kutumia rasilimali zilizopo, usahihi na uadilifu lakini vile vile kuangalia viwango na ubora wa huduma hiyo inayotolewa kwa mujibu wa fedha inayotolewa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: ...nipende tu kumwambia mifumo ipo, tunayo mifumo ya tathmini ya uwazi kabisa ya *OPRAS*, na kuanzia mwezi Julai, tutaanza kupima utendaji wa Taasisi zote za umma, tutawaanzishia *performance contract* watendaji wote wa taasisi za umma katika kuhakikisha kwamba wanaenenda kwa mujibu wa viashiria na kuona kwamba kunakuwa na utendaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru na niseme na mimi kwa ufupi naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa kutupa habari njema, maana ikianza hii *performance contract* kwa watumishi wote yaani hapo ndipo penyewe, maana wako wengi wanalipwa mishahara yaani anachokifanya hata hakieleweki. Dakika saba sasa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi. (*Makofii*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nampongeza sana yeye, Naibu wake, Katibu Mkuu, timu ya wataalam na wote walioshiriki katika kupanga jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba Serikali imejipanga vizuri sana katika kuondoa kero hasa za uwekezaji kwa sababu tunajua uwekezaji wote unaanza kwenye msingi wa ardhi. Baadhi ya uwekezaji mkubwa ambao tunautarajia kama wa *LNG* Wabunge wamezungumza, nataka kuwahakikishia kwamba wizara yangu imeshatoa hati ya eneo lote kwa *TPDC*, hakuna tatizo la ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika eneo la uwekezaji wa bomba la mafuta kutoka Uganda, nataka kuwahakikishia kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na wabia tumeshapiga picha ya anga ya upana wa mita 200 katika eneo lote la mpaka. Kwa hiyo, najua kuna *speculators* ambao wameshaanza kupanda miti na vibanda humo, picha tunazo; hamtapata fidia watu ambao mnaweka weka katika maeneo hayo kwa sababu tumeshapiga picha za anga na kazi inaendelea katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumejianda kabisa kuondoa kero katika eneo la ardhi ili kuhakikisha wawekezaji wa ndani na nje wanawekeza wa ndani na nje wanawekeza na Watanzania wanapata unafuu katika kumiliki ardhi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha tutapanga *master plan* katika miji 30, tumeshaanza. *Master plan* ambazo zitaelekeza maeneo mbalimbali ya uwekezaji pamoja na hao wamachinga ambao wanasa jiliwa, *master plan* hizi lazima zielekeze maeneo ya kufanya biashara. Wizara yangu haitasaini *master plan* yoyote ambayo haitaelekeza maeneo ya kufanya biashara hasa za watu wadogo wadogo katika miji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, katika umilikaji wa ardhi, *EPZ* tumewapa maeneo makubwa, lakini sheria tumetunga mwaka huu *EPZ* na *TIC* tumewapa jukumu lingine la kutoa hati. Zamani ilikuwa wawekezaji wanapewa hati na Wizara ya Ardhi. Kwa hiyo, *EPZ* na *TIC* sasa wanatoa wenyewe *derivative right* ili kupunguza urasimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika umilikaji wa Watanzania na wageni, uwekezaji na ujenzi wa Mipango Miji, jambo moja liliokuwa linawakwaza Watanzania ni gharama ya umilikaji wa ardhi. Mwaka huu pekee tumeamua kama Serikali kuondoa asilimia 67 ya tozo kubwa ambayo ilikuwa inawakwaza sana watanzania na wawekezaji katika katika umilikaji wa ardhi inaitwa *premium*. Kwa hiyo, fikiria kama wewe ulikuwa unatakiwa kulipa shilingi milioni 100 sasa kuanzia tarehe moja mwezi wa saba utalipa milioni 33. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali imeamua hivi ili kuwapa nafuu watu wengi zaidi waweze kumiliki ardhi na Serikali kila mwaka iendelee kupata kodi. Kwa hiyo, tumefanya makubwa sana katika kuhakikisha kwamba tunarahisisha suala zima la uwekezaji ili kuhakikisha kwamba kila mwananchi anamiliki ardhi bila kikwazo kikubwa.

Mheshimiwa Spika, hapa Dodoma ilikuwa ni eneo pekee ambalo wawekezaji wa nje hawawezi kufika kwa sababu ya mkanganyiko wa umilikaji wa ardhi. Mheshimiwa Rais aliagiza na utekelezaji umenza, imefutwa *CDA* na sasa watu wote wanaomiliki ardhi Dodoma wataanza kupata *title deed* kama wananchi wengine katika maeneo mengine ya Tanzania, na watapata *title deed* zenye miaka 99.

Mheshimiwa Spika, wale wote waliokuwa wanapata *lease* tumeanza utaratibu wa kubadilisha ili waweze kupata *title deed* za miaka 99. Walikuwa wanapata *lease* za miaka 33 lakini sasa tutawaongeza kila mwenye hati ataongezewa miaka 66 na kwa agizo la Mheshimiwa Rais kwamba hawa watu wote wabadilishiwe hati bila kuongezwa gharama yoyote, bure. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kila mmoja sasa mwenye *lease* aliyekuwa na hati Dodoma ni fursa aende Manispaa ili aweze kupata *title deed* ya miaka 99. Maana yake ni nini? Ukipata *title deed* sasa *TIC* wanaweza kumpa *derivative right* yule mwekezaji ambaye utampata kutoka nje ambaye anaweza akaingia ubia na wewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea na jitihada za kufanya *audit*, tunajua katika kupanga mipango hii ya uwekezaji, wako matapeli wanaingia wana-*take advantage* kuchukua ardhi ya Tanzania kwa ajili ya kujipatia mitaji au kuhamisha mitaji, wanatumia ardhi yetu kufanya *mortgage* na kuhamisha pesa. Kwa hiyo, tunafanya *audit* kuwatambua wale wote ambao wamemiliki ardhi. Kwanza hawana sifa, wengine si raia, lakini wale ambao wamemiliki ardhi kubwa na bila kuziendeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita Mheshimiwa Rais amefuta mashamba yenye ekari zaidi ya elfu ishirini Mkoa wa Morogoro, na katika kipindi cha mwaka huu mmoja na nusu Mheshimiwa Rais ameshafuta mashamba yenye ekari zaidi ya 100,000 katika nchi hii, na mashamba haya yanapangwa ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wa wawekezaji walio mahiri wanamilikishwa kwa kufuata sheria. Tunajua wapo watu wamemiliki hata maeneo ya madini kwa sura za Tanzania na hati za Kitanzania.

Vilevile wapo wenzetu wengine wana hati mbili mbili za kusafiria, kwa maana wana uraia wa nchi mbili. Tunafanya uhakiki na wale wote ambao watagundulika wana hati mbili mbili lakini wamemiliki ardhi ya Tanzania tutanyang'anya kama ambavyo tumeshawanyang'anya watu wengine. Ule wakati wa longo longo umekwisha sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kila mmoja anayetaka kumiliki ardhi atapewa na nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Spika kwamba Serikali tumejipanga, tumerahisisha sana utaratibu na tumeondoa kero nyangi sana katika ardhi, umilikaji umekuwa *smooth*. Zamani ilikuwa ili uweze kupata hati unashubiri mwaka mmoja, leo *maximum* ni mwezi mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha mwaka mmoja tumejipanga twende katika lengo la wiki moja, na kutokana na mfumo tulouanza kuufunga Dar es Salaam, tumeshaanza kufanya *scanning* ya *document* mbalimbali katika Wilaya ya Kinondoni na Ubungo; kwa Dar es Salaam

tutaanza kufikia lengo hilo la wiki moja mwakani. Tukifunga mitambo hii Nchi nzima, tunaweza kufika mpaka siku mbili. Vile vile Ulipaji wa kodi mwakani tutaanza kutumia mtandao; tutalipa kodi kwa kutumia mtandao wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kwamba jitihada zinazofanywa na Mheshimiwa Rais lazima na sisi Wizara mbalimbali kama Wizara yangu ya Ardhi, tumuuunge mkono kwa kufanya yale yanayotuhusu ndani ya wizara yetu. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi.

Sasa tunaingia Wizarani, Wizara ya Fedha na Mipango na tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri uanze kuititia hoja mbalimbali na una dakika ishirini.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na kabla sijaanza kuchangia naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sote kufika hii siku ya leo na kunijalia mimi mwenyewe uzima na nafasi katika kulitumikia Taifa langu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba pia niwashukuru wazazi wangu, baba na mama yangu, mimi kama kitinda mimba wao nawashukuru

sana kwa kuendelea kuniombea, kuniamini na kunipa radhi yao ili niweze kulitumikia taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru sana rafiki yangu wa kudumu na mume wangu mpenzi Dkt. Muhajir Kachwamba ambaye yupo ndani ya Bunge hili, nikushukuru sana kwa kuendelea kuwa rafiki yangu kwa kila hali na katika kila gumu na jema ninalolipitia, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Dkt. Muhajir Kachwamba naomba usimame hapo ulipo, karibu sana na mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Abubakar usimame, karibu sana na ahsanteni sana. Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukaendelea. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naomba pia nimshukuru mtoto wangu mwingine ambaye yupo shulen i yuko kidato cha nne, Samira Muhajir; nimuombee kwa Mwenyezi Mungu aweze kufanya vizuri katika maandalizi yake na mtihani wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe pongezi; pongezi zangu ziende kwa Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kwa uthubutu, ujasiri na ujemedari wake wa kurejesha hadhi ya taifa letu ndani ya Bara letu la Afrika. Tanzania imekuwa mfano na namshukuru sana Mheshimiwa Rais, naendelea kumpongeza na niseme kama Mbunge wa Kondoa, kama alivyosema alipokuwa akiomba kura alipofika Kondoa na sasa anayatekeleza kwa vitendo yale yote aliyowaahidi wapiga kura wetu wa Jimbo la Kondoa. Nimwambie wapiga kura wetu wa Jimbo la Kondoa wapo na yeche asilimia mia moja wanamuunga mkono, aendelee kuchapa kazi kwa niaba yao na kwa niaba ya Watanzania kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru na nimpe pongezi sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Amekuwa ni kiongozi makini, mwenye dira na asiyetetereka; namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi ya kufanya kazi na Mheshimiwa Dkt. Mpango. Imedhihirika kwenye bajeti hii

ya mwaka huu imemuonesha Mpango ni nani katika tasnia ya uchumi, huyu ndiye Dkt. Mpango, katika tasnia ya uchumi wanakufahamu Dkt. Mpango, chapa kazi sisi watumishi tulio wako chini yako tuko na wewe, tutapokea maelekezo yako na tutaendelea kuyatekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia niwape pongezi watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango; naomba niwakumbushe wakati tunaanza vikao vya Kamati ya Bajeti pale mwezi wa pili niliwaambia kama ni siku basi sasa hivi ndiyo alfajiri, ndio saa kumi na moja, mpaka tutakapoelekea. Naomba niwape pongezi sana, wamefanya kazi usiku na mchana bila kupumzika wakipokea maelekezo na wakiyafanya kazi mpaka saa kumi usiku, hongereni sana chini ya Katibu wetu Mkuu Bwana Doto James. Mmeonesha kwamba Wizara ya Fedha tunaweza na tumeweza kurejesha hadhi na tunaendelea kukimbia, hongereni sana na tupo pamoja na nanyi viongozi wenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie baadhi ya hoja ambazo zimetolewa humu ndani, niweze kuzitolea ufanuzi. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuleta hoja mbalimbali ambazo ni za kuimarisha na pale penye kukosoa mmeweza kukosoa, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo ningependa kuitolea ufanuzi ipo katika kitabu cha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Mssemaji katika Wizara ya Fedha na Mipango, nayo alisemea kuhusu hali ya uchumi wa Taifa na akaendelea kusema ametoa katika taarifa ya Benki ya Dunia. Naomba ninukuu maneno machache yaliyoandikwa kwenye kitabu kile, aliandika yafuatayo:-

"Kukua kwa uchumi kumepungua kutokana na upatikanaji wa fedha kuwa hafifu na kutotabirika/ kutokueleweka kwa Rais Magufulli."

Mheshimiwa Spika, hoja yake ya pili, aliandika, baadhi ya wawekezaji wa kigeni wameamua au; naomba tuangalie sana hapa ninaposema au kwa sababu anaandika

neno halafu analitafutia neno la pili; au wanataka kupunguza shughuli zao na akasema sababu zake ni hizi zifuatazo; alisema moja, ni masharti mapya, magumu na kutozwa kodi kubwa na sababu ya pili katika hilo akatoa *reference* kutoka *PricewaterhouseCoopers Comparative World Studies of Tax Regimes of 2014*.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge na hasa ndugu zangu wa Kambi Rasmi ya Upinzani tunapojenga hoja zetu tuzijenge tukiwa na uhakika nazo. Umesema mwanzo kabisa kwamba kutotabirika au kutokueleweka kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Magufuli halafu *reference* ya 2014, hivi *reference* ya 2014 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alikuwa Rais kweli? Kwa hiyo, tuwe na uhakika na nini tunakipeleka.

Mheshimiwa Spika, unasema masharti magumu na kutozwa kodi kubwa; Mheshimiwa Spika wewe ni shahidi na Bunge lako tukufu, ni kodi zipi mpya ambazo zimeongezwa baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani? Anaongelea hizo kodi mpya na kubwa anatoa *reference* ya mwaka 2014. Hii ni ngumu sana, lazima tuwe na uhakika ni nini tunakifanya na tunalitendea haki Taifa letu kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nimwambie na niwaambie Watanzania kwa ujumla, kwanza waendelee kuamini taarifa iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu hali ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nina kitabu nimekiacha hapa, nitakukabidhi wewe ili ndugu zetu wakifanyie *reference*. Hiki ni kitabu kilichoandikwa na *World Bank* alikosema ye ye amepata *data* hizi. Katika kitabu hiki cha taarifa ilioandikwa na *World Bank* ni cha tarehe 23 Februari, 2017; chenye kichwa cha habari kinasema *United Republic of Tanzania Systematic Country Diagnostic*.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu hiki ambacho ni *very current*, cha mwezi wa pili, ndani yake wamesema nini;

wamesema, naomba ni-*quote* maneno yao kwa Kiingereza, wana sema:-

"For the past 10 years the country's macroeconomic performance has been robust, with GDP growing annually at an average of 6.5 percent-higher than the Sub-Saharan African average and that of many regional peers." (Makof)

Mheshimiwa Spika, tafsiri isiyo rasmi katika hili ni kwamba kwa miaka kumi sasa uchumi wa Taifa letu umekuwa mzuri na umekuwa ukikua kwa zaidi ya wastani wa asilimia 6.5, juu zaidi ya wastani wa ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara na wenzetu waliotuzunguka katika Ukanda wetu wa Afrika Mashariki. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hizi ndizo taarifa tunazotakiwa kuwapa wananchi wetu, kwa lengo lolote lile ambalo unalo ni vizuri kuzisema kwa umakini. (Makof)

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hiyo ya Benki ya Dunia ya mwezi wa pili inasema kumekuwa pia na kupungua kwa umaskini kunakoambatana na kupungua kwa utofauti wa kipato kati ya makundi mbalimbali ndani ya jamii. Huu ndio uchumi wa Tanzania na niwaombe Watanzania waendelee kuamini. Kitabu hiki kimetaja sababu ambazo tumekuwa tukizisema hapa kwa nini wamesema hiki wanachokiona na kwa nini taarifa zao zimeonesha hili. (Makof)

Mheshimiwa Spika, wamesema taarifa ya kwanza ni kuimari ka miundombinu ya barabara na masoko ndani ya nchi yetu. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, nani si shahidi wa kwamba Nchi yetu imeweza kuunganishwa sasa mkoa kwa mkoa nchi nzima kasoro Mkoa mmoja wa Rukwa. Tuitendee haki nchi yetu, tuwatendee haki viongozi wetu, tumtendee haki Mheshimiwa Rais wetu ambaye kabla ya kuwa Rais alikuwa Waziri wa Miundombinu na Uchukuzi, lazima tumtendee sana haki. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sababu au kiashiria cha pili kilichosababisha *conclusion* ya taarifa yao na utafiti wao, walisema ni kumiliki kwa vyombo mbalimbali vya mawasiliano na usafiri kwa Watanzania wote. Sisi sote ni mashahidi, kijiji gani utaenda ndani ya nchi hii ukose usafiri dunia ya leo? Hilo ni jambo la msingi sana, utafika popote hata kama kijiji kipo *interior* kiasi gani utapata usafiri na utafika, naomba ndugu zetu waweze kututendea haki.

Mheshimiwa Spika, naamini sisi sote humu kama Waheshimiwa Wabunge tunawahudumia wapigakura wetu kwa *e-payments*; hivi kweli sisi ndio wa kusema kwamba uchumi wa nchi yetu hauki? Nani ambaye hatumi *M-Pesa*, Tigo-Pesa, Airtel-Money kwa wapigakura wake kijiji chochote ndani ya Tanzania? Lazima tujitendee haki na tuwatendee haki Watanzania. Hivi ni baadhi tu ya viasharia viliviyowekwa na taarifa hii, vipo vingi, kama nilivyo sema nitakabidhi taarifa hii kwako ili ambaye anataka kufanya *reference aje afanye reference* ili tuwe na uelewa wa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie na nukuu chache kuhusu hali ya uchumi wa Taifa letu kutoka kwa wageni mbalimbali waliolitembelea Taifa letu miezi michache iliyopita. Mmoja wao alikuwa Naibu Mkurugenzi wa Benki ya Dunia, Bwana Tao Zhang; akiwa Tanzania, wala hakuwa Washington, alikuwa Tanzania; alisema hivi, nanukuu maneno yake:-

"Uchumi wa Tanzania umebaki kuwa imara kutokana na maboresho ya kisera yanayotekelezwa chini ya uongozi thabiti wa Rais John Pombe Joseph Magufuli." (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, akasema hasa katika suala la ukusanyaji wa mapato na vita dhidi ya rushwa na ugaidi. Hao ndio wachumi wa dunia na wanafanya *analysis* kwa kutumia *data* ambazo ni *credible*, naomba tuendelee kuwaamini.

Mheshimiwa Spika, sishangazwi sana na maneno haya yaliyopo kwenye Hotuba hii ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Naomba ninukuu pia maneno ya mwekezaji mmoja kutoka

China ambaye alikuwa anatafuta taarifa za kwenda kuwekeza katika viwanda vya ngozi na viatu nchini Ethiopia. Mwekezaji huyu kabla hajaenda alikuwa akitafuta taarifa, na haya maneno yake alisema, akasema:-

"Ukiwa nje ya Afrika unapewa picha na baadhi ya watu wakiwemo Waafrika wenyewe kwamba Afrika ni sehemu ya vita, Afrika ni sehemu iliyojaa njaa, Afrika ni sehemu ya magonjwa na kusahau kuwa Afrika ina mchango mkubwa na fursa nyingi katika mchango wa dunia." (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nanukuu maneno haya ili tu Watanzania watuelewe, kwamba tunachokifanya chini ya uongozi wa jemedari, Dkt. John Pombe Magufuli ni kuimarisha uchumi wa kila Mtanzania (*inclusive growth for everyone in Tanzania*) hiki ndicho tunachokifanya. Niwaombe Watanzania wapuuze taarifa zillizowasilishwa, niwaombe sana ndugu zangu, Mheshimiwa Bunge lako hili ni Tukufu, litendewe haki kwa kuletewa taarifa ambazo ni haki, taarifa ambazo ni halali, taarifa zenye vyenzo vyenye uhakika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hili, naomba sasa niendelee na baadhi ya hoja nyine. Hoja ya pili ambayo ninapenda kuielezea ilisemwa na niliitolea maeleo, yawezekana sikuelewa vizuri; ilikuwa ni kuhusu Serikali kutoa maeleo kuhusu utekelezaji wa ahadi ya shilingi milioni hamsini.

Mheshimiwa Spika, wewe umeshuhudia Waheshimiwa Wabunge wakiongea kwa uchungu, wengine kwa kejeli ambazo sio nzuri na hili pia limeandikwa kwa kejeli kubwa sana katika Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Naomba nikumbushe, wakati tuna-conclude Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango nilisema fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zilitengwa shilingi bilioni 59.5, na mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 60 chini ya Fungu 21 - Wizara ya Fedha na Mipango. Fedha zimetengwa na hazina wasiwasi kwamba hazipo, zipo fedha hizi. Nikasema kwamba

tunachokifanya sasa ni kuhakikisha tunasoma mfumo mzima, tunajifunza kutokana na makosa yaliyotendeka huko nyuma ili tuhakikishe fedha hizi za walipa kodi wa Tanzania zinakuwa na matokeo chanya katika Taifa letu na zinaweza kutekeleza kile ambacho kimesababisha Mheshimiwa Rais aweze kuahidi ahadi hii ya shilingi milioni hamsini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yapo maswali ambayo tunajaribu kujiuliza kama wataalam wa uchumi, kwamba hivi *governance* ya hii shilingi milioni hamsini ikoje katika kila kijiji? Hivi tunaposema tunapeleka, tunapeleka shilingi milioni hamsini hizi katika mfumo upi? Tunajiuliza ni njia gani bora tunaweza kumpatia pesa Mtanzania huyu aliyeo kijijini kwangu kule Kalamba. Tunajiuliza, je, baada ya kutambua kijiji kinahitaji kiasi hiki tunawezaje sasa kujua nani anapata nini na kwa kiasi gani na anakwenda kutekeleza mradi gani? Tunaweza kujiuliza na kujibu maswali, je, ni mfumo gani tunataka kuutumia sasa ili kurejesha fedha hizi? Tukumbuke nilisema hapa kwamba fedha hizi si zawadi, fedha hizi ni mkopo. Fedha hizi zinatakiwa zipelekwe zikaimarishe uchumi na hatimaye tuhakikishe zinazunguka kwa Watanzania wote na kila Mtanzania anafaidika na pesa hii na mwisho wa siku pesa hizi zinarudi ndani ya Serikali yetu tukiwa tumeimarisha uchumi wa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba mpaka tulipofika tupo hatua nzuri sana, na pesa kama nilivyosema shilingi bilioni 59.5 zipo, shilingi bilioni 60 tumetenga kwenye bajeti yetu ya mwaka huu, zote tutazipeleka kama ambavyo tuliahidi. Sasa hivi tumefika hatua nzuri, tayari Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa kuhusu utaratibu na maeneo pamoja na mfumo utakaotumika katika kutekeleza programu hii ya uwezeshaji wananchi wetu kiuchumi. Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na tumeona kwa pamoja, hakuna ahadi anayoahidi akashindwa kuitekeleza, anatekeleza ahadi zake zote na hili atalitekeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye hoja nyingine ambayo imesemwa sana kwamba Serikali inaona

kuwa na utaratibu wa kukopa zaidi katika soko la ndani, hali hii kiuchumi si nzuri kwa kuwa taasisi za fedha zinakimbilia kuikopesha Serikali zaidi kuliko sekta binafsi. Katika hili tunafahamu zipo *instruments* mbalimbali zinatumika kuhakikisha Serikali inakopa na inakopa kwa vigezo, inakopa ikiwa na ukomo kwamba inakopa kiasi gani ili isiathiri utendaji wa sekta binafsi ndani ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama Wizara ya Fedha na Mipango tunafahamu sekta binafsi ndiyo *engine* ya uchumi, hatuwezi Serikali kufanya kitu chochote kinyume na sekta binafsi. Tunachukua tahadhari ya kutosha katika kulifanya hili na Serikali, kama nilivyosema, imeweka ukomo wa kukopa ndani usiozidi asilimia 1.5 ya Pato la Taifa kwa mwaka ili kuzipa nafasi benki za biasara kuendelea kukopa mikopo kwenye sekta binafsi ambayo ndiyo *engine* ya uchumi wetu kama nillivyosema. Kwa mwaka huu tumeona kwamba tupunguze kiwango cha kukopa kutoka ndani na mwaka huu tunakopa asilimia moja tu ya Pato la Taifa ili kuipa nafasi sekta binafsi kuchukua mikopo ndani ya benki zetu. (*Makof*)

Jambo lingine ambalo limesemewa sana; nililijibu lakini naona nalo halikukaa vizuri au Waheshimiwa Wabunge hawakunielewa ilikuwa ni mikopo kutoka mifuko ya hifadhi ya jamii, kwamba Serikali imekuwa na tabia ya kukopa fedha kutoka Mifuko ya Jamii bila kuzirudisha kwa wakati, nini mpango wa Serikali wa kulipa madeni hayo?

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kama nilivyosema kwenye jibu la hoja iliyopita, kukopa ndani ya nchi na hasa kwa mifuko yetu tunaipa nafasi pia mifuko yetu kupata fedha ambazo ni za uhakika. Hata hivyo, katika kulipa madeni haya naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba katika uchumi malipo ni jambo la muhimu lakini kuhakikisha unalipa nini ni jambo la muhimu zaidi, na hicho ndicho ambacho kimechelewesha malipo haya kwa Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii. Tumefanya uhakiki; na ninaomba nitoe taarifa chache tu ya kuona ni kwa nini Serikali iliona ni muhimu kufanya uhakiki wa madeni haya, tuchukue mfano mmoja... (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, malizia sasa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, muda umekuwa ni mchache sana lakini naomba niseme kwamba hoja hizi tutaziwasilisha kwa maandishi, na ninaomba niseme kwamba nia na lengo la Serikali yetu ni jema sana la kuhakikisha tunalipa mikopo yote, si ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii tu bali ya wakandarasi, wazabuni pamoja na watumishi. Tunafanya hivyo kuhakikisha Watanzania wanaweza kuimarisha uchumi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaomba niseme naunga mkono hoja hii ya Serikali iliyowekwa Mezani na Waziri wa Fedha na Mipango ambayo imetuhakikishia Serikali yetu ina nia ya dhati ya kuhakikisha uchumi wa viwanda na uchumi wa kati unafika Tanzania kabla ya mwaka 2025. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, nikuhakikishie Dkt. Muhajir mke unaye. (*Makof/ Kicheko*)

Sasa nimuite mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango ili aweze kujibu na kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha una dakika 60 ambayo ni sawa na saa moja. (*Makof*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuhitimisha mjadala wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2017/2018. Utakumbuka tarehe 08, Juni, 2017 niliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018

na Mapendeleko ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba zote mbili nilieleza shughuli mbalimbali zilizotekeliza na Serikali katika kipindi cha mwaka 2016/2017 pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza. Aidha, nilieleza malengo na miradi ya kipaumbele ambayo Serikali inakusudia kutekeleza katika mwaka 2017/2018 na mapendeleko ya bajeti. Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi ya kuzipitia hotuba hizo pamoja na viambatisho vyake na kutoa maoni na mapendeleko juu ya namna bora zaidi ya kufanikisha ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri mjadala huu ambaou unatarajiwa kuhitimishwa hivi leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua michango iliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini pamoja na maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yaliyowasilishwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba kwa niaba ya Msemaji wa Kambi hiyo kwa Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, ninathamini sana maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wote. Wabunge 193 walichangia mjadala wa Bajeti Kuu ya Serikali, kati ya hao wa kuzungumza walikuwa ni 165 na 28 kwa maandishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi na Wizara yangu tunawashukuru kwa dhati kabisa kwa pongezi ambazo mlitupatia, nikianza na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alinipigia simu kutoa pongezi zake, lakini pia ninyi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wengi ambaou wametupongeza kutoka ndani na nje ya nchi yetu, kwa kweli mmetupatia nguvu ya kufanya vizuri zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala wa hotuba nilizoziwasilisha, Serikali imepokea michango mingi sana na ushauri. Yapo maeneo yaliyoungwa mkono na mengine ambayo yalilenga kuboresha Bajeti ya Serikali au kuikosoa. Napenda kulihakikishia Bunge kwamba tumepokea michango yote yenyе afya kwa maendeleo ya Taifa letu. Baadhi tutayazingatia katika bajeti hii na bajeti zitakazofuata; na leo nitadhihirisha tena kwamba bajeti hii haijawahi kutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua ambazo ziliungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wengi ni pamoja na zifuatazo:-

Kwanza, ni kufuta ada ya mwaka ya leseni ya magari, kutoa msamaha wa kodi, riba na adhabu zinazoambatana na madeni yote ya ada ya leseni ya magari yaliyolimbikizwa kwa miaka ya nyuma, kuanzisha maeneo maalum (*clearing houses*) ya kukagua na kuthibitisha thamani ya madini kabla ya kusafirishwa, kuondoa VAT kwenye bidhaa za mtaji, kusamehe VATkwenye vyakula vya mifugo, kutoa msamaha wa VAT na ushuru wa forodha kwenye vifaa maalum vya kutengeneza vifaa vya watu wenye ulemavu; pia miradi ya kielelezo itakayopewa msukumo maalum katika mwaka wa 2017/2018 ikiwemo miradi ya maji, zahanati, vituo vya afya, uendelezaji wa elimu katika ngazi zote, ununuzi wa vifaa tiba, ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, uimarishaji wa Shirika la Ndege la Tanzania, miradi ya umeme, miradi ya makaa ya mawe na chuma, uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji, ujenzi wa barabara za kuunganisha mikoa na ule wa bomba la mafuta kutoka Hoima - Uganda hadi Bandari ya Tanga, lakini pia kuendeleza utulivu wa uchumi wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nami niungane pia na Waheshimiwa Wabunge wengi waliopongeza juhudhi zilizochukuliwa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kulinda rasilimali za Taifa letu ili kuhakikisha kwamba Watanzania tunanufaika na rasilimali za nchi na hususan madini.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Jemadari wetu Mkuu kwa kuthubutu kufichua na kuweka hadharani udhalimu ambao tumekuwa tunafanyiwa kwa miaka mingi kuititia utoroshaji wa madini na upotevu wa mapato ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunamhakikishia Mheshimiwa Rais wetu kuwa tunamuunga mkono na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu amlinde, ampe afya njema na amtie nguvu katika kazi yake ngumu ya kuongoza mapambano dhidi ya uporaji wa rasilimali za nchi yetu. Ushindi ni lazima na hakuna kurudi nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kidogo juu ya ushauri uliotolewa na Wabunge wengi. Kama nilivyo sema mwanzo, yapo maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi katika maeneo mbalimbali ili Serikali iangalle namna ya kuyazingatia katika bajeti hii na zijazo. Naomba kurejea ushauri muhimu sana uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongeza kasi ya kutekeleza miradi ya maji nchini na hasa vijijini kwa kuongeza bajeti ya maji;
- (ii) Kuboresha mfumo wa utozaji kodi ya majengo;
- (iii) Kukamilisha haraka utaratibu mzuri na endelevu na kuanza kutoa shilingi milioni 50 kwa kila kijiji haraka iwezekanavyo;
- (iv) Kuongeza kasi ya kulipa madeni ya ndani ya wakandarasi, watoa huduma na watumishi;
- (v) Kudhibiti kasi ya ukuaji wa Deni la Taifa;
- (vi) Kuendeleza utulivu wa uchumi ikiwa ni pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei;
- (vii) Kuimarisha thamani ya shilingi na kuongeza wigo wa huduma za kibenki hadi vijijini; na

(viii) Kujenga mazingira rafiki kwa uwekezaji na kufanya biashara nchini kwa kudumisha mashauriano na ushirikiano wa dhati na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kufafanua baadhi ya hoja.

Hoja ya kwanza, Serikali ilishauriwa iongeze tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli kwa ajili ya Mfuko wa Maji ili kuwe na chanzo kinachotabirika (*ring fence*).

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni hoja mama ambayo ilitawala mjadala wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Baada ya Serikali kutafakari kuleta pendekezo la kufuta ada ya *Motor Vehicle License* ili kuondo kero ya muda mrefu ya kutoza ada hiyo hata kama magari hayatembe na kufidia mapato hayo kwa kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya dizeli, petrol na mafuta ya taa kwa shilingi 40 kwa lita; Waheshimiwa Wabunge walishauri mapato yatakayotokana na hatua hiyo, ndiyo yaelekezwe kwenye Mfuko wa Maji kwa kutambua kwamba kuongeza zaidi ushuru wa bidhaa kwenye mafuta, kutaathiri wananchi wengi kwa kuwa kutasababisha bei za bidhaa karibu zote, chakula, usafiri, usafirishaji, gharama za uzalishaji na gharama za maisha kwa ujumla kupanda sana kutokana na kupandisha bei ya nishati hiyo muhimu tena katika kipindi ambacho bei za mafuta katika Soko la Dunia inatarajiwa kuongezeka kwa wastani wa dola 50 kwa pipa hadi dola 60 mpaka 65 katika mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuelekeza chanzo cha mapato mahususi kwenye matumizi maalum (*revenue earmarking*) unasaidia kuongeza fedha kwenye eneo linalolengwa na pia kuhakikisha upatikanaji wa fedha (*funding stability*). Ni kweli pia utaratibu huu umeleta matokeo chanya kwenye programu ya kusambaza umeme vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini. (*Makof*)

Aidha, ahadi iliyopo katika katika ilani ya uchaguzi ya CCM 2015 hadi 2020, ni deni na Serikali ina nia thabiti ya kumtua mama ndoo kichwani katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali katika kipindi kifupi cha miezi 18 zinathibitishwa na kukamilika kwa miradi mikubwa ya maji ikiwemo Ruvu Chini ambayo inatoa lita milioni 270 kwa siku; Ruvu Juu lita milioni 196 kwa siku; Visima vya Mpera na Kimbiji lita milioni 260 kwa siku na Sumbawanga lita milioni 13 kwa siku. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya maji iliyokamilika ni Nansio, Ukerewe lita milioni 8.6 kwa siku, Bukoba Mjini lita milioni 18 kwa siku, Musoma Mjini lita milioni 30 kwa siku, Sengerema lita milioni 15 kwa siku, lakini pia mradi ule wa Msanga Mkuu kule Mtwara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, Serikali inapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge hili kwa ajili ya miradi ya maji kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambazo ni shilingi bilioni 249.5 na Mfuko wa Maji shilingi bilioni 158.5 zitatolewa kuendana na mpango kazi na kupitia Kamati ya Bajeti, Bunge litapewa taarifa rasmi ya utekelezaji wa hadi hii ya Serikali kila nusu mwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua nyingine zitakazochukuliwa na Serikali ni pamoja na zifuatazo:-

Kwanza, ni kuharakisha mchakato wa mikopo kwa ajili ya miradi ya maji kutoka taasisi mbalimbali na nchi rafiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba leo terehe 20 Juni, 2017 nimesaini mkopo wa

dola za Kimarekani milioni 400 kutoka Benki ya *Credit Swiss* ili kugharamia miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna miradi mikubwa sita:-

Kwanza kuna mradi wa upanuzi wa huduma za maji Mijini ambao utagusa Mikoa ya Kagera, Rukwa, Dodoma, Morogoro, Pwani, Simiyu, Iringa, Mara na Mwanza. (*Makofii*)

Mradi wa pili ni mradi wa uchimbaji wa visima na ujenzi wa Mabwawa katika Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Shinyanga na Simiyu. (*Makofii*)

Mradi wa tatu ni mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji Mijini, itagusa Mikoa ya Rukwa, Dodoma, Morogoro, Kigoma, Kagera, Lindi, Manyara, Mtwara, Tabora, Ruvuma na Kilimanjaro. (*Makofii*)

Mradi wa nne, ni mradi wa upanuzi wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira Dar es Salaam na hii itagusa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. (*Makofii*)

Mradi wa tano ni kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji. Itagusa Mikoa ya Pwani, Rukwa, Ruvuma, Tanga, Kigoma, Dodoma, Manyara, Njombe, Singida, Shinyanga, Tabora, Songwe, Mwanza, Kagera, Geita, Mara na Morogoro (*Makofii*)

Mradi wa sita ni mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga na mikoa itakayohusika ni Shinyanga na Simiyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha taratibu za mkopo kutoka *Exim Bank of India* dola milioni 500 ambazo ni takriban shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya miradi ya maji katika miji 17 nchini. Hivi sasa mkopo huo umeshakufanyiwa uchambuzi na Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Madeni na Waziri wa Fedha na Mipango amesharidhia kwa niaba ya Serikali, fedha hizi zikopwe. Taratibu zinazobaki sasa ni

kukamilisha usanifu wa miradi hii na kupata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hatimaye kusaini mkataba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inafuatilia upatikanaji wa fedha *Euro* milioni 102 kutoka *Green Climate Change Fund* kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji ya Simiyu. Pia nchi rafiki ikiwemo Morocco na Misri zimeonyesha utayari wa kugharamia utekelezaji wa miradi ya maji hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyine ilikuwa ni kwamba Serikali inatoza Kodi ya Leseni ya Magari kwa mwaka (*Annual Motor Vehicle License Fee*) kwa Watanzania maskini ambao hawamiliki gari kwa kutoza kodi hiyo katika mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ikiwemo mafuta ya taa unalenga kuwalinda Watanzania dhidi ya madhara ya uchakachuaji wa mafuta (*fuel adulteration*).

Kwa sasa tofauti ya kodi zinazotozwa kwenye mafuta ya taa na Dizeli ni shilingi 53 kwa lita. Endapo ushuru huu wa shilingi 40 hautaongezwa kwenye mafuta ya taa, tofauti ya kodi itakuwa shilingi 93 kwa lita ambayo itachochaea uchakachuaji wa mafuta utakaosababisha uharibifu wa magari na mitambo na kupoteza mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ongezeko la tozo kwenye petroli, dizeli na mafuta ya taa limefikiwa ili kuondoa kero ya muda mrefu ya wamiliki wa magari kudaiwa ada ya *Motor Vehicle License* hata kama gari halitembe, lakini pia tumefanya hivyo kwa namna ambayo haitachochaea uchakachuaji wa mafuta. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo pia itaiwezesha Serikali kupata mapato ambayo yatatumika kugharamia huduma muhimu za jamii kama barabara, afya, dawa na vifaa tiba

ambavyo Watanzania masikini pia watafaidika nazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, palikuwepo na hoja kwamba msamaha (*Tax Amnesty*) ambayo nilitangaza ile tarehe 8 Juni, 2017 ambayo ulitolewa kwenye Ada ya Mwaka ya Leseni uhusishe na ada ya ukaguzi wa vifaa vya kuzima moto (*Fire Inspection Fee*).

Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hatua ya Serikali ya kutoa msamaha (*Tax Amnesty*) kwa ada ya leseni ya magari itahusisha pia ada, riba na adhabu ya madeni yote ye *fire inspection fee* yaliyolimbikizwa miaka ya nyuma. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Rudia.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nitarudia tena.

Mheshimiwa Spika, hatua ya Serikali ya kutoa msamaha (*Tax Amnesty*) kwa ada ya leseni ya magari itahusisha pia ada, riba na adhabu ya madeni yote ye *fire inspection fee* yaliyolimbikizwa miaka ya nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba tozo ya shilingi 10,000 kwenye nyumba ambazo hazijathaminiwa hususan za vijiji ni kuwaongezaa mzigoo wananchi wa kijiji, lakini pia ile tozo ya shilingi 50,000 kwa ghorofa ambazo wanaishi wastaafu iondolewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kodi ya majengo hutozwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Miji (*The Urban Authorities Rating*) Sura ya 289. Kifungu cha pili cha Sheria ya Mamlaka ya Miji (*The Urban Authorities Act*) inabainisha kuwa kodi ya majengo inatozwa kwenye majengo yaliyojengwa kwenye Mamlaka za Majiji, Miji na Miji Midogo. Vijiji havitahusika katika kodi hii. (*Makofii*)

Aidha...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge wanasemasema, hamsikilizi vizuri. Naomba Mheshimiwa Waziri arudie hili. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kodi ya majengo hutozwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Miji (*The Urban Authorities Rating*) Sura ya 289 na kifungu cha pili cha Sheria ya Mamlaka ya Miji (*The Urban Authorities Act*) inabainisha kuwa kodi ya majengo inatozwa kwenye majengo yaliyojengwa kwenye Mamlaka za Majiji, Miji na Miji Midogo. Vijiji havihuksiki katika kodi hii. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, aidha,...

SPIKA: Waheshimiwa hata hilo hamshangilii pia! (*Kicheko/Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Tunashauri mhamie vijijini! (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa sheria, wananchi wenyewe umri zaidi ya miaka 60 hawapaswi kulipa kodi ya majengo wanayoyatumia kama makazi yao wenyewe. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Rudia.

MBUNGE FULANI: Hatujasikia vizuri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ninasema, aidha kwa mujibu wa sheria, wananchi wenyewe umri zaidi ya miaka 60 hawapaswi kulipa kodi ya majengo wanayoyatumia kama makazi yao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, palikuwa na hoja kwamba Serikali isitoze kodi ya majengo kwenye nyumba za tope na tembe.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha (3); "Kodi ya majengo hutozwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Miji, Sura ya 289 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha ya mwaka

2015." Kwa mujibu wa kifungu cha pili cha Sheria za Mamlaka za Miji (*The Urban Authorities Act*) kinabainisha kuwa kodi ya majengo inayotozwa kwenye majengo yaliyojengwa kwenye Mamlaka za Majiji, Manispaa, Miji Midogo na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha tatu cha Sheria hii kimetafsiri nyumba zinazotakiwa kutozwa kodi ya majengo kuwa ni nyumba zote zilizoko ndani ya Mamlaka ya Majiji, Manispaa, Miji Midogo na Halmashauri za Wilaya ambazo zimeshajengwa na kuanza kutumika kwa makazi. Kwa maelezo hayo, kodi ya majengo inatozwa kwa nyumba zote zilizoko kwenye Mamlaka ya Majiji, Miji na Miji Midogo ambazo zimeshaanza kutumika kwa makazi kama ilivyobainishwa kwenye hotuba yangu ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018. Hata hivyo, tozo hizo hazitahusisha nyumba za tope na tembe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nilieleze Bunge lako na wananchi kwa ujumla kuwa kodi ya majengo kama nilivyosema itatozwa katika Miji, Majiji na Miji Midogo kwa mujibu wa Sheria za Kodi ya Majengo ya Mamlaka ya Miji Sura ya 289. Kodi hiyo itatozwa katika majengo ya kudumu yaani yale yaliyojengwa kwa tofali za saruji, tofali za kuchoma na kuezekwa kwa bati na siyo za udongo wala zilizoezekwa kwa nyasi au zile za tembe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwasilishaji wa mapato ya kodi ya majengo kwa Halmashauri. Mapato ya kodi ya majengo na mabango yatakayokusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuhifadhiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, Serikali itaweka utaratibu wa kurejesha mapato hayo kwenye Halmashauri ambapo watatakiwa kuwasilisha mahitaji yao halisi. Aidha, Serikali itapitia mahitaji yao ili kujiridhisha kabla ya kuwarejeshea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kutokutoza kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) kwenye magari ya kubeba wagonjwa. Kwa kutambua umuhimu wa huduma za afya kwa wananchi wetu na hasa katika maeneo ya vijijini,

Serikali imeamua kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye magari yanayotumika katika kubeba wagonjwa (*ambulance*). (*Makofii/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: Rudia, rudia hiyo!

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa magari yanayotumika katika kubeba wagonjwa (*ambulance*). Hatua hii itahusisha magari yanayoingizwa nchini yakiwa yametengenezwa mahsusii kwa ajili ya kubeba wagonjwa na kwamba yanaingizwa nchini kwa matumizi ya hospitali au vituo vya kutoa huduma za afya vilivyosajiliwa kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itatumia utaratibu wa Hati ya Malipo ya Hazina (*Treasury Voucher System*) katika kusimamia misamaha hii ambapo kodi inayosamehewa italipiwa na Serikali kupitia Hazina kama inavyofanyika kwa taasisi za dini na kadhalika ili kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye ada na vibali vya uwindaji vitolewavyo na Serikali. Serikali inaondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye ada, leseni na vibali vya uwindaji. Hatua hii ina lengo la kuhamasisha ukuaji wa shughuli za uwindaji na sekta ya utalii kwa ujumla. (*Makofii*)

Kulikuwa na hoja kuhusu ada ya tathmini ya mazingira. kutokana na kilio cha wawekezaji wengi na hasa katika Sekta ya Viwanda, napendekeza kufuta Ada ya Kufanya Tathmini ya Mazingira (*Environmental Impact Assessment*) kwa wawekezaji wote wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, narudia.

MBUNGE FULANI: Rudia!

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Napendekeza kufuta Ada ya Kufanya Tathmini ya Mazingira (*Environmental Impact Assessment*) kwa wawekezaji wote wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali ifanye marekebisho kwenye Sheria ya *EPOCA*, Serikali imelisikia hili na baada ya kutafakari kwa kina, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya *EPOCA* ili:-

Moja, hisa za asilimia 25 zitakazouzwa na kampuni ya mawasiliano kwenye Soko la Hisa ziuzwe kwa umma ili kujumuisha Watanzania au Kampuni yoyote ya Kitanzania; Watanzania wanaoishi nje ya nchi, kampuni zinazomilikiwa kwa pamoja baina ya Watanzania na raia wa nje; raia na kampuni au taasisi za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; au raia wa kampuni kutoka nchi nyingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa sharti liliopo kwa mujibu wa sheria ni kwa hisa husika kuuzwa kwa raia wa Tanzania pekee.

Mheshimiwa Spika, ya pili ni kuziondoa kampuni ndogo za mawasiliano ambazo zina leseni ya *application service* kwenye sharti la kuza hisa kwenye Soko la Hisa ili kubaki na kampuni kubwa za mawasiliano zenye leseni ya *network facility* au *network service*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, Kampuni ya simu itakayoshindwa kufikia mauzo ya asilimia 25 kutokana na kutofaulu kwa toleo kwa umma (*Unsuccessful Public Offer*), Waziri mwenye dhamana atatoa maelekezo yaani *directives* ya namna kampuni husika itakavyoweza kutoa hisa kufikia asilimia 25 kwa kadri hali ya soko itakavyoruhusu, baada ya kupokea maombi ya kampuni ya simu iliyotolewa chini ya Sheria ya *EPOCA* na baada ya kupokea mapendekezo ya Mamlaka ya Masoko na Mitaji na Dhamana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoa huduma na wauza bidhaa katika maeneo yasiyo rasmi kusajiliwa; ili kuhamasisha

wafanyabiashara ndogo ndogo, kurasimisha shughuli zao na Serikali iweze kukusanya kodi, utaratibu nilioutangaza kupitia Bajeti Kuu ya Serikali kuhusu kuwatambua wafanyabiashara wa aina hii na kuwapa vitambulisho, itahusisha pia watoa huduma za chakula (*caterers*), washereheshaji (*masters of ceremony*) katika shughuli mbalimbali na wafanyabiasha wadogo wasio rasmi wanaofanya biashara katika maeneo rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie. Ili kuhamasisha wafanyabiashara wadogo kurasimisha shughuli zao na Serikali iweze kukusanya kodi, utaratibu nilioutangaza kupitia Bajeti Kuu ya Serikali kuwatambua wafanyabiashara wa aina hii na kuwapa vitambulisho; itahusisha pia watoa huduma za chakula (*caterers*), washereheshaji (*masters of ceremony*) katika shughuli mbalimbali na wafanyabiasha wadogo wasio rasmi wanaofanya biashara katika maeneo rasmi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu utozaji wa tozo kwa kutumia fedha za kigeni kwenye vyombo vya uvuvi vilivyojiliwa nchini; Serikali imesikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na kero wanayopata wavuvi nchini ya kutozwa tozo mbalimbali kwa fedha za kigeni kwenye vyombo vya uvuvi vilivyojiliwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuanzia sasa Serikali inaagiza taasisi zote zinazohusika na utozaji wa tozo hizo ziache utaratibu huo mara moja na zianze kutoza kwa kutumia shilingi ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja nytingine ilikuwa kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kukusanya kodi inayotokana na mapato kutoka kwenye sekta ya michezo ya kubahatisha.

Kwa kuzingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, Serikali imeona kuna uwezekano wa kupata mapato mengi kutoka kwenye sekta ya michezo ya kubahatisha. Hivyo, kuanzia tarehe 1 Julai, 2017 mapato yote yatakayotokana na michezo ya kubahatisha yatakusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*).

Mheshimiwa Spika, mapato hayo yatawasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali, Serikali itaweka utaratibu wa kuzirejesha fedha hizo kwenye Bodi ya Michezo ya kubahatisha baada ya kuhakiki mahitaji na matumizi ya Bodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba uchumi wa taifa siyo shirkishi, na bajeti iko kinyume na mahitaji ya ukuwaji shirkishi wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe darasa kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dhana ya uchumi shirkishi ni pana sana. Kwa lugha nyepesi ukuaji wa uchumi unakuwa shirkishi kama jamii inashiriki na kunufaika katika shughuli kuu zinazokuza uchumi wa nchi. Ndilo kusema lazima uchumi kwa upana wake uwe unakua na kunemeesha wananchi walio wengi kwa namna ambayo ni endelevu (*broad based growth that generate sustain progress in living standards*).

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi shirkishi unapimwa kwa viashiria vingi, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa fursa za ajira (*job creation*), kupungua kwa umasikini, kuongezeka kwa tabaka la kati katika nchi (*growth of the middle class*), kupungua kwa tofauti za kipato (*declined in income inequality*), kupanuka kwa wilgo wa fursa na huduma za kiuchumi na hususan masoko na huduma za kifedha (*financial services*) na usalama (*security*).

Mheshimiwa Spika, aidha, ukuaji wa uchumi shirkishi, unajengwa juu ya nguzo (*pillars*) takriban saba ambazo ni:-

- (1) Elimu na ujuzi; (*Makofi*)
- (2) Huduma za kijamii na miundombinu; (*Makofi*)
- (3) Mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi; (*Makofi*)
- (4) Huduma za kifedha na uwekezaji;

- (5) Ujasiliamali na ukuzaji wa rasilimalia (*accumulation of assets*);
- (6) Ajira na mafao ya wafanyakazi; na
- (7) Uhawalishaji wa rasilimali fedha (*fiscal transfers*).

Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wanaopenda kupata elimu ya kina juu ya somo hili, kuna vitabu na machapisho mengi na wanaweza kujsomea ikiwa pamoja na taarifa ya hivi karibuni ya *World Economic Forum* ambayo inaitwa *The Inclusive Growth and Development Report, 2017*. Hivyo, siyo sahihi hata kidogo kuangalia kigezo kimoja tu na kutoa hukumu kwamba ukuaji wa uchumi siyo shirikishi au kwamba bajeti iko kinyume na mahitaji ya ukuaji shirikishi wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa 2016 ambacho kiligawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, tarehe 8 Juni, kinaonesha wazi kuwa Tanzania imepiga hatua nzuri katika viashiria vingi na ujenzi wa misingi ya uchumi shirikishi chini ya dhana ya kujenga uchumi wa viwanda. Bajeti ya mwaka 2017/2018 imejielekeza katika maeneo yote ya msingi kwa ujenzi wa uchumi shirikishi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa kila kitu siyo waridi na haiwezekani kuwa na ukuaji wa uchumi shirikishi katika kipindi kifupi, maana maendeleo ni mchakato.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo bado yanahitaji msukumo zaidi ikiwa ni pamoja na sekta ya kilimo ambayo katika nchi yetu inaa jiri takribani theluthi mbili ya Watanzania lakini imekuwa ikikua kwa kasi ndogo na ndiyo maana Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza tija kwenye kilimo kwa kutilia mkazo kilimo cha umwagiliaji kuhakikisha upatikanaji wa mikopo, pembejeo na masoko ya uhakika, kuhamasisha kilimo cha kibishara na kujenga myororo wa thamani.

Mheshimiwa Spika, aidha, Tanzania ni mfano bora duniani kwa upande wa huduma za kifedha jumuishi (*financial inclusion*), ambapo zaidi ya watu milioni 17 wanafanya miamala ya malipo kupitia simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kodi na tozo nyingi, tozo 16 ambazo zinatoza wamiliki wa shule binafsi. Serikali imesikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuondoa baadhi ya kodi na tozo kwenye shule binafsi. Serikali imezingatia maoni hayo na imeamua kuondoa tozo zifuatazo:-

Kwanza, ni tozo ya kuendeleza Mafunzo ya Ufundı (*SDL*); na pili, ni ada ya Zimamoto. Lengo la hatua hizi ni kupunguza gharama kwa wazazi na walezi katika kuwapatia watoto wetu elimu na kuziwezesha shule kutoa elimu kwa gharama nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Serikali kuwa wamiliki wa shule wataipokea dhamira hii njema ya Serikali; na hivyo kupitia viwango na ada wanazozitoza ili kuzipunguza na hivyo kutoa fursa zaidi kwa watoto na vijana kutoka katika familia maskini ili ziweze kumudu ada za shule hizo binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya utegemezi wa kibajeti, kwamba pamoja na ukweli kuwa washirika wa maendeleo kutoka nje wanaendelea kupunguza kasi yao ya kutoa mikopo na misaada, bado bajeti ya Serikali imeendelea kuongeza kiasi cha utegemezi wa mikopo na misaada.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza kasi ya makusanyo ya mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi kutoka kwa washirika wa maendeleo. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2011/2012 kiwango cha utegemezi kimeendelea kupungua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 fedha za nje zilikuwa shilingi trilioni 3.9 sawa na asilimia 29 ya bajeti;

mwaka uliofuta 2012/2013, fedha za nje zilikuwa shilingi trilioni 3.1 sawa na asilimia 21 ya bajeti; mwaka wa 2013/2014 fedha za nje zilikuwa shilingi trilioni 3.8 sawa na asilimia 21 ya bajeti; mwaka 2014/2015 fedha za nje zilikuwa shilingi trilioni 2.9 sawa na asilimia 15 ya bajeti; mwaka 2015/2016 fedha za nje zilikuwa shilingi trilioni 2.3 sawa na asilimia 10 ya bajeti; na mwaka huu wa fedha 2016/2017 fedha za nje zilikuwa shilingi trilioni 3.6 sawa na asilimia 12 ya bajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu unaendana kabisa na fundisho la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere linalosema *self-reliance is the means by which people develop.* (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali ichukue hatua ya kuyaelekeza mabenki ya kibiashara kuititia Benki Kuu ya Tanzania, kupunguza riba kama ambavyo wao wamepunguziwa ili wananchi waweze kukopa.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kutumia Mfumo wa Riba wa Soko Huru, ulichukuliwa na Serikali takribani miongo miwili iliyopita, baada ya mfumo ulikuwepo wa kudhibiti riba, kusababisha benki zetu kuwa na mikopo mikubwa chechefu na kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, tangu mfumo wa soko huria umeanza kutumika, mikopo iliyokwenda kwenye sekta binafsi imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, uwiano kati ya mikopo kwa sekta binafsi na Pato la Taifa ilipanda kutoka 4% mwaka 2000 hadi 16% mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa soko huria pia umesaidia kuelekeza mikopo kwenye shughuli za kiuchumi zenye tija zaidi na hivyo kuimarisha mchango wa sekta binafsi katika ukuaji wa uchumi. Kama wengi manavyojua, tumeshuhudia uchumi kukua kwa wastani wa 6.7% kila mwaka katika kipindi cha zaidi ya muongo mmoja uliopita. Hivyo, haitakuwa busara kurudi katika utaratibu wa kudhibiti riba ambapo hapo awali ultuletea shida. (*Makof*)

Aidha, Benki Kuu, ikiwa msimamizi wa benki za biashara, ikitoa maagizo ya kupunguza riba itakinzana na jukumu lake la kuzisimamia benki ipasavyo, maana endapo benki zitapata hasara, itakuwa vigumu kuzichukulia hatua, kwani Benki Kuu itakuwa imehusika katika kuzipangia riba.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu ili kuongeza ukwasi hivi karibuni yaani kupunguza *discount rate* na sehemu ya amana zinazowekwa Benki Kuu zinaonesha matokeo ya kushusha riba katika soko la jumla, ambapo riba ya mikopo ya siku moja baina ya benki za biashara imeshuka kutoka wastani wa 13% mwezi Disemba, 2016 hadi wastani wa 5% katika wiki mbili za kwanza za mwezi Juni, 2017.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo wastani wa riba ya dhamana za Serikali imeshuka kutoka 15.12% hadi asilimia 7.95. Matokeo haya yanaashiria kwamba riba za kukopesha nazo zitashuka kutokana na nguvu za soko.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo kwa sasa ni kuongezeka kwa mikopo chechefu ambayo inafanya benki zifanye tahadhari kubwa katika kutoa mikopo pamoja na kuendelea kutoza riba kubwa. Benki Kuu imezielekeza benki zenye uwiano mkubwa wa mikopo chechefu ziweke mikakati ya kurudisha uwiano huo kwenye kiwango kinachotakiwa cha 5% na kuzihimiza kutumia taarifa za *Credit Reference Bureaus* ili kupunguza mikopo chechefu na riba.

Mheshimiwa Spika, palikuwa na hoja ya malimbikizo ya VAT, na madai mbalimbali kwamba ni nini mkakati wa Serikali kulipa malimbikizo hayo?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kufungua akaunti ya *Escrow* kwa ajili ya kufanya marejesho ya madai yanayotokana na ununuzi wa sukari inayotumika viwandani na hivyo kuondoa changamoto zilizokuwepo kama nilivyotangaza siku niliposoma hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai mbalimbali (*arrears*), Serikali inaendelea kuyahakiki na kulipa. Kama nilivyoeleza katika hotuba ya bajeti, hadi mwezi Juni, 2016 madai yaliyokuwa yamewasilishwa na taasisi mbalimbali yalikuwa ya jumla ya shilingi bilioni 2934.4 ambapo jumla ya shilingi bilioni 1997.9 sawa na asilimia 68.1 zilithibitika kuwa madai halali baada ya uhakiki.

Mheshimiwa Spika, kati ya madai yaliyohakikiwa, Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 796.5 hadi iliopofikia mwezi Machi, 2017 na hivyo kubakia na madai ya shilingi bilioni 1201.4 ambayo yataendelea kulipwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Madai yaliyolipwa; wakandarasi wamelipwa jumla ya shilingi bilioni 632.1, wazabuni shilingi bilioni 78.8, watumishi shilingi bilioni 67.5 na watoa huduma shilingi bilioni 17.8.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga shilingi bilioni 1,000 kwa ajili ya kuendelea kulipa madai hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marejesho ya VAT Serikali imeboresha utaratibu wa uhakiki ili kudhibiti changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba fedha za maendeleo zinaonekana kuwa nyingi kwa kuwa zimechanganywa pamoja na fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, nitasema tu kwa kifupi kwamba uwekezaji katika elimu ndiyo uwekezaji bora (*is the best investment*), hivyo kuwezesha vijana wa Kitanzania kusoma elimu ya juu kwa kuwapatia mikopo, ni uwekezaji wa kimaendeleo kwa hakika na ndiyo maana ni lazima ziwekwe kwenye fedha za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba bajeti ya mwaka ujao wa fedha haina chochote kuhusu Benki ya Wakulima iliyoanzishwa mwaka 2015 kwa kusudio la mtaji

wa shilingi triliuni moja na kukopesha wakulima 200,000 kwa mwaka, lakini sasa imeishia kukopesha wakulima 3,700 na mtaji wa shilingi bilioni 60 tu kwa miaka mitano. Mbali na shilingi bilioni 60 za awali, Serikali imeshaipatia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*) fedha zaidi za kuongeza mtaji ambazo ni shilingi bilioni 209.5, baada ya Serikali na *TADB* kutia saini mkataba wa fedha hizo mnamo tarehe 5 Juni, 2017. Fedha hizo zinatokana na mkopo wa Serikali kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) na ni sehemu ya utekelezaji kwa awamu azma ya Serikali ya kuipatia benki hiyo mtaji wa angalau shilingi bilioni 800. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea sasa ni taratibu za kibenki za kuhakikisha miamala stahiki inafanyika kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika na *TADB*, hii ikijumlisha pia Benki Kuu ya Tanzania kupokea fedha hizo kwa dola za Kimarekani ambazo ni millioni 93.5 na kuzibadilisha na kuzilingiza kwenye akaunti ya *TADB* kwa shilingi za Kitanzania zilizotajwa.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinategemewa kuongeza kiasi cha mikopo itakayotolewa kwa wakulima na wafugaji na pia kuiwezesha benki kutekeleza mapango wake mpya wa kuwafikia wakulima nchi nzima kwa utaratibu maalum (*clustery*).

Aidha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo tayari imefanya mawasiliano rasmi na Makatibu Tawala wa Mikoa yote nchi na Wizara ya Kilimo, Utalii, Mifugo na Uvuvi na ile ya Viwanda na Biashara ya Zanzibar na kuwaomba waainishe na kuwasilisha katika benki hiyo miradi ya kilimo ya kipaumbele ambayo mikoa yao inapendekeza izingatiwe zaidi katika kupatiwa mikopo na benki.

Mheshimiwa Spika, kuiongezea mtaji benki yetu ya kilimo, ni sehemu ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano wenyе lengo la kufungamanisha maboresho ya sekta ya kilimo na mpango mpana wa nchi kuelekea uchumi wa viwanda na hususan viwanda vile vinavyotegemea kiasi kikubwa malighafi zinazotokana na mazao ya kilimo ya ndani ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa hii Benki ya Kilimo na benki nyingine za maendeleo zinawezeshwa ili kuchangia maendeleo ya kilimo na viwanda kama ilivyodhamiliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kuwa kama nilivyoeleza katika hotuba zangu, hatua zilizopendekezwa kwenye bajeti hii, zinalenga kujenga msingi madhubuti wa uchumi wa viwanda na kupanua fursa za ajira na biashara.

Mheshimiwa Spika, dhamira yetu sote ni kufikia kiwango cha uchumi wa kipato cha katii itakapofika mwaka 2025. Ili kushiriki katika mafanikio hayo, ni lazima kila mmoja wetu atakayeshiriki katika shughuli halali ya uzalishaji au kutoa huduma na afanye hivyo kwa juhudini na maarifa ili kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa bajeti hii kunahitaji nidhamu ya hali ya juu katika usimamizi wa mapato na matumizi. Ili kufikia azma hii, juhudini ya pamoja kati ya Serikali na wadau wote zinahitajika ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi kwa kuwekeza zaidi katika maeneo ya kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa kila Mtanzania kutimiza wajibu wake hususan kulipa kodi stahiki ili bajeti hii iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa na kama Waheshimiwa Wabunge mlivyositisita.

Mheshimiwa Spika, napenda nirudie maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwamba kila mwananchi akinunua kitu au huduma, adai risiti na yule anayeuzua kitu au huduma na yeye atoe risiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru sana watumishi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake zote kuanzia wahudumu wetu ambao walikesha na sisi usiku kucha ili kuandaa bajeti nzuri kwa Watanzania. Niseme kwa lugha ya kigeni *I am proud of you and keep it up in service of our mother land. Maintain professionalism and integrity.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi/Vigelegele*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono hadi na Wabunge, imepigiwa na vigelegele. Nawashukruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuunga mkono hoja hii *overwhelmingly*.

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango kwa majumuisho ya hoja yako yaliyofafanua hoja mbalimbali na kuweka sawa mambo mbalimbali na kuzingatia sana maoni ya Wabunge yaliyotolewa kwa muda wa karibu wiki nzima. Kwa kweli umekuwa msikilizaji safari hii, umeweuka recordkubwa kabisa. (*Makofi*)

Sasa mtihani wako mmoja tu mwakani kuvunja record yako, maana mwanariadha lazima avunje record; lakini record ya mwaka huu tunakuvulia kofia. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakutana hapa kwa ajili ya kufanya maamuzi ya kuhusiana na hoja hii, ambapo kama nilivyoeleza mwanzo, Katiba ya nchi inatutaka tufanye uamuzi na kura; maelezo yake tutayotoa hapo jioni.

Kura zitakuwa tatu; kura moja ya kukubali "Ndiyo"; kura ya kukataa "Siyo", na kura ya ku- "*Abstain*" lakini maelezo yake tutayatoa jioni. Kura hii ni katika kura muhimu sana kwa sababu Kikatiba tukiipitisha bajeti hii kama ambavyo wajibu wetu sisi Wabunge ulivyo, kwa kuiwesha Serikali, tutakuwa tumeipa Serikali nafasi ya kutekeleza mipango hii tulioizungumza Bungeni hapa na ambayo imekubalika kwa mwaka ujao wa fedha.

Waheshimiwa Wabunge, likitokea lisilotarajiwa kwamba bajeti hii imekataliwa, basi maana yake na sisi

wenyewe sio Wabunge kuanzia wakati huo, tunaenda katika uchaguzi. Kwa hiyo, siyo uamuzi wa mchezo mchezo. (*Makofii*)

Kwa wale wenzetu ambao wanapendaga kipindi kama hicho Mbunge mmoja mmoja kutaka labda kutoka nje au nini, ruksa, lakini unatoka taratibu. Hata mkiwa kumi au wangapi, haya, lakini kwa amani na salama, japo sitarajii jambo kama hilo, lakini likitokea sitashangaa.

Nina matangazo madogo mawili; moja, ni la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, ana wageni wake kutoka Zanzibar huko ambao ni dada yake Ndugu Veronica, mdogo wake Ndugu Enedi na Mkwe wake Ndugu Zakia. Wote hao nawakaribisha hapa Bungeni. Zanzibar mbali bwana, karibuni sana, mmevuka bahari, karibuni sana. (*Makofii*)

Pia nina tangazo la Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Katibu wa Wabunge wa CCM, anawataarifu Wabunge wa CCM kwamba kutakuwa na Kikao cha Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi saa 2.00 usiku, *White House*. Mheshimiwa Jasson anasema, saa 2.00 usiku *White House* Wabunge wote wa CCM mnatakiwa mhudhurie kule. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Futari.

SPIKA: Kwa kweli nadhani tusogeze, tufanye saa 3.00 ili iende vizuri. Kwa ruhusa yako Mheshimiwa Jasson tufanye saa 3.00 usiku ili futari ipate nafasi yake. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Tumekuwa tukiandaa baadhi ya hizi shughuli, siku ile ya Bajeti tulipata nafasi ya kupata futari iliyokuwa imeandaliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na wageni wote walikuwepo, Mabalozi na kadhalika wote tulihudhuria pale na ilikuwa imeandaliwa kwa wema kwa kweli, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuandaa futari ile. Leo pia na mimi nimepata nafasi, naandaa kama nilivyowataarifuni. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nimejifunza kitu kimoja ambacho sikupenda sana kukisema, lakini nikisema hapa kidogo. Kuna baadhi ya wenzetu wengi wamekatazana rasmi kuhudhuria shughuli kama hizo.

Sasa mimi sitaki kuingilia uhuru wao, wana haki ya kufanya hivyo, kama wanaona ni sawa sawa, lakini mimi mwenzao ningependa kuwashauri tu hasa viongozi wanaofanya mambo hayo kutazama tena njia zao, yapo mambo mengine ni ya kijamii tu. (*Makofi*)

Ukifika mahali kiongozi unaanza kuwazuia watu hata mambo ya kijamii, ujue unaenda mbali kidogo. Kwa sababu kwa bahati nzuri Bunge linavyoendeshwa hili, labda Wabunge wengine wanaweza wasielewe hasa wa Kambi mbalimbali. Hili Bunge linavyoendeshwa, linaendeshwa katika namna ya mawasiliano mengi sana ya sisi kwa sisi. Endapo kuna jambo ambalo linakwaza, linasababisha hata watu wasiweze kupata futari kwa pamoja, basi ni vizuri viongozi wa pande hizo tukakaa tukaondoa vikwazo hivyo kama viro, maana mimi sjui. (*Makofi*)

Lakini kama havipo, basi ni ushauri wangu kwamba tuwe tunajumuika, kwa sababu sera hizo zikienea nina hakika kabisa na pande nydingine nazo zitaanza na nina hakika matokeo yake ni mipasuko ambayo hakuna anayeihitaji hapa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Najua mnanijibu, mnafanya mnayoyafanya lakini Mwenyezi Mungu anajua kwamba mnachokifanya siyo busara katika kufanya hivyo. (*Makofi*)

Huu ni mwezi Mtukufu, mwezi ambao kama wewe ni muislamu au sio muislamu, ni mwezi wa kusamehe hata pamoja na maaduni zako, ni mwezi wa kuzungumza na wenzako, ni mwezi wa kutoa mkono upande wa pili, ndiyo maana ya ibada. Siyo mwezi wa chuki na kubaguana na kadhalika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, baada ya maneno hayo, nawakaribisha tena kwenye futari wale watakaokuwa na nafasi ya kufika, wasiofika, *inshallah*, kila la kheri, tutaendelea kuwa pamoja hapa hapa, mjengo huu huu, lakini niwahakikishie, tuna-*take note*. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo kama nilivyosema saa 10.00 jioni tutaanza zoezi lile la kupiga kura. Kwa hiyo, naomba wote kabisa kuwahi.

Kwa jinsi hiyo basi, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Sasa ni wakati wa shughuli ambayo itahitimishwa kwa Wabunge kuhojiwa mmoja mmoja kadri maelezo yatakavyotolewa na Katibu hapa, kuhusu kupitisha au kutokupitisha, Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Kwa jinsi hiyo, *Sergeant-at-Arms* naomba ugonje kengele ili kuhimiza Wabunge wote walioko nje na mahali

engine popote waweze kuingia. Endelea na suala la kengele huko nje.

(Hapa kengele iligongwa ili kuruhusu Waheshimiwa Wabunge kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba tusikilizane ili tuweze kuendelea. Naomba waliosimama wakae tupate ushirikiano tuweze kwenda kwa pamoja maana yake tupo wengi hapa. Naomba wale waliosimama wakae tafadhalli; na wale mnaoongea hebu punguzeni kidogo sauti ili tuweze kusikilizana. Jambo hili linahitaji kusikilizana kwa umakini mkubwa, kwa sababu ni zoezi la Kikatiba.

Kwa kawaida inatakiwa tujue idadi wa Wabunge wallopo, lakini kwa kuwa kura hii ya Mbunge mmoja mmoja kwa kuitwa jina lake, nina hakika tunapofika mwisho ndiyo tunakuwa na idadi ambayo ina uhakika kabisa kuliko hii ya watu walivyokaa, maana unaweza ukamhesabu mtu, halafu akatoka nje asipige kura, itatuletea taabu baadaye kujua ikoje. Katibu atatuongoza baadaye utaratibu gani tutafuata.

Waheshimiwa Wabunge, nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo, kuhusiana na zoezi na utaratibu wa kupiga kura leo tarehe 20 Juni, 2017.

Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa tumeishahitimisha mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018, tunatakiwa sasa kufanya uamuzi na kuyapitisha au kutoyapitisha.

Kanuni ya 107(2) inaeleza kuhusu utaratibu wa kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Serikali. Kanuni hiyo inasomeka kama ifuatavyo; *“Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutoyapitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi, kwa kutaja jina la Mbunge mmoja mmoja.”*

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 94 (1) ya Katiba na Kanuni ya 77(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la

Januari, 2016, pamoja na mambo mengine zinazelekeza kwamba, akidi ya kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi ni nusu ya Wabunge wote.

Kwa kuwa idadi ya Wabunge wote ni 391, hivyo kabla ya kuanza zoezi la kupiga kura tunatakiwa kuwa na Wabunge tusiopungua 195 humu ndani. Kwa hiyo, hiyo ndiyo kazi ambayo Katibu atatuhakikishia kama tunazidi 195 na kwa kuangalia kwangu hapa naona kama mambo ni mazuri, lakini Katibu atatuthibitishia.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 79 (1) inafafanua kuwa: "mambo yote yanayohitaji kuamuliwa na Bunge, yataamuliwa kwa kufuata maoni ya Wabunge walio wengi, waliohuduria na kupiga kura Bungeni."

Hivyo, tutafuata utaratibu ufuatao; kwanza, kama nilivyoelekeza, kengele itapigwa ili Waheshimiwa Wabunge walio nje ya ukumbi waingie. Tumeshafanya hivyo hadi sasa; pili, Katibu atawahesabu Wabunge wote walio ndani ya ukumbi wa Bunge hili ili kuona kama akidi inatimia. Kwa hiyo, hapa tunachohitaji sisi atuambie tu kama tunazidi 195.

Tatu, zoezi la kupiga kura litaanza ambapo Katibu ataanza kusoma majina ya Waheshimiwa Wabunge mmoja baada ya mwingine na kila atakayeitwa...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Naomba tusikilizane ndugu zangu. Kila atakayeitwa ana mojawapo ya majibu matatu, ama Ndiyo, ama Hapana ama neno la kiingereza *Abstain*. *Abstain* mnajua maana yake nini.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo tutapatiwa matokeo ya kura kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Kwa kuwa sasa karibu tunaanza zoezi, baada ya Katibu kutuambia idadi yetu, natoa dakika moja au mbili

kama kuna mtu ana neno lolote, ana jambo lolote la kuhusu utaratibu, kabla sijamruhusu Katibu sasa tusonge mbele.

Hakuna, maana yake mmenipa ruhusa tusonge mbele. Katibu sasa tuendelee.

Katibu anashughulikia suala la idadi, halafu tutaendelea. Katibu tuendelee.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, idadi kamili ya Wabunge waliopo ndani kwa sasa ni 310 na inawezekana ikaongezeka kwa sababu kuna baadhi ya Wabunge wanaendelea kuinggia. Kwa hiyo tunaanza zoezi la kupiga kura.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyiningine nawaombeni sana, punguzeni sauti sana. Hata wewe mwenyewe ukisikia sauti za wenzako, utaona tu inakulazimu kwa kweli upunguze sauti, ili zoezi liweze kwenda vizuri, kila mtu asikike, anayesema Ndiyo isikike, anayesema Hapana isikike na anaye-*Abstain* isikike. Nawaombeni sana. Ikiwezekana kila mmoja atumie chombo wakati wa kusema mojawapo ya maneno hayo. Nawaombeni, siwazuui kusema, lakini punguza sauti sana. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, tutakwenda kwenye orodha tuliyonayo ambayo tunaitumia wakati wote wa kupiga kura, tutaanza na viongozi walioko ndani, halafu tutakwenda kwenye kundi maalum la Waheshimiwa Wabunge wenye udhuru, halafu tutakwenda kwa utaratibu wa Mawaziri na tutamalizia kwa utaratibu huo huo kwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Spika, nianze zoezi hili kama tulivyosema, tunaomba msiweke maneno mengi zaidi kwa sababu tuna-*record*. Ukiitwa, ujibu Ndiyo, Hapana au *Abstain*.

WABUNGE FULANI: *Abstain* kwa kiswahili.

SPIKA: Kwa Kanuni zetu, hayo ndiyo maneno matatu mtakayoyatumia. Hicho ndiyo kiswahili chake kwa leo. Ni Ndiyo, Hapana au *Abstain*. (*Kicheko/Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe, kura unayopiga leo ni kura ambayo pia Jimboni kwako, maana yake hupigi wewe kama wewe, unapiga kwa niaba ya wananchi wako. (*Makof*)

Naona mmelishangilia hili, labda nilieleze kwa nusu dakika kwa kuwa mmelishangilia sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Mabunge kama ya kwetu haya, au katika nchi kama za kwetu, baadhi ya watu huwa hawawekei kumbukumbu ya mwenendo wa Mbunge alipokuwa katika nafasi ya uongozi. Huko tunakoenda lazima tujue hiyo ni sehemu ya maisha tuliyonayo. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, mbona hamtaki nimalize, mnashangilia! Ninyi mshukuru mna Serikali inayoongozwa humu ndani na Mheshimiwa Majaliwa, mpole sana, kweli kabisa! Tutafika huko mbele siku moja, kwamba mimi niwe na nafasi hiyo, halafu unaniambia hapa hapana, halafu nipelekee watu wako maji, hawayapatil! (*Makof/Kicheko*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Kuwa Waziri Mkuu wiki moja. (*Kicheko/Makof*)

SPIKA: Katibu tuendelee, nilikuwa nafafanua tu.

NDG. DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Spika, naomba sasa tuanze zoezi la kura.

KUPIGA KURA

Mhe. Dkt. Tulia Ackson.....	Ndiyo
Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa.....	Ndiyo
Mhe. Freeman Aikaeli Mbewe.....	Hakuwepo
Mhe. Andrew John Chenge.....	Ndiyo
Mhe. Mussa Azzan Zungu.....	Ndiyo

Mhe. Najma Murtaza Giga.....	Ndiyo
Mhe. George Mcheche Masaju.....	Ndiyo
Mhe. Zaynabu Matitu Vulu.....	Ndiyo
Mhe. Subira Khamis Mgatu.....	Ndiyo
Mhe. Hamoud Abuu Jumaa.....	Ndiyo
Mhe. Ibrahim Hassanali Mohamedali	Ndiyo
Mhe. Mansoor Shanif Hiran.....	Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene.....	Ndiyo
Mhe. Angellah Jasmine Kairuki.....	Ndiyo
Mhe. January Yusuf Makamba.....	Ndiyo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama.....	Ndiyo
Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Augustine Philip Mahiga.....	Hakuwepo
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.....	Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe.....	Ndiyo
Mhe. Charles John Poul Mwijage.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako.....	Ndiyo
Mhe. Ummy Ally Mwalimu.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge.....	Ndiyo
Mhe. Selemani Said Jafo	Ndiyo
Mhe. Luhaga Joelson Mpina.....	Ndiyo
Mhe. Antony Peter Mavunde	Ndiyo
Mhe. William Tate Olenasha.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Edwin Amandus Ngonyani.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Ashatu Kachambwa Kijaji.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Merdard Matogolo Kalemani.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Susan Alphonse Kolimba.....	Ndiyo
Mhe. Angeline Sylvester Lubada Mabula.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Ramo Matala Makani.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla.....	Ndiyo
Mhe. Anastazia James Wambura.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni.....	Ndiyo
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia.....	Ndiyo

Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima..... Hakuwepo
Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa..... Ndiyo
Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab..... Ndiyo
Mhe. Jasson Samson Rweikiza..... Ndiyo
Mhe. Peter Joseph Serukamba..... Ndiyo
Mhe. Albert Obama Ntabaliba..... Ndiyo
Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu..... Hakuwepo
Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King..... Hakuwepo
Mhe. Capt. Mst. George Huruma Mkuchika..... Ndiyo
Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye..... Hakuwepo
Mhe. Vedasto Edgar Ngombale..... Hakuwepo
Mhe. Doto Mashaka Biteko..... Hakuwepo
Mhe. Raphael Japhary Michael..... Hapania
Mhe. Ruth Hiyob Mollel..... Hapania
Mhe. Ally Saleh Ally..... Hapania
Mhe. James Francis Mbatia..... Hapania
Mhe. John John Mnyika..... Hakuwepo
Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa Hapania
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya..... Hakuwepo
Mhe. Juma Hamad Omar..... Hapania
Mhe. Godbless Jonathan Lema..... Hakuwepo
Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare..... Hapania
Mhe. Esther Nicholas Matiko..... Hapania
Mhe. Antony Calist Komu..... Hapania
Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo..... Hapania
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel..... Hakuwepo
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi Hapania
Mhe. Hamidu Hassan Bobali..... Hapania
Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu..... Hakuwepo
Mhe. Joseph Michael Mkundi Hapania
Mhe. Pauline Philipo Gekul..... Hapania
Mhe. Yussuf Kaiza Makame..... Hapania
Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma..... Ndiyo (*Makof/*
Vigelegele)

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mzalendo!

MHE. HAWA A. GHASIA: Huyo ndio mwanaume huyo.
(*Makof*)

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

Mhe. David Ernest Silinde.....	Hapana
Mhe. Qambalo Willy Qulwi.....	Hapana
Mhe. John Wegesa Heche	Hapana
Mhe. Riziki Shahari Mngwali	Hapana
Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi	Hapana
Mhe. Mwita Mwikabe Waitara	Hapana
Mhe. Masoud Abdallah Salim	Hapana
Mhe. Salma Mohamed Mwassa	Hapana
Mhe. Cecilia Daniel Paresso.....	Hapana
Mhe. Cecil David Mwambe.....	Hapana
Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf.....	Hapana
Mhe. Zubeda Hassan Sakuru.....	Hapana
Mhe. Devotha Mathew Minja.....	Hapana
Mhe. Peter Ambrose Paciens Lijualikali.....	Hakuwepo
Mhe. Abdallah Ally Mtolea.....	Hapana
Mhe. Rashid Ali Abdallah	Hapana
Mhe. Maida Hamad Abdallah	Ndiyo
Mhe. Hamida Mohamed Abdallah.....	Ndiyo
Mhe. Munde Tambwe Abdallah.....	Ndiyo
Mhe. Bahati Ali Abeid	Ndiyo
Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood.....	Ndiyo
Mhe. Khadija Hassan Aboud.....	Ndiyo
Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi.....	Ndiyo
Mhe. Lameck Okambo Airo.....	Ndiyo
Mhe. Ajali Rashid Akbar.....	Ndiyo
Mhe. Stella Ikupa Alex	Ndiyo
Mhe. Abdallah Haji Ally.....	Hapana
Mhe. Jamal Kassim Ali	Ndiyo
Mhe. Khamis Mtumwa Ali.....	Ndiyo
Mhe. Mbarouk Salim Ali	Hapana
Mhe. Khadija Salum Ally	Hapana
Mhe. Hussein Nassor Amar.....	Ndiyo
Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Ndiyo
Mhe. Ussi Salum Pondeza Amjadi	Ndiyo
Mhe. Saul Henry Amon.....	Ndiyo
Mhe. Jumaa Hamidu Aweso.....	Ndiyo
Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Hakuwepo
Mhe. Omary Ahmad Badwel	Ndiyo

Mhe. Faida Mohamed Bakar.....Ndiyo
Mhe. Zainab Mussa Bakar.....Hapania
Mhe. Hussein Mohamed Bashe.....Ndiyo
Mhe. Innocent Lughia Bashungwa.....Ndiyo
Mhe. Mbaraka Salim BawazirHakuwepo
Mhe. Kasuku Samson Bilago..... Hapania
Mhe. Innocent Sebba BilakwateNdiyo
Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba.....Ndiyo
Mhe. Abdallah Majura Bulembo.....Ndiyo
Mhe. Halima Abdallah Bulembo..... Ndiyo (*Makofi*)
Mhe. Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga.....Ndiyo
Mhe. Selemani Said Bungara.....Hapania
Mhe. Felister Aloyce Bura.....Ndiyo
Mhe. Jerome Dismas Bwanausi.....Ndiyo
Mhe. Marwa Ryoba Chacha.....Hapania
Mhe. Josephine Tabitha Chagula.....Ndiyo
Mhe. Hawa Mchafu Chakoma.....Ndiyo
Mhe. Lathifah Hassan Chande.....Hapania
Mhe. Mary Pius Chatanda.....Ndiyo
Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni.....Ndiyo
Mhe. Sikudhani Yassini Chikambo.....Ndiyo
Mhe. Abdallah Dadi ChikotaNdiyo
Mhe. Dkt. Rashid Mohamed Chuachua.....Ndiyo
Mhe. Cosato David Chumi.....Ndiyo
Mhe. Mbaraka Kitwana Dau.....Ndiyo
Mhe. Dkt. David Mathayo David.....Ndiyo
Mhe. Mashaka Makame FoumNdiyo
Mhe. Tauhida Cassian Gallos Nyimbo..... Ndiyo
Mhe. Leonidas Tutubert Gama.....Ndiyo
Mhe. Alex Raphael Gashaza.....Ndiyo
Mhe. Josephine Johnson GenzabukeNdiyo
Mhe. Boniphace Mwita Getere.....Ndiyo
Mhe. Anna Joram Gidarya.....Hapania
Mhe. Seif Khamis Said GulamaliNdiyo
Mhe. Haji Ameir Haji.....Ndiyo
Mhe. Miza Bakari Haji Hapania
Mhe. Mwantumu Dau Haji.....Ndiyo
Mhe. Othman Omar Haji..... Hakuwepo
Mhe. Khatib Said Haji Hapania
Mhe. Azza Hillal Hamad.....Ndiyo

Mhe. Juma Kombo Hamad.....	Hapana
Mhe. Paschal Yohana Haonga.....	Hapana
Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga.....	Ndiyo
Mhe. Joseph Leonard Haule.....	Hapana
Mhe. Juma Othman Hija.....	Ndiyo
Mhe. Augustine Vuma Holle.....	Ndiyo
Mhe. Joram Ismael Hongoli	Ndiyo
Mhe. Yussuf Salim Hussein.....	Hapana
Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma.....	Ndiyo
Mhe. Khalifa Mohamed Issa.....	Hapana
Mhe. Zacharia Paulo Issaay.....	Hakuwepo
Mhe. Asha Mshimba Jecha.....	Ndiyo
Mhe. Emmanuel Papian John.....	Ndiyo
Mhe. Asha Abdallah Juma.....	Ndiyo
Mhe. Juma Ally Juma	Ndiyo
Mhe. Mwantakaje Haji Juma	Ndiyo
Mhe. Jafar Sanya Jussa.....	Ndiyo
Mhe. Ritta Enespher Kabati	Ndiyo
Mhe. Risala Saidi Kabongo	Hapana
Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka	Hapana
Mhe. Mgeni Jadi Kadika.....	Hapana
Mhe. John Peter Kadutu.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu.....	Ndiyo
Mhe. Haji Khatib Kai.....	Hapana
Mhe. Moshi Selemani Kakoso.....	Ndiyo
Mhe. Joseph George Kakunda.....	Ndiyo
Mhe. Bonnah Moses Kaluwa	Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Diidorus Buberwa Kamala.....	Ndiyo
Mhe. Vicky Paschal Kamata.....	Ndiyo
Mhe. Josephat Sinkamba Kandege.....	Ndiyo
Mhe. Maria Ndila Kangoye.....	Ndiyo
Mhe. Constantine John Kanyasu.....	Ndiyo
Mhe. Sebastian Simon Kapufi	Ndiyo
Mhe. Katani Ahmad Katani.....	Hakuwepo
Mhe. Zainab Athman Katimba.....	Ndiyo
Mhe. Hassan Seleman Kaunje.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa.....	Ndiyo
Mhe. Kan. Mst. Masoud Ali Khamis.....	Ndiyo
Mhe. Yussuf Haji Khamis.....	Hapana
Mhe. Sadifa Juma Khamis.....	Ndiyo

Mhe. Ali Salim Khamis Hapana
Mhe. Fakharia Shomar Khamis.....Ndiyo
Mhe. Mohammed Juma Khatib..... Hapana
Mhe. Munira Mustapha Khatibu..... Hapana
Mhe. Aida Joseph Khenani..... Hapana
Mhe. Omari Abdallah Kigoda.....Ndiyo
Mhe. Mendrad L. Kigola.....Ndiyo
Mhe. Omari Mohamed Kigua Ndiyo
Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe.....Ndiyo
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete.....Ndiyo
Mhe. Salma Rashid Kikwete.....Ndiyo (*Makofi*)
Mhe. Ali Hassan Omar King.....Ndiyo
Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu..... Hakuwepo
Mhe. Mariam Nasoro KisangiNdiyo
Mhe. Jumanne Kibera Kishimba.....Ndiyo
Mhe. Jesca David Kishoa..... Hapana
Mhe. Kiswaga Boniventura Destery.....Ndiyo
Mhe. Dunstan Luka KitandulaNdiyo
Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga.....Ndiyo
Mhe. Allan Joseph Kiula.....Ndiyo
Mhe. Susan Limbweni Kiwanga.....Ndiyo
Hapana, hapana, hapana!! (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

(Hapa Wabunge wa CCM waliimba CCM, CCM,CCM)

MBUNGE FULANI: Ita mwininge, Watu wetu hao.
Imetoka hiyo! (*Kicheko/Makofi*)

Mhe. Grace Sindato Kiwelu Hapana

MHE. PAULINE P. GEKUL: Hiyo ndiyo tunaifanyaje sasa?
Mbona Mheshimiwa Pinda alikosea?

Mhe. Sylvester Francis Koka..... Hakuwepo
Mhe. Leah Jeremia KomanyaNdiyo

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika,
samahani sana kura yangu ni ya hapana. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane ndugu zangu.

Naomba tumhakikishie Mheshimiwa Susan Kiwanga kwamba pamoja na kwamba hana barabara, hana nini, hana nini kule, lakini kasema bajeti haitaki. Ni hapana hapo andika. Kazi kwenu Mawaziri. (*Makof*)

Naomba tunyamaze ili tuendelee na kura.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

Mhe. Yosepher Ferdinand Komba.....	Hapana
Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma.....	Ndiyo
Mhe. Saed Ahmed Kubenea	Hapana

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Kwa rekodi zetu, tunaomba turudie.

Mhe. Leah Jeremia Komanya	Ndiyo
Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka.....	Hapana
Mhe. Rhoda Edward Kunchela.....	Hapana
Mhe. Elias John Kwandikwa.....	Ndiyo
Mhe. Julius Kalanga Laizer.....	Hapana
Mhe. George Malima Lubeleje.....	Ndiyo
Mhe. Kangi Alphaxard Ndege Lugola	Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida	Hapana
Mhe. Anna Richard Lupembe	Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde	Ndiyo
Mhe. Kemilembe Julius Lwota.....	Ndiyo
Mhe. Hamad Salim Maalim.....	Hapana
Mhe. Amina Iddi Mabrouk.....	Ndiyo
Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula.....	Ndiyo
Mhe. Khamis Yahaya Machano	Ndiyo
Mhe. Lucy Simon Magereli.....	Hapana
Mhe. Catherine Valentine Magige	Ndiyo
Mhe. Esther Alexander Mahawe	Ndiyo
Mhe. Almas Athuman Maige	Ndiyo
Mhe. Ezekiel Magolyo Maige	Ndiyo
Mhe. Kunti Yusuph Majala	Hapana

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Salome Wycliffe MakambaHapana
Mhe. Makame Kassim MakameNdiyo
Mhe. Joel Mwaka MakanyaagaNdiyo
Mhe. Amina Nassoro MakilagiNdiyo
Mhe. Hussein Ibrahim Makungu Ndiyo
Mhe. Tunza Issa MalapoHapana
Mhe. Anne Kilango MalecelaHakuwepo
Mhe. Angelina Adam MalembekaNdiyo
Mhe. Ignas Aloyce Malocha Ndiyo
Mhe. Issa Ali MangunguNdiyo
Mhe. Vedastus Mathayo ManyinyiNdiyo
Mhe. Sixtus Raphael MapundaNdiyo
Mhe. Agness Mathew MarwaNdiyo
Mhe. Gimbi Dotto Masaba Hapana
Mhe. Hassan Elias MasalaNdiyo
Mhe. Stephen Julius Masele.....Ndiyo
Mhe. Augustino Manyanda MaseleNdiyo
Mhe. Susanne Peter MaselleNdiyo
(Makofi)

(Hapa baadhi ya Wabunge walishangilia)

Mhe. Susanne Peter MaselleHapana

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Bajeti haijapata kutokea hii. *(Makofi/Kicheko)*

WABUNGE FULANI: CCM, CCM, CCM.

Mhe. Susanne Peter Maselle Hapana

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Naomba utulivu ndani ya nyumba ili tuweze kuendelea vizuri.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Naomba utulivu wenu Waheshimiwa Wabunge, halafu tumsikilize Katibu.

Mhe. Susanne Peter Maselle Hapana

MBUNGE FULANI: Aaaaah.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

Mhe. Yahaya Omary Massare Ndiyo
Mhe. Flatei Gregory Massay Ndiyo
Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe Hakuwepo
Mhe. Silafu Jumbe Maufi
Mhe. Lucy Thomas Mayenga Ndiyo

MHE. SILAFU J. MAUFI: Silafu Maufi nipo, Ndiyo

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

Mhe. Mussa Bakari Mbarouk Hapana
Mhe. Prosper Joseph Mbena Ndiyo
Mhe. Janeth Zebedayo Mbene Ndiyo
Mhe. Richard Philip Mbogo Ndiyo
Mhe. Taska Restituta Mbogo Ndiyo
Mhe. Mwanne Ismail Mchemba Ndiyo
Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki Hapana
Mhe. Bhagwanji Maganalal Meisuria Ndiyo
Mhe. Neema William Mgaya Ndiyo
Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa Ndiyo
Mhe. Godfrey William Mgimwa Ndiyo
Mhe. Suzana Chogisasi Mgonokulima Hapana
Mhe. Omary Tebweta Mgumba Ndiyo
Mhe. Joseph Kizito Mhagama Ndiyo
Mhe. Mboni Mohamed Mhita Ndiyo
Mhe. Esther Lukago Midimu Hakuwepo
Mhe. James Kinyasi Millya Hakuwepo
Mhe. Desderius John Mipata Ndiyo
Mhe. Nimrod Elirehema Mkono Hakuwepo
Mhe. Martha Moses Mlata Ndiyo
Mhe. Goodluck Asaph Mlinga Ndiyo
Mhe. Lucia Michael Mlowe Hapana
Mhe. Ester Michael Mmasi Ndiyo
Mhe. Ally Keissy Mohamed Ndiyo

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Halima Ali MohammedHapana
Mhe. Twahir Awesu MohammedHapana
Mhe. Amina Saleh MolelNdiyo
Mhe. Daimu Iddi MpakateNdiyo
Mhe. Dkt. Hadji Hussein MpondaNdiyo
Mhe. Maryam Salum MsabahaHapana
Mhe. Jacqueline Ngonyani MsongoziNdiyo
Mhe. Martin Mtonda MsuhaNdiyo
Mhe. Daniel Edward MtukaNdiyo
Mhe. Maulid Said MtuliaHapana
Mhe. Muhammed Amour Muhammed Hapana
Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo Hakuwepo
Mhe. Oscar Rwegasira MukasaNdiyo
Mhe. Joyce John MukyaHapana
Mhe. Phillipo Augustino MulugoNdiyo
Mhe. Mary Deo MuroHapana
Mhe. Benardetha Kasabago MushashuHakuwepo
Mhe. Mussa Hassan MussaNdiyo
Mhe. Raisa Abdallah MussaHapana
Mhe. Joseph Kasheku MusukumaNdiyo
Mhe. Hawa Subira MwaifungaHapana
Mhe. Frank George MwakajokaHapana
Mhe. Sophia Hebron MwakagendaHapana
Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ataNdiyo
Mhe. Emanuel Adamson MwakasakaNdiyo
Mhe. Fredy Atupele MwakibeteNdiyo
Mhe. Edward Franz MwalongoNdiyo
Mhe. Victor Kilasile MwambalaswaNdiyo
Mhe. Venance Methuselah MwamotoNdiyo
Mhe. Zainabu Nuhu MwamwindiNdiyo
Mhe. Dkt. Mary Machuche MwanjelwaNdiyo
Mhe. Savelina Silvanus MwijageHapana
Mhe. Abbas Ali MwinyiNdiyo
Mhe. Mariam Ditopile MzuzuriNdiyo
Mhe. Shamsi Vuai NahodhaHakuwepo
Mhe. Joshua Samwel NassariHapana
Mhe. Suleiman Masoud Nchambi Hakuwepo
Mhe. Mashimba Mashauri NdakiNdiyo
Mhe. Richard Mganga NdassaNdiyo
Mhe. Dkt. Faustine Engelbert NdugulileNdiyo

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Deogratias Francis Ngalawa	Ndiyo
Mhe. William Mganga Ngeleja	Ndiyo
Mhe. Stephen Hillary Ngonyani	Hakuwepo
Mhe. Ahmed Juma Ngwali	Hapana
Mhe. Oran Manase Njeza	Ndiyo
Mhe. Juma Selemani Nkamia	Ndiyo
Mhe. Dua William Nkurua	Ndiyo
Mhe. Nape Moses Nnauye	Ndiyo
Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko	Ndiyo
Mhe. Musa Rashid Ntimizi	Ndiyo
Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu	Ndiyo
Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo	Ndiyo
Mhe. Nassor Suleiman Omar	Hapana
Mhe. Lucy Fidelis Owenya	Hapana
Mhe. Upendo Furaha Peneza	Hapana
Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed	Ndiyo
Mhe. Shally Joseph Raymond	Ndiyo
Mhe. Salum Mwinyi Rehani	Ndiyo
Mhe. Catherine Nyakao Ruge	Hapana
Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare	Ndiyo
Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza	Hapana
Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq	Ndiyo
Mhe. Machano Othman Said	Ndiyo
Mhe. Saumu Heri Sakala	Hapana
Mhe. Mattar Ali Salum	Ndiyo
Mhe. Ahmed Ally Salum	Ndiyo
Mhe. Salum Khamis Salum	Ndiyo
Mhe. Saada Mkuya Salum	Ndiyo
Mhe. Deo Kasenyenda Sanga	Ndiyo
Mhe. Edwin Mgante Sannda	Ndiyo
Mhe. Njalu Daudi Silanga	Ndiyo
Mhe. Joseph Roman Selasini	Hapana
Mhe. Oliver Daniel Semuguruka	Ndiyo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby	Ndiyo
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi	Ndiyo
Mhe. Shaabani Omari Shekilindi	Ndiyo
Mhe. Juliana Daniel Shonza	Ndiyo
Mhe. Mussa Ramadhan Sima	Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta	Ndiyo
Mhe. Joyce Bitta Sokombi	Hapana

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Jitu Vrajjal Soni	Ndiyo
Mhe. Rose Kamil Sukum	Hapana
Mhe. Khalifa Salum Suleiman	Ndiyo
Mhe. Sabreena Hamza Sungura	Hapana
Mhe. Grace Victor Tendega	Hapana
Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest	Hapana
Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka	Ndiyo
Mhe. Dkt. Charles John Tizeba	Ndiyo
Mhe. Fatma Hassan Toufiq	Ndiyo
Mhe. Salim Hassan Turky	Hakuwepo
Mhe. Rose Cyprian Tweve	Ndiyo
Mhe. Abdallah Hamis Ulega	Ndiyo
Mhe. Martha Jachi Umbulla	Ndiyo
Mhe. Ally Seif Ungando	Ndiyo
Mhe. Khamis Ali Vuai	Ndiyo
Mhe. Selemani Jumanne Zedi	Ndiyo
Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto.....	Hakuwepo

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Spika, hapo ndiyo mwisho wa orodha yetu.
Kama kuna Wabunge walioingia baada ya hapo, tunaomba tuwatambue.

SPIKA: Naomba Wabunge ambao wakati Katibu anaita majina hapa mlikuwa ama hampo ama mlirukwa ama kwa vyovyote vile hamjapiga kura sasa msimame pale mliro na tutatumia utaratibu atakaouelekeza Katibu. Tufuate utaratibu gani, Katibu.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Tuite mmoja mmoja.

SPIKA: Haya Katibu endelea kuwaita mmoja mmoja. Endeleeni kusimama, ukiitwa ndiyo ukae.

Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel	Hapana
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya	Ndiyo
(Makof)	

(Hapa baadhi ya Wabunge walishangilia)

SPIKA: Chombo hakifanyi kazi, hiyo *microphone* yako haifanyi kazi?

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Kwa maendeleo ya Kaliua, Ndiyo.

SPIKA: Eeh unatakiwa usikike.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Kwa maendeleo ya Kaliua, Ndiyo. (*Makofi*)

(Hapa Wabunge walishangilia kwa makofi na vigelegele)

MBUNGE FULANI: Apelekewe maendeleo.

SPIKA: Katibu endelea.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

Mhe. Zacharia Paulo IssaayNdiyo
Mhe. Othman Omar HajiHapana
Mhe. Prof. Norman Sigalla KingNdiyo

SPIKA: Kuna mkono kule nyumba eeh! Bado Katibu.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Silafu Maufi sikusikia jina langu vizuri. Silafu Maufi, Ndiyo. (*Makofi*)

MHE. HAWA A. GHASIA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Tusubiri, nitaichukua baada ya matokeo kutoka, nimeshaona miongozo miwili, muda ukifika nitawaita.

MBUNGE FULANI: Tuko wengi.

SPIKA: Wote mtapata nafasi leo, tuna muda mpaka futari ifike! (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tuwape nafasi sasa meza ya Katibu wafanye kazi ya kufanya *tallying* ili tupate majibu ya uhakika.

(Hapa Zoezi la Kuhesabu Kura Lilianza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati Katibu na timu yake wanaenda kuhesabu, najua walitambulishwa asubuhi lakini kipekee niwatambulishwa tena. Kuna wazee ambao wapo kwenye *gallery* yangu pale, wazee wa *Tanzania Legion*, wale wazee waliopigana kwenye Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Wale mnaoweza wazee wangu naomba msimame hapo mlipo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wazee hawa ni viongozi wa chama hicho cha Wapiganaji wa Vita ya Dunia iliyoisha mwaka 1945. Wengi wao wana miaka 90 na kwenda mbele na mnawaona bado ni wazima, wanawenza kupiga tai sawasawa. Karibuni sana wazee wangu na nilitangazie Bunge kwamba tarehe 27 Julai, 2017 kama sikosei, wazee hao kutoka nchi nzima ya Tanzania watakuja hapa Dodoma na watavaa mavazi yale waliyokuwa wanavaa wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia na watapiga gwaride hapa Dodoma kwenye uwanja wa Jamhuri kwa mwendo waliokuwa wakienda enzi hiso wakiwa na makamanda wao wa enzi hiso. Kwa hiyo, watu wa Dodoma na Waheshimiwa Wabunge kama mtakuwepo tarehe hiso ni vizuri sana kuwaona wazee wetu wakifanya mambo hayo. *(Makofi)*

Naomba sasa mkae na karibuni sana, wazee wetu tunawapenda sana na mtume salamu kwa wazee wenzenu popote pale walipo. Pia muwaambie Waziri wa Fedha leo amewasamehe kulipa kodi ya nyumba zenu wote mlioko mijini, ninyi wa zaidi ya miaka 60 kwenda mbele hamtalipa kodi hiyo. Kwa hiyo, kuna kila sababu kusema kwamba bajeti hii ni nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wazee hawa leo nilipokuwa nazungumza nao wameniongezea historia kidogo wakaniambia kwamba ile Vita Kuu ya Pili ya Dunia ilipoisha,

wapiganaji wa Tanganyika waliporudi nyumbani kutoka Burma, Egypt na mahali pengine wote waliletwa Kongwa kwanza. (*Makof*)

Baada ya kufika pale ndiyo wakafanyiwa ule utaratibu wa kuondoka jeshini kwa kuangalia huyu anaenda kufanya nini na kupewa masuala ya kuwa raia (*civilian*), huyu anaenda kufanya kitu gani anaandaliwa kwa maana hiyo, yule anataka kufanya jambo gani akitoka pale anaandaliwa kwa maana hiyo lakini vilevile kujua huyu anatoka mkoa fulani ili kuandaliwa usafiri. Kwa hiyo, Kongwa ndiyo palikuwa kambi kubwa ya wapiganaji wote hawa waliopigana wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, hizi ni historia muhimu ambazo lazima tuendelee kuwa nazo zinasaidia sana kuona kama Taifa tunatoka wapi, tuko wapi na tunaelekea wapi. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa uendelee kuwalea wazee hawa, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria uendelee kuwalea wazee hawa na Waheshimiwa Mawaziri wote mnaohusika hasa mwenyewe Mheshimiwa Ummy Mwalimu, wazee hawa ni sehemu ya *portfolio* yako, tuendelea kuwa nao. Lakini huwa najiuliza, hii Vita Kuu ya Dunia wanawake hawakupigana? Sijawahi kukutana na mzee mwanamke aliyepigana vita hii. Kama wapo itakuwa vizuri sana tuweze kuwaona pia na tuchukue historia yao tuiweke mahali pake. Ahsanteni sana. (*Makof*)

Sasa kwa kuwa Katibu anahesabu na hatujui atachukua muda gani badala ya kukaa na kunyamaza hapa, mimi naona tuchukue miongozo iko mitatu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Tunaanza, Mheshimiwa Waitara halafu Mheshimiwa Sugu, haya ninyi wawili kaeni. Mheshimiwa Kitwanga, unakaa huko siku hizi? Mwingine?

MHE. HAWA A. GHASIA: Hawa Ghasia.

SPIKA: Mheshimiwa Hawa kaa, Mheshimiwa Msukuma nimekuona, Mheshimiwa Waziri nimekuona.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Amina.

SPIKA: Amina nani?

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mollel.

SPIKA: Haya wanatosha.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mlinga Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Kitwanga nimekuona.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mlinga.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Mlinga, naanza na Mheshimiwa Waitara halafu Mheshimiwa Sugu.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Natumia Kanuni ya 68(7) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 46(1).

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi wakati nauliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Kubenea, swali namba 424, Mheshimiwa Waziri alitoa majibu na ndiyo maana akatumia Kanuni ya 46(1).

SPIKA: Wengine hatukuwepo lilikuwa linahusu nini hilo swali?

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, lilikuwa linahusu Wizara ya Viwanda, kufufua Kiwanda cha Matairi kule Arusha (*General Tyre*). Mheshimiwa Kubenea alitaka kujua hatua iliyo fikia sasa ya kukifufua kiwanda hicho, lakini la pili alitaka kujua zimetumika shilingi ngapi mpaka hapo.

Mheshimiwa Spika, katika majibu Mheshimiwa Waziri hakueleza kama kiwanda kimefuliwa wala hakutaja mahali popote idadi ya fedha iliyotumika. Mbaya zaidi katika Kamati ya Viwanda Mheshimiwa Waziri aliwaambia hajapewa fedha ile shilingi milioni 100 iliyoombwa kufanya kazi ya utafiti ila alipewa shilingi milioni 50. Leo alipokuwa hapo nje akasema fedha zile alizosema humu ndani siyo kwamba alipewa kutoka bajeti kuu alitafuta kwenye vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitaka nijue ni kwa nini swalii hili halikujibiwa kikamilifu kwa sababu ni swalii ambalo limeulizwa mara nyingi sana na Wabunge hasa wa Mkoa wa Arusha na lina maslahi mapana ya Taifa, lakini kwenye Kamati yake aliomba na akalalamika kwamba fedha hajapewa, humu ndani akasema fedha amezipata, huko nje anasema fedha hizo siyo za bajeti kuu badala yake ni vyanzo vingine. Sasa kidogo ikawa imechanganya, nikataka nipate mwongozo wako katika masuala kama haya tunapouliza maswali ya msingi tupate majibu sahihi inakuwaje majibu yanakuwa siyo sawasawa?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako katika jambo hilo.

SPIKA: Hilo sidhani kama lina haja hasa ya kupewa nafasi sasa hivi kwa sababu Mawaziri wapo hapa hapa, mnaweza mkakutana mka-*clear* hilo jambo. Pili Waheshimiwa Wabunge tuache kuuliza maswali mawili mawili, unatakiwa mtu uulize swalii moja, sasa hapo Mheshimiwa Kubenea ameuliza mawili ndani ya swalii moja ndio maana wakati mwingine unaweza ukajibiwa mojawapo halafu ukasema lingine halijajibiwa na kadhalika. Mara nyingi tujielekeze kwenye kuuliza swalii moja ambalo linatakiwa na Waziri yupo na anafikika, kwa hiyo tufanyi hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Sugu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri bajeti yangu hii ni ya saba au ya nane lakini leo nimeshtuka na naomba Mwongozo katika hili pale ulipoelekeza Serikali kwa kuwataja Mawaziri kwamba tukipiga kura ya "Hapana" hawataleta maji na kadhalika. (*Makof*)

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, mimi nataka kufahamu, je, kuna Kanuni yoyote tumevunja kwa kupiga kura ya "Hapana" maana ulivyokuwa unatoa *introduction speech* ulisema tuna *option* tatu, kupiga kura ya "Ndiyo," "Hapana" au "Abstain." Wako watu walifika mbali ili wawe na uhakika wakakuuliza "Abstain" kwa Kiswahili wakitaka kupiga waseme nini ukasema kwa leo ni hivyo hivyo "Abstain," kwa hiyo ulitoa *option* tatu. Sasa unapiga mkwara kwamba tukichagua *option* mojawapo ambayo umetupa wasilete maji na unasisitiza Mawaziri wasikilize na wakati hela za maji ni kodi za wananchi wote pamoja na wale walituchagua sisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati unagombea ulisema anayekaa karibu na mgonjwa ndiye anayejua mahitaji. Wewe unakaa na wagonjwa wote, wa kipindupindu na sisi wa maralia, kwa hiyo, unajua mahitaji yetu sote. *Why unachagua upande like trying hard to kill democracy* katika Bunge? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa hili limeelekezwa kwangu ni vizuri kidogo nilieleze kwa sekunde chache ili tupate na nafasi ya miongozo mingine.

Waheshimiwa Wabunge, niliwakumbusha Wabunge kwamba sisi ni wawakilishi wa wananchi. Hakuna hata mmoja aliyejilita hapa kwa kutaka kwake yeye kama yeye kwamba mimi nataka kwenda Bungeni halafu akawa hapa, hayupo hata mmoja. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale waliopita njia kwa mfano ya kuchaguliwa, umechaguliwa na watu wa chama chako, umechaguliwa na watu wasiokuwa wa chama chako, umechaguliwa na watu wa dini yako, huenda umechaguliwa na watu wasiokuwa na dini yako yaani umechaguliwa na watu wa aina mbalimbali na wewe ndio msemaji wao, wewe ndio kiongozi wao. (*Makofi*)

Wakati wowote ni muhimu kwa Mbunge yejote yule kukumbuka unawakilisha *a wider group*, una watu wengi mgongoni kwako na wewe unapopiga kura hapa hupigi kura wewe kwa mdomo wako, wewe ni mdomo wa wale unaowawakilisha. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama wewe ni Mbunge unayewajibika, unaposema hapa "Ndiyo" maana yake hao unawawakilisha wamesema "Ndiyo," unaposema hapa "Hapana" maana yake hao unaowawakilisha wamekwambia useme "Hapana." (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa nini nimesema hivyo? Kama unaowawakilisha wamesema hawataki maji, sasa wewe ufanyaje, si unasema hawataki. Kwa hiyo, utaratibu ule ambao huwa nauona hapa Bungeni, wengine mnasema "Hapana," mnakatiza hapa, mnafanya mipango kwa Mawaziri na mimi nawashangaeni Mawaziri. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mbona wewe hujapiga kura?

SPIKA: Mtu anakataa bajeti machoni penu unaona anasema "Hapana," kesho anakuja anafanya mpango kwako unampa mradi lakini natambua pia kuna wanaosema "Hapana" wafanyaje maana wamelazimishwa, hilo najua, najua kabisa. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Katika kumalizia, maana mnapiga kelele hata siwasikii...

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Nimeulizwa ndio maana najibu. Ukiona mtu anasema "Hapana" kwa bajeti ambayo ina mshahara wake ye ye mwenyewe, halafu kesho mtu huyo anazunguka anakwenda kupokea mshahara walichosema "Hapana," basi unamsamehe bure au siyo jamani. (*Makofi/Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

SPIKA: Tunaendelea na Miongozo, Miongozo, Miongozo.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Spika.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kuhusu Utaratibu.

SPIKA: Mheshimiwa Waitara ni Miongozo, kaa chini.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Waitara, kaa chini ni Miongozo sasa.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

SPIKA: Utaratibu utachukuliwa baada ya Miongozo.

MHE. MWITA M. WAITARA: Haya sawa.

SPIKA: Shida yenu mkishaongea hamtaki wenzenu waongee, tunaendelea na utaratibu. Mheshimiwa Waziri wa Nchi halafu atafuata Mheshimiwa Kitwanga.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nadhani nirudi kwenye suala la Kanuni.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hizi ambazo zinaongoza shughuli mbalimbali ambazo ziko ndani ya Bunge letu Tukufu zimeweka utaratibu mzuri ambao unawaruhusu Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwakilisha wananchi wao katika mambo mbalimbali.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. MWITA M. WAITARA: Kanuni.

SPIKA: Hebu naomba tusikilizane, hizi fujo fujo hazisaidii sana. Nafikiri hata ninyi mlisikilizwa sasa muwasikilize na wenzenu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Una haraka gani anayekuwa *addressed* ni mimi.

MHE. MWITA M. WAITARA: *(Aliongea bila kutumia kipaza sauti).*

SPIKA: Mheshimiwa Waitara onyo la kwanza. *(Makofi)*

MHE. MWITA M. WAITARA: La pili. *(Kicheko)*

SPIKA: Sergeant-at-Arms anzeni kukaa sawasawa. *(Makofi/Kicheko)*

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

SPIKA: Naomba askari wa Bunge mkae sawasawa.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

SPIKA: Nasema kwa mara ya tatu askari wa Bunge mkae sawasawa popote pale mlipo. (*Makofii*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

SPIKA: Kwa nini mnapenda shari? Tuelewane wewe umeongea wenzako wamekusikiliza uwe na nafasi ya kusikiliza wenzako, kama unataka fujo utakuwa *handled* kwa fujo, kwa hiyo tusikilizane.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

MBUNGE FULANI: Mtoe.

SPIKA: Hivi anayenijibu ni nani huyo?

MBUNGE FULANI: Aende nje.

SPIKA: Wewe Katibu, anayenijibu ni nani?

MBUNGE FULANI: Marwa

MBUNGE FULANI: Ryoba.

MBUNGE FULANI: Waitara.

SPIKA: Ni Waitara huyo huyo?

MBUNGE FULANI: Waitara.

SPIKA: Basi Waitara nakutaka utoke nje kwa hiari yako mwenyewe. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Ryoba, Ryoba.

SPIKA: Utoke nje tena haraka, kabla sijawaita wale mabwana.

(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara alikuwa akikusanya makabrasha yake)

SPIKA: Waitara utoke nje unanicheleweshea muda.
(Makofii)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara aliendelea kukusanya makabrasha yake)

MBUNGE FULANI: *(Aliongea bila kutumia kipaza sauti).*

SPIKA: Sijakuruhusu useme kaa chini tafadhali.

((Hapa Mheshimiwa Mwita M. Waitara alitoka ndani ya Ukumbi wa Bunge)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi tuendelee.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, tunaendelea kutumia Kanuni ya 68(1) na wote tullisimama kuhusu Mwongozo. Kanuni ya 68(7) kinazungumzia kuhusu Mwongozo, hatuna muda wa kupoteza wa kuisoma lakini kama Waheshimiwa Wabunge watataka nisome nitaisoma lakini nadhani wote tunajua Kanuni ya Mwongozo ni Kanuni gani.

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nataka kusema ni kwamba naomba Mwongozo wako, Kanuni hizi za Bunge ambazo tunazitumia zimeweka misingi bora na imara kabisa ambayo inatuwezesha sisi Wabunge wote ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kufanya uwakilishi wetu wa kuwawakilisha wananchi wetu katika mambo mbalimbali lakini kimsingi katika mambo ya kuwapelekea maendeleo yanasisimamiwa na Kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hizi pia zimeweka utaratibu wa kimsingi wa kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali. Lengo la kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa kutumia Kanuni hizi ambazo Mheshimiwa Spika unaziongoza, baada ya Wabunge kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali, hapo sasa wananchi ambao tunawawakilisha humu ndani watakwenda kunufaika na huduma mbalimbali na nitaomba nizitaje chache. Kwa mfano, tukishapitisha bajeti hii ya Serikali tunakwenda kupitisha fedha za ujenzi wa zahanati kwa wananchi tunaowawakilisha; tunaenda kutoa huduma za dawa kwa wananchi wetu tunao wawakilisha; tunaenda kutoa huduma ya pembejeo kwa wananchi tunaowawakilisha; tunaenda kutoa elimu bure; tunaenda kupeleka maji; tunaenda kupeleka umeme; tunaenda kupeleka barabara; tunaenda kupeleka ajira kwa watoto wetu wasiokuwa na ajira; tunaenda kulipa malimbikizo ya madai mbalimbali ya watumishi wa Serikali wakiwemo walimu; tunakwenda kujenga nyumba za watumishi wa Serikali wakiwemo manesi, madaktari na walimu wetu na tunakwenda pia kutengeneza mfumo wa kitaasisi wa kibajeti wa kupambana na ujisadi katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, inapokuja tunapitisha bajeti ambayo inaenda kutatua kero hizi za Watanzania baadhi ya Wabunge wanasema bajeti hii hapana isipitishwe...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, halafu mfumo huu huu wa kikanuni unaweka utaratibu, tukishapitisha bajeti hii mwezi huu Bunge linakwisha, Bunge litakalofuata tutakuja na maswali ya kuihoji Serikali kwa nini haijapeleka huduma mbalimbali kwa wananchi na wakati huo bajeti ya kupeleka huduma hizo kwa wale wananchi wetu tumeikataa ndani ya Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo ninapoomba mwongozo wako, je, hivi mtu anayekataa bajeti ataruhusiwa

tena kuihoji Serikali kwa nini hajapeleka huduma hizo kule anakotoka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walismama wakitaka kuomba Mwongozo wa Spika*)

SPIKA: Ahsante, majibu nitatoa baadaye. Waheshimiwa ninayo orodha nilishaandika na nyie wote mlisikia niacheni nimalize hotuba yangu, tukiwa na muda tutaedelea nawaona. Mheshimiwa Kitwanga.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, nikishukuru. Natumia Kanuni ya 68(7), siko mbali sana na wewe Mheshimiwa Spika na msemajji allyepita. Kwa kawaida sisi sote ni Wabunge kuna mambo ya msingi ambayo kwa vyovyote vile sisi kama Bunge inabidi twende pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo kwa tofauti ya vyama vyetu tunatofautiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu nipate mwongozo wako, umeambiwa pesa hizi hapa katumie halafu unasema mimi sizitaki kwa sababu najitosheleza, kuna lazima gani tena sisi tupeleke pesa huko? Naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni hiyo ya 68(7). Wabunge tunapoigomea bajeti kwa kusema "Hapana" tafsiri yake ni kwamba Serikali iporomoke na isiendelee kuwepo na sisi wenyewe Wabunge tusambae kuanzia leo, tukarudie uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, najaribu kufikiria sana kwamba tulikuwa tunapambana na makinikia hapa, hawa wanapiga kelele kutetea wezi. Leo tunapitisha bajeti ambayo kwa

umakini kabisa tumechangia mawazo yetu siku sita na ya kwao yamechukuliwa hata na Waziri Mheshimiwa Mpango yamesomwa mazuri tu hapa na wote wakapiga makof, tumefika kwenye kupidisha bajeti wanakataa.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama kuna haja ya kumumunya maneno na kwa vile Watanzania wanatusikiliza na kutuangalia hawa watu, watu wao wameridhika. Ukienda kwenye Jimbo langu kule Nzera hatujawahi kuona lami, tumepigania makinikia, tunapitisha bajeti halafu mnaenda kuwarundikia hela za nini hawa? Chukueni hela hizo zileteni kwenye Jimbo langu la Geita tuna shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ulipoita jina langu mimi nilisema kwa besi ambayo sijawahi kuzungumza nilisema "Ndiyo" kwa sababu hatujaona lami. Hawa kina Msigwa na kina nani wana lami na wana kuku, hawana shida leteni pesa, tusiware hela hawa ili liwe fundisho. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Ghasia

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kupidha Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni muda huu mfupi ambapo tulikuwa tunapigia kura bajeti ya Serikali ambayo inahusu sekta zote iwe maji, umeme na kila kitu na mionganoni mwetu wapo ambao tumesema "Ndiyo" na wapo ambao wamesema "Hapana." Mwongozo ambao nilikuwa nauomba kwako pamoja na Serikali, hivi kuna uhalali wowote wa waliosema "Ndiyo" na waliosema "Hapana" kupata haki sawa katika bajeti hii iliyopitishwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nauliza hivyo kwa sababu kama ambavyo waliotangulia kusema tutakavyokuja kuuliza maswali na wao watataka kuuliza maswali kwenye Wilaya yangu, kwenye jimbo langu, naletewa lini maji, naletewa lini umeme? Hivi kwa mtu ambaye ameikataa bajeti anayo haki ya kupelekewa miradi kwenye eneo lake na anayo haki ya kuuliza maswali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo huo kwako na kwa Serikali, je, wanayo haki ya kuwahudumia hao ambao wameikataa bajeti? (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Tuanzie umeme tu wa *REA*.

SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni hiyo hiyo ya 68(7) kuhusiana na kilichotokea hapa na ningependa tu kuongezea machache kwa sababu mengi yamezungumzwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, wenzetu walitoka nje na tukapitisha hiyo bajeti lakini Serikali kwa kujua kwamba pande zote mbili ni za kwake bado wakapeleka hizo fedha za maendeleo. Tumekaa hapa sasa hivi tunaelekeea mwezi wa tatu na kwa bahati nzuri katika bajeti hii tumejadili kwa siku saba. Tukirudi katika bajeti zote zilizopita upande wa pili walikuwa na Mawaziri Vivuli ambao na wao walileta mapendekezo yao na baadhi ya mapendekezo yamefanyiwa kazi. Hata katika bajeti hii kuu ambayo tumeipigia kura muda mfupi uliopita pia walileta mapendekezo kwa kuchangia kila mmoja.

Mheshimiwa Spika, napata kigugumizi na naomba mwongozo wako kwa sababu uwepo wetu hapa ni katika kuhakikisha kwamba bajeti hii inapopita mimi kule kwetu Arumeru kuna shida nyingi, Arusha tuna shida nyingi na wapo Wabunge humu ambao wameikataa hiyo bajeti, je, ni haki? Vilevile kwa Mawaziri hawa ambao ndiyo tunaowategemea wao wanakamata mpini katika kuhakikisha kwamba wanapeleka maendeleo kule kwa kupeleka fedha ambazo tumezipitisha hapa, watakapopeleka fedha kule na sisi Wabunge tukazuia, je, tutatenda kosa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako tafadhali. (*Makof!*)

SPIKA: Wa mwisho katika orodha niliyokuwa nayo, ile tuliyoidhinisha mwanzoni ni Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) kutokana na kitu kilichotokea Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, huwa tuna *party caucus*, huwa tunapigwa msasa kabla ya vitu kama hivi, kabla ya kupiga kura tunafundishwa nini maana ya kupiga kura, nini maana ya kupiga "Ndiyo" ama "Hapana." Hata wewe utakuwa shahidi ulipotoa ufanuzi baada ya Mheshimiwa Sugu kuuliza wakakana kura zao, wakapiga makelele kwa maana hiyo walikuwa hawajui.

Mheshimiwa Spika, sasa illi kuleta usawa, naomba Mwongozo wako, kwamba utenge fungu la kutoa semina kwa Wabunge wote ili wajue nini maana ya kupiga kura ya "Hapana" na nini maana ya kupiga kura ya "Ndiyo" kwa sababu hawaelewi wajibu wao. Sasa hivi ukirudia tena watasema "Ndiyo wote wale pale. (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge wa Kambi Rasm ya Upinzani walismama ili kuomba Mwongozo wa Spika)

SPIKA: Sasa hamuwezi kusimama 30 haiwezekani na hasa mabosi wenu wa mbele wakishasimama wengine wote mnakaa chini, waachieni hawa wawili wa mbele labda nitamruhusu na Mheshimiwa James peke yake, kwa maana hiyo ni watatu. Kwa hiyo, wengine ridhikeni kwamba hawa wataongea kwa niaba yenu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Wale ni viongozi wako pia, labda leo mniambie siyo viongozi wenu hawa. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sema.

SPIKA: Kwa taarifa nilizonazo Mezani hawa ndio viongozi wenu wote, kwa hiyo, tulia viongozi wako wamesimama. Haya ninyi kaeni basi aongee kiongozi wenu, nimesikia kumbe ndiyo kiongozi wenu ninyi kaeni chini, basi kaa, tulia viongozi wako wanataka kusema. (*Kicheko*)

Tutaenda kwa *seniority*, sijui nani aliingia Bungeni *senior* hapo, jipangeni wenyewe aliyeingia wa kwanza halafu afuate aliyeifuata. Wenyewe hao, watatu hao nimewaruhusu lakini ni dakika mbili, mbili tu.

MBUNGE FULANI: Duh.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ni kweli nilliingia kwenye Bunge hili mwaka 1995, Bunge la mfumo wa vyama vingi nya siasa. Tulipewa semina na Mheshimiwa Spika Mstaafu Pius Msekwa, namna ya Mabunge ya *Commonwealth* yanavyo-*behave* na kuna suala la *three line whip*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mnachokizungumza hasa wakati huu wa bajeti, hili siyo Bunge la kwanza tangu mwaka 1995. Katiba yetu katika Ibara ya 3 inasema nchi yetu ni ya mfumo wa vyama vingi nya siasa.

Kwa hiyo, hili linalotokea hapa na kwa kuwa dua yetu inasema tumwombe Mwenyezi Mungu atujalie hekima na busara ya kufanya maamuzi sahihi, nashauri tu mlele *constitutional amendment* ili nchi hii iwe ya mfumo wa chama kimoja cha siasa. (*Makofii*)

SPIKA: Nawaombeni tuwasikilize hawa Wabunge.

WABUNGE FULANI: Aah.

SPIKA: Ndio nimewapa nafasi ni vizuri watumie dakika zao mbili vizuri na tunapoongea hapa Bungeni tuwe tunakumbuka hivi vitu Watanzania wengi wanavisikiliza na kadhalika. Kwa hiyo, tuwape nafasi wazungumzaji, endelea Mheshimiwa nakulinda.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ili zikishasemwa zidumu fikra za Mwenyekiti basi fikra hizo zidumu. Hata hivyo, nakumbuka Mwalimu kabla hajaondoka madarakani alisema siyo zidumu fikra za Mwenyekiti bali zidumu fikra sahihi za Mwenyekiti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *trend* hii sasa kama inaenda kwamba huna haki aufikra au uhuru wa kuwa na mawazo mbadala, hata Isaac Newton anatuambia katika kani mkabala kuna kani iliyo mrejeo sawa na kinyume na basi tufuate upande mmoja, *sincerely* toka sakafu ya moyo wangu, nashauri tufanye *constitutional amendment*, tuwe na chama kimoja cha siasa anayeweza kuingia huko aingie huko badala ya kupoteza rasilimali za Watanzania, kupoteza muda wa Watanzania, tukisema tupo kwenye demokrasia ya mfumo wa vyama vingi vya siasa kumbe hapana ukiwa na mawazo tofauti wewe ni adui wa jamii. (*Makofî*)

WABUNGE FULANI: Aah.

SPIKA: Ahsante dakika mbili zimeisha Mheshimiwa James.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: *Senior* mwengine anayefuata. Kumbe Mheshimiwa David ni *senior* kwa Mheshimiwa Peter eeh?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Nitakupa nafasi nimekuona Mheshimiwa Waziri, acha wamalizie.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kauli za leo za viongozi ndani ya Bunge ndiyo ambazo zinaweza zikapasua Taifa.

WABUNGE FULANI: Aaah.

MBUNGE FULANI: Muachenii aongee.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, sisi tuko ndani ya Bunge kama Wabunge wa Taifa, Bunge zima, sisi wote ni Watanzania. Hakuna kitu kinasikitisha, mimi niko mwaka wa saba humu ndani, miaka saba tuliyopitisha bajeti nimeshuhudia kura zote, kura ya "Ndiyo," "Hapana" na "Abstain." Miaka saba Bunge limekuwa likipitisha kwa mfumo huo na hakujawahi kutokea kauli za kusema wewe ukipiga "Ndiyo" utapata maji, wewe ukipiga "Hapana" hutapata maji, haijawahi kutokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote wananielewa kwa hiki ninachokisema...

SPIKA: Umebakiza dakika moja malizia.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ndiyo nakwenda namalizia, tusijenge Taifa tunaloweza kulipasua wenyewe. Mimi niliamini ulipokuwa unazungumza ulikuwa unafanya kama utani ambapo sasa watu wasiokuwa na uelewa sawasawa wakalichukua hili jambo kuwa *serious*. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Aaah.

SPIKA: Mheshimiwa Spika, ni vizuri ukaliweka sawa, tuko hapa kutetea kodi za wananchi wetu, tuko hapa kuainisha Serikali ilipokosea na Serikali ilipoweka mambo sawasawa, ndio kazi ambayo tunafanya hapa Bungeni. Tuko hapa hii ni bajeti ya 56 tangu tupate uhuru kama ni tatizo la maji bado lipo tangu tumepata uhuru, kama ni tatizo la afya lipo tangu tumepata uhuru. Tunapo-*pause challenge* lengo letu...

SPIKA: Ahsante sana dakika zako mbili zimeisha.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, lengo letu tunataka Serikali ifanye vizuri zaidi, ndiyo lengo tunalolitaka. (*Makofii*)

SPIKA: Umesikika, ahsante sana. Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. La kwanza ambalo naomba lieleweke kwa heshima kubwa kabisa, sisi hatujaja hapa kwa bahati mbaya kama Wapinzani na kuwepo kwetu kama wawakilishi, wananchi waliotuchagua walijua kabisa wanachagua watu wa Upinzani. Hata mawazo tunayoyaleta hapa wananchi wa Jimboni kwetu wanajua kabisa misimamo ya Wabunge wao wanataka nini, kwa hiyo, hatujaja hapa kwa bahati mbaya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pili, amezungumza sana Mheshimiwa James Mbatia, tunapopiga kura hapa au pesa ya Serikali inapopelekwa kwa wananchi siyo kwamba sisi Wapinzani tunafanyiwa hisani. Isionekane kwamba hiyo ni hisani ni pesa za Serikali, za walipa kodi, humu Bungeni tunaonyesha mitazamo tofauti. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tukisoma historia ndugu zangu maendeleo yoyote duniani yameletwa kwa hoja mbili zinazopingana, *simple as that.*

MHE. DAVID E. SILINDE: Yes.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Lakini mnakotaka kutupeleka mnaturudisha nyuma kitu ambacho hakiko duniani.

Mheshimiwa Spika, lakini kikubwa, kwa hesabu kubwa...

SPIKA: Malizia dakika ya pili.

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, ndio namalizia. Kwa heshima kubwa wala sitaki ioneckane kwamba nakidharau Kiti chako lakini kwa siku tano au ngapi wiki zilizopita ukisoma Kanuni ya 8 ambayo inaelekeza namna ya uendeshaji wa Bunge, kwa heshima kabisa Mheshimiwa Spika umekuwa *biased* na umekuwa ukishiriki kwenye michango, unatu-*direct* namna ya kuchangia. Sasa kuwepo kwetu hapa kama ukituongoza wewe na wewe ukishiriki inapoteza maana ya kuwepo Spika ambaye ni hakimu ambaye hupendelei. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, upande huu walikuwa wanaongea, wametoa Miongozo yao kinyume cha taratibu, watu wote wametoa Mwongozo unaofanana kanuni zinakataa lakini wameendelea kuzungumza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pilii...

SPIKA: Mheshimiwa Peter, unapoamua kabisa kumtuhumu Spika unapaswa kujipanga vizuri maana yake unachosema hata nikiulizwa na mtu niseme ulikuwa unaongea kitu gani, *I don't whether I can follow.*

MBUNGE FULANI: Aaaah.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nimkuomba radhi, nimesema...

SPIKA: Yaani unazungumzia kitu gani *in particular.*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, *in particular* nimesema, kwa mfano juzi wakati nachangia bajeti ulinisimamisha mara tatu...

SPIKA: Mimi nilifikiri leo tungeonhea ya leo?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Si umesema nitoe *particular* ili nielekeze kitu...

SPIKA: Sasa tukianza ya juzi na juzi ile?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Basi tuache ya nyuma
in particular leo...

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika,
sijamaliza.

MBUNGE FULANI: Mwongozo umerudiwa.

SPIKA: Zimeisha dakika mbili. Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nilisimama kwa ajili ya kutoa taarifa lakini kwa sababu ya mamlaka uliyonayo ukasema usitoe taarifa utanipa muda mwingine, kwa hiyo, naomba nizungumze kwa *context* ya taarifa kuwataarifu kwa madai yaliyosemwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, dunia inabadilika, mfumo tunaoutumia sisi tumeu-copykwenye mfumo wa nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Practice*) katika kuendesha Mabunge. Mfumo ule katika kipindi kama hiki cha kupiga kura ya bajeti kuna kura tatu kwa namna tulivyorithi na ambazo ndizo zilizosemwa hata kwenye Kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na mabadiliko yanayotokea duniani ya mazoea ya Mabunge mbalimbali watu wanabadilika. Kwa mfano, maandalizi ya bajeti za nchi siku za nyuma ilikuwa si shirikishi, ni Serikali inayotawala inaandaa bajeti, inapeleka kwa hiyo mnakwenda kubishana pale, lakini siku hizi sasa bajeti ni shirikishi. Mchakato wa bajeti unashirikisha hatua zote kuanzia mipango mpaka na bajeti yenyewe na maoni ya pande zote huchukuliwa. Hata kwa mfano Waziri wa Fedha alikuwa anajibu kupokea baadhi ya mapendekezo ya upande wa Upinzani na akasema haya nayachukua, haya nayachukua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kubwa hapa ni mawili, moja *the effect* ya kura ya "Ndiyo" na "Hapana" ni nini? Unaposema "Hapana" bajeti hii isipite maana yake Bunge livunjwe. Kwa hiyo, hii inaonyesha kwamba hauko *serious* unapenda Bunge livunjwe, lakini pia hata yale mawazo yako uliyoyaleta kwenye Serikali au katika mchakato mzima ya upande wa Upinzani yakakubaliwa na yenyewe yaliyokubaliwa na yenyewe unayakataa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nini kinatokea? Kwa baadhi ya Mabunge yaliyoendelea yanazidi kubadilika, kwa mfano, Bunge la India leo hii limebadilika linapiga kura mbili tu, linapiga kura ya "Ndiyo" au "*Abstain*," kura ya "Hapana" haipo. Kwa nini wamefikia hapo? Wamefikia hapo kwa sababu maoni yale ni shirkishi na baadhi ya mambo yanakuwa yamechukuliwa kwa hivyo huwezi ukakataa katakata ndiyo maana *you can only "Abstain"* lakini siyo kusema "Hapana."

Kwa hiyo, uki sema hapana kwa *connotation* yake ndiyo maana Mheshimiwa Spika unai-reflect kwa wananchi ambao wanasubiri maendeleo, wanasubiri shida zao zikatatuliwe kwa kuititia bajeti hii, unaposema hapo *completely the effect* yake ni kwamba wananchi wako wasiende kutatuliwa matatizo yao, ndiyo maana yake. (*Makofi*)

SPIKA: Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Katibu anazidi kujijandaa kumalizia mahesabu yake na mimi nimalizie kwa sababu wengi mlitaka miongozo kwa *ku-sum up* yote kwa pamoja. Nimshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene amenisaidia katika kujaribu kueleza kwa sababu sikuwa na muda wa kujaribu kuweka mambo yote, nadhani siku moja sijui tuwe na semina au nini ingawa siamini kama semina itasaidia kwa sababu, nisiseme sana.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili la bajeti ya leo tunayoihitimisha hapo limeanza kule kwenye Serikali zetu za Mitaa, kwenye Vijiiji, Kata, Halmashauri za Wilaya na wengine ni wajumbe huko limeanza huko na tumeshiriki kote huko

kama si wote lakini baadhi yetu tumeshiriki. Limekuja linapanda juu, sisi hapa tumeanza mapema mwezi wa Machi, mahali fulani hivi, tukaanza taratibu mara twende kwenye miradi nchi nzima huko tunazunguka, ndiyo jambo lenyewe linatengenezwa hivyo. (*Makofii*)

Tukaja kwenye Kamati zetu mbalimbali, sekta mbalimbali, kila Wizara mkakaa nazo huko, kumbukeni kumbi ambazo mmeenda huko sijui Hazina, sijui wapi, wengine mmeenda Mwanza hili hili, mwezi Aprili yote hili hili, Mei yote hili hili, mpaka leo tarehe 20 Juni. Limepitia hatua mbalimbali na hakuna hatua moja ambayo sisi kama Bunge tunaifanya tukiwabagua Wabunge fulani kwa sababu ni wa Chama Tawala au kwa sababu ni wa Upinzani. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, bajeti hizi na tulibadilisha Kanuni zetu, Mheshimiwa James Mbatia ananiambia mambo ya mwaka 1995 lakini mwaka 1995 Mheshimiwa James hamkuwa na bajeti shirikishi. Mlikuwa na bajeti mnakaa hapa, siku ya kwanza ya Bunge la bajeti anakuja Waziri wa Fedha, anasoma bajeti ya Serikali na huo ndio msimamo wa Serikali. Hajaulizwa mtu, hajafanya nini mtu, mnakaa hapo mnapiga maneno weee, mwisho mnapiga kura mmemaliza, mnataka hamtaki hamuwezi kubadilisha chochote katika bajeti ambayo imesomwa. (*Makofii*)

Leo hii ni tofauti, tunaanza na mapendekezo, sijui nini, tulikuja tarehe fulani hapa mwanzoni kule akataja *ceiling* ya Serikali, Waziri alikuja hapa, mipango ikoje, yote tunajenga kwa pamoja, kwa pamoja, kwa pamoja, leo ndio mwisho wa jambo lenyewe la pamoja. Tunafika mwisho mwenzangu mwingine ambaye kwenye bajeti hii ya Mheshimiwa Mpango ana bajeti kubwa kwenye jimbo lake mara mbili, mara tatu ya bajeti ya Kongwa au ya Mbunge mwingine ye yote aliyesema "Ndiyo." Yeye mwenye bajeti mara mbili, mara tatu anasema "Hapana." Sasa huu ni mchezo gani, kama upinzani ndio huo una maana gani? Upinzani siyo huo! Huwezi kukaa hapa miaka saba Mheshimiwa Silinde, kazi yako kwa miaka saba ni kusema hapana tu kwa kila jambo,

aiwezekani, hata lile ambalo umeshiriki wewe mwenyewe, unanielewa. (*Makofii*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

SPIKA: Nakusikia Mheshimiwa Susan Lyimo. Nakusikia vizuri sana na wewe ni *senior* na tulishaambiana hapa kama ungekuwa na jambo ungesimama kusema. Ukinivunja heshima na mimi nakuvunjia tu, wala halina shida. Ukishakuwa humu ndani lazima uwe tayari kusikiliza wengine na wewe uwe tayari kusikilizwa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, katika kumalizia niseme hata mimi huwa inanisumbua kabisa, tena *I am not joking*, linanisumbua kwamba mtu umeshiriki jambo mwanzo mwisho, umeoneshwa kila kitu mwanzo mwisho na baadhi ya mawazo yenu yamekubalika halafu dakika ya mwisho, sitaki!

MBUNGE FULANI: Na posho juu.

SPIKA: Sawa, hutaki, sasa mradi hutaki, kama alivyosema Mheshimiwa Jenista, miezi mitatu ijayo unatunga swalii, kule kwangu kwa nini kitu fulani, ambacho kinahusu fedha uliyosema sitaki, sasa Waziri akujibuje? (*Makofii*)

Kwa hiyo, ushauri wetu ulikuwa mwelesi tu kwa Waheshimiwa Mawaziri kwamba wanapokuja muwaambie tu lakini ulikataa bajeti. Halafu ukitaka kumsaidia msaidie labda mwakani atabadilika. Kama nilivyosema wengine wanasema "Hapana" siyo kwamba wanataka ndani ya moyo wao, basi tu wafanyeje, eeh! Maana mimi nayajua majimbo ambayo mtu hawezi kusema "Hapana" yaani labda awe ana matatizo mkubwa sasa yeze mwenyewe, yana shida kweli kweli, mwanzo mwisho. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tuendelee, lakini huko mbele iko haja ya kuangalia, hivi kama tatizo ni kitu fulani labda cha kushirikiana vizuri zaidi, hatuwezi kufika huko? Tukakifanya hicho ili

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tukaelewana? Mbona kwenye Kamati mnaelewana? Kwa nini ikishafika hapa tu basi tabu? (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya hatua hiyo, mimi nimalizie kwa kuomba tumpe nafasi Katibu wa Bunge sasa, atusomee matokeo ya zoezi letu. Katibu endelea.

MATOKEO YA KURA

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, naomba nirejeshe taarifa ya zoezi la kupiga kura. Kwa mujibu wa Kanuni ya 107 ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa taarifa ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote waliokuwepo katika ukumbi huu wakati tunaanza zoezi na baadaye wengine waliongezeka ni 356. Wabunge mliopiga kura ni 355. Kura moja ya uamuzi haikupigwa, ni kura ya Spika.

Mheshimiwa Spika, kura za "*Abstain*" ni zero, maana ya sifuri; kura za "*Hapana*" ni 95 na kura za "*Ndiyo*" ni 260. (*Makofi/Vigelegele*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Tunaanza na *REA*.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa matokeo haya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 yamepitishwa kwa jumla ya kura 260 sawa na asilimia 73. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: *REA, REA, REA, REA.*

SPIKA: Baada ya matokeo haya kutangazwa na Katibu, kama alivyoeleza, sasa naomba nitamke rasmi kwamba Bunge hili limepitisha Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama alivyoomba kwa mwaka wa fedha 2017/2018. (*Makofi*)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa niaba ya Bunge hili niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wote, nikisema hivyo nina maana na Naibu Mawaziri wote, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wako, ndugu zangu kutoka Wizara ya Fedha, wote kabisa Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na wengine wote, lakini vilevile Makatibu Wakuu wa Wizara zote na watendaji wao wote wanaowafuatia kwa kazi kubwa sana ambayo mmeifanya katika zoezi hili ambalo tumelieleza kwamba ni shirikishi na lina mduara mkubwa na huwa linaanza mbali sana. Maana kwa kawaida mwisho wa bajeti moja huwa ni mwanzo wa maandalizi ya bajeti nyingine, ni mchakato mrefu sana wenye kupitia hatua nyingi. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, ni ukweli usiopingika matatizo ya nchi hayawezi kutatuliwa kwa bajeti moja. Rafiki yangu Mheshimiwa Silinde aliposimama alisema ye ye ameshiriki kupitisha bajeti saba, tunataniana siku moja moja na mimi nimtanie kidogo, akasema matatizo ya afya hayajaisha, ya maji hayajaisha na mengine hayajaisha.

Nimkumbushe tu hata hiyo nchi ya Marekani iliyoendelea kuliko zote mpaka leo wana Waziri wa Afya maana yake ni kwamba hata iweje matatizo hayaishagi kwa mwanadamu. Kwa hiyo, Serikali ikiwepo lazima iendelee kutoa huduma za afya kwa sababu watakaougu wapo na watakuwepo. Lazima itoe huduma za maji kwa sababu maji ni uhai, binadamu hawezu kuishi bila maji yaani mambo haya ni endelevu kabisa. (*Kicheko/Makofî*)

Kwa hiyo, tunawapongezeni sana, ni matarajio yetu, sisi Wabunge wote na nyie Wabunge wote nawapongeza kwa kushiriki kwenye mchakato huu. Mmeshiriki sana na naomba tunakoenda tuzidi kuuelewa. Najua Wabunge walio

wengi ni wapya, michakato hii ilikuwa bado ni migeni lakini sasa tunavyozidi kwenda mnazidi kufahamu nafasi yenu iko wapi katika mduara mzima. (*Makof*)

Kwa kweli niishukuru sana Serikali, kama tulivyosema bajeti ya mwaka huu ni ya kupigiwa mfano kwa sababu Serikali imesikiliza. Yapo tutakayoendelea kuyasemea ndiyo maana sisi ni Wabunge. Kwani matatizo yakiisha kuna haja ya kuwa na Bunge, sasa si yameisha. Sababu tu sisi tuko hapa maana yake kwamba yako ya kufanya, ndiyo maana yake. (*Makof*)

Kwa hiyo, tutaendelea kusema msituchoke, tutaendelea kushauri kwa sababu wajibu wetu ni kuendelea kuboresha, kuendelea kupiga *brush*, kuendelea kupiga nakshi-nakshi, ili nchi yetu iweze kufika mahali pazuri zaidi na zaidi. Kwa hiyo, tunawapongeza sana, tunashukuru sana na tutatoa kila aina ya ushirikiano kuona bajeti hii inafanikiwa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hatua hii na baada ya kutoa pongozi kubwa sana kwa Serikali, tunapaswa sasa tupitishe Muswada wa Sheria ya Fedha ya Matumizi ya mwaka 2017 ambayo huwa inaitwa *The Appropriation Bill, 2017*, ambayo inaendana na Kanuni ya 108(1), (2) na ya (3). Utaratibu huo ni kwamba tutapitisha sheria hiyo katika mfululizo wa hatua zake zote bila ya kuwa na mjadala au mapendekezo ya mabadiliko yoyote kutoka kwa Wabunge.

Muswada huu hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ile ya Bunge ya Kudumu au ya Kisekta wala Kamati ya Bunge Zima na masharti kuhusu Muswada Kusomwa kwa Mara ya Kwanza katika Muswada huu hayatatumika.

Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu huwa hautangazwi kwenye Gazeti la Serikali kabla haujashughulikiwa Bungeni kama Miswada mingine inavyokuwa. Kwa kura ile ambayo tumepiga hapa na

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

matokeo yaliyotoka maana yake ni kwamba tumepitisha *The Appropriation Bill* ila kiutaratibu wa Kibunge sasa nitamtaka Katibu aendelee kwa Kusoma kwa Mara ya Kwanza na hatua zinazofuata kwa mujibu wa Kanuni ile ya 108(1). Kwa wale ambao wanataka kujua vizuri jambo hili, mtasoma kwa wakati wenu Kanuni zenu kuanzia Kanuni ya 108, Katibu. (*Makofi*)

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2017 (*The Appropriation Bill, 2017*)

(*Kusomwa kwa Hatua zake zote*)

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuidhinisha jumla ya shilingi triliungi thelathini na moja, bilioni mia saba na kumi na moja, milioni mia tisa themanini na tano, laki nane na themanini na nne elfu kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2018, kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo [*A Bill for an Act to apply a sum of thirty one trillion, seven hundred eleven billion, nine hundred eighty four thousand shillings out of the Consolidated Fund to the service of the year ending on the 30th Day of June, 2018, to appropriate the supply granted for that year, to authorize the reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes.*].

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

**MUSWADA WA SHERIA YA KUIDHINISHA MATUMIZI YA
SERIKALI WA MWAKA 2017 (*THE APPROPRIATION BILL, 2017*)
KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI**

ISSN 0856-01001X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BILL SUPPLEMENT

No. 4

16th June, 2017

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 24 Vol. 98 dated 16th June, 2017
Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

APPROPRIATION ACT, 2017

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section Title

1. Short title.
2. Interpretation.
3. Issuance of TShs. 31,711,985,884,000 out of Consolidated Fund.
4. Appropriation of moneys voted.
5. Power of the Minister to borrow.
6. Power of the Minister to reallocate certain appropriation moneys.

SCHEDULE

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
..... June, 2017

JOHN W. H. KIJAZI
Secretary to the Cabinet

A BILL

for

An Act to apply a sum of Thirty One Trillion, Seven Hundred Eleven Billion, Nine Hundred Eighty Five Million, Eight Hundred Eighty Four Thousand Shillings out of the Consolidated Fund to the Service of the year ending on the thirtieth day of June, 2018, to appropriate the supply granted for that year, to authorise the reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes.

ENACTED by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

Short title 1. This Act may be cited as the Appropriation Act, 2017.

Interpreta-
tion
Cap. 348
Cap. 439

2. The expressions used in this Act shall each have the meaning ascribed to it in the Public Finance Act and Budget Act.

Issuance
of Shs.
31,711,98
5,884,000
out of
Consolida-
ted Fund

3. The Treasury may issue out of the Consolidated Fund and apply towards the supply granted for the service of the year ending on the thirtieth day of June 2018, the sum of Thirty One Trillion, Seven Hundred Eleven Billion, Nine Hundred Eighty Five Million, Eight Hundred Eighty Four Thousand Shillings.

Appropriati-
on of
moneys
voted

4. The sum granted by section 3 shall be appropriated to the purposes and in the amounts specified in the third, fourth and fifth columns respectively of the Schedule to this Act.

- Power of the Minister to borrow
- 5.-(1) The Minister may, at any time or times not later than the thirtieth day of June, 2018, borrow within or outside the United Republic or partly within and partly outside the United Republic, any sum or sums not exceeding in the whole sum of Thirty One Trillion, Seven Hundred Eleven Billion, Nine Hundred Eighty Five Million, Eight Hundred Eighty Four Thousand Shillings by way of loan, advance, the issue of bills or bank overdraft and on such terms and conditions as the Minister may deem expedient, and may charge that loan or advance on any of the assets of the United Republic, including securities forming part of the Consolidated Fund.
- (2) Any money borrowed under this section shall be placed to the credit of the exchequer account and shall form part of the Consolidated Fund, and be available in any manner in which that Fund is available.
- (3) Any money borrowed under this section shall be subject to repayment in accordance to the conditions prescribed in the Loan Agreements between the United Republic of Tanzania and the Lenders, and any sum required for the repayment of any money so borrowed, and of any interest payable in respect of that money shall be charged on and paid out of the Consolidated Fund.
- Cap. 134
- (4) The powers conferred upon the Minister by this section shall be in addition to the powers of the Minister under the Government Loans, Guarantees and Grants Act.
- Power of the Minister to reallocate certain appropriated moneys
6. - (1) Where the Minister is satisfied that it is necessary in the public interest that provision be made for defraying the expenditure of any Region, Ministry or Independent Department of the Government in excess of any sum voted for it or for any service for which no sum is voted, and that it would be detrimental to the public interest to postpone the expenditure until provision is made for it by the National Assembly, subject to the provisions of the Budget Act, he may authorise the application of any surplus arising out of savings in the Consolidated Fund or any vote in the Schedule to this Act (other than votes for pensions, gratuities or other retirement benefits, or for widow's and orphans' pension) for or towards the excess or service.
- Cap. 439
- (2) Where the Minister authorises the application of any surplus under this section, he shall cause to be laid before the National Assembly, a supplementary estimates Bill or Statement of reallocation, as the case may be, in accordance with the provisions of the Constitution and the Budget Act.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- Cap.439 (3) Subject to the conditions specified in the Budget Act the Minister may delegate all or any of the powers conferred upon him by this section to any public officer subject to such limitations as the Minister may specify.

Cap 348 (4) The provisions of section 22 of the Public Finance Act, shall not apply to the powers conferred upon the Minister by this section.

Cap.439 (5) Subject to the conditions specified in the Budget Act the Minister may, by certificate under his hand, reallocate any sums arising from savings in the Consolidated Fund to any of the purposes specified in the second, third and fourth columns respectively of the Schedule to this Act, and where this occurs, the provisions of sections 3 and 4 shall take effect as if the total sum granted out of the Consolidated Fund and the amounts appropriated for the purpose specified in such certificate were raised by the amount or amounts specified in the certificate.

*Appropriation Act***SCHEDULE**

(Made under Section 4)

Vote No. (1)	Ambit (2)	Recurrent Expenditure Shs. (3)	Development Expenditure Shs. (4)	Total Shs. (5)
02	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Teachers' Service Commission	12,422,291,000	-	12,422,291,000
03	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the National Land Use and Planning Commission	2,115,372,000	-	2,115,372,000
04	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Records and Archives Management Department	2,375,726,000	2,000,000,000	4,375,726,000
05	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the National Irrigation Commission	4,055,481,000	20,103,412,000	24,158,893,000
07	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Treasury Registrar	104,917,488,000	2,000,000,000	106,917,488,000
09	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Secretariat of the Public Remuneration Board	1,721,987,000	-	1,721,987,000
10	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Joint Finance Commission	1,386,818,000	-	1,386,818,000
11	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Oil and Gas Bureau	711,073,000	-	711,073,000
12	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Judicial Service Commission	1,102,911,000	-	1,102,911,000
13	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Financial Intelligence Unit	1,515,586,000	-	1,515,586,000
14	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Fire and Rescue Force	30,284,288,000	3,500,000,000	33,784,288,000
15	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Commission for Mediation and Arbitration	3,409,750,000	-	3,409,750,000
16	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Attorney General Office	7,282,523,000	-	7,282,523,000
18	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the UNESCO Commission	663,123,000	-	663,123,000
20	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the State House	16,267,586,000	-	16,267,586,000
21	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Treasury	570,667,099,000	1,395,636,702,000	1,966,303,801,000
22	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Public Debts and G/Services	9,472,122,300,000	-	9,472,122,300,000
23	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Accountant General Department	45,960,838,000	3,600,000,000	49,560,838,000
24	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Tanzania Cooperative Development Commission	6,293,854,000	-	6,293,854,000
25	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Prime Minister	5,923,228,000	-	5,923,228,000
26	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Vice President	4,914,608,000	-	4,914,608,000
27	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Registrar of Political Parties	19,525,938,000	-	19,525,938,000
28	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Home Affairs-Police	593,212,597,000	5,253,623,000	598,466,220,000
29	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Home Affairs-Prisons Service	198,123,603,000	7,254,742,000	205,378,345,000
30	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the President Office and Cabinet Secretariat	368,314,145,000	379,570,890,000	747,885,035,000

Appropriation Act

Vote No. (1)	Ambit (2)	Recurrent Expenditure Shs. (3)	Development Expenditure Shs. (4)	Total Shs. (5)
31	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Vice President's Office	8,214,535,000	6,788,452,000	15,002,987,000
32	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the President's Office-Public Service Management and Good Governance	26,695,038,000	7,000,000,000	33,695,038,000
33	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ethics Secretariat	6,990,422,000	1,650,000,000	8,640,422,000
34	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Foreign Affairs and East Africa Co-operation	142,845,419,000	8,000,000,000	150,845,419,000
35	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Public Prosecutions Division	14,914,063,000	-	14,914,063,000
37	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Prime Minister's Office	21,819,483,000	66,165,373,000	87,984,856,000
38	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Defence	1,205,244,290,000	8,000,000,000	1,213,244,290,000
39	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the National Service	283,362,530,000	6,000,000,000	289,362,530,000
40	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Judicial Fund	106,959,018,000	18,158,011,000	125,117,029,000
41	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Constitutional Affairs and Justice	7,056,046,000	2,806,020,000	9,862,066,000
42	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the National Assembly Fund	114,452,262,000	7,200,000,000	121,652,262,000
43	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Agriculture, Livestock Development and Fisheries - Agriculture	64,562,759,000	150,253,000,000	214,815,759,000
44	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry Industries, Trade and Investment - Industries	24,172,493,000	73,840,377,000	98,012,870,000
45	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the National Audit Office	61,832,948,000	11,800,948,000	73,633,896,000
46	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Education, Science and Technology	419,843,419,000	916,841,822,000	1,336,685,241,000
48	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Lands and Human Settlements Development	43,255,083,000	25,400,000,000	68,655,083,000
49	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Water and Irrigation	24,457,460,000	623,606,748,000	648,064,208,000
50	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Finance and Planning	55,039,643,000	11,570,500,000	66,610,143,000
51	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Home Affairs	18,567,866,000	20,000,000,000	38,567,866,000
52	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children - Health	291,932,052,000	785,805,952,000	1,077,738,004,000
53	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Health - Community Development, Gender and Children	35,300,602,000	2,606,278,000	37,906,880,000
55	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Commission for Human Rights and Good Governance	3,894,182,000	2,272,796,000	6,166,978,000
56	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the PO-Regional Administration and Local Authority	32,022,298,000	417,256,688,000	449,278,986,000
57	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Defence and National Service	17,910,997,000	205,000,000,000	222,910,997,000
58	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Energy and Minerals	59,705,755,000	938,632,006,000	998,337,761,000
59	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Law Reform Commission	2,034,335,000	-	2,034,335,000

Appropriation Act

Vote No. (1)	Ambit (2)	Recurrent Expenditure Shs. (3)	Development Expenditure Shs. (4)	Total Shs. (5)
60	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry Industries, Trade and Investment – Trade and Investment	17,852,240,000	6,350,000,000	24,202,240,000
61	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Electoral Commission	4,764,294,000	10,000,000,000	14,764,294,000
62	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Works, Transport and Communication - Transport	91,142,025,000	2,477,931,183,000	2,569,073,208,000
64	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Agriculture, Livestock Development and Fisheries - Fisheries	14,792,646,000	2,000,000,000	16,792,646,000
65	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Prime Ministers' Office – Labour, Youth Development, Employment and Disabilities	12,656,130,000	17,400,000,000	30,056,130,000
66	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Planning Commission	4,936,364,000	4,475,800,000	9,412,164,000
67	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Public Service Recruitment Secretarial	2,365,975,000	750,000,000	3,115,975,000
68	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Works, Transport and Communication - Communication	4,104,139,000	14,000,000,000	18,104,139,000
69	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Natural Resources and Tourism	96,794,662,000	51,803,284,000	148,597,946,000
91	The Salaries, expenses and Development Expenditure of Anti Drug Commission	4,015,912,000	-	4,015,912,000
92	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Tanzania Commission for AIDS	2,528,604,000	3,455,343,000	5,983,947,000
93	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Immigration Department	50,200,098,000	4,000,000,000	54,200,098,000
94	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Public Service Commission	4,909,516,000	-	4,909,516,000
96	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Information, Culture, Arts and Sports	21,892,695,000	6,320,000,000	28,212,695,000
98	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Works, Transport and Communication - Works	34,123,282,000	1,895,582,432,000	1,929,705,714,000
99	The Salaries, expenses and Development Expenditure of the Ministry of Agriculture, Livestock Development and Fisheries – Livestock Development	25,963,524,000	4,000,000,000	29,963,524,000
36	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Katavi Region	57,273,546,000	23,835,445,000	81,108,991,000
47	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Simiyu Region	133,670,359,000	39,561,069,000	173,231,428,000
54	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Njombe Region	120,472,060,000	30,907,892,000	151,379,952,000
63	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Geita Region	164,319,542,000	41,478,543,000	205,798,085,000
70	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Arusha Region	215,047,810,000	58,085,803,000	273,133,613,000
71	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Coast Region	170,279,100,000	50,849,559,000	221,128,659,000
72	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Dodoma Region	207,739,837,000	51,599,629,000	259,339,466,000
73	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Iringa Region	152,886,772,000	38,087,699,000	190,974,471,000
74	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Kigoma Region	159,680,888,000	44,828,305,000	204,509,193,000
75	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Kilimanjaro Region	244,688,363,000	47,881,493,000	292,569,856,000

Appropriation Act

Vote No. (1)	Ambit (2)	Recurrent Expenditure Shs. (3)	Development Expenditure Shs. (4)	Total Shs. (5)
76	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Lindi Region	112,035,860,000	28,075,889,000	140,111,749,000
77	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Mara Region	214,199,437,000	46,000,347,000	260,199,784,000
78	The Salaries, expenses and Development Expenditure Mbeya Region	228,035,937,000	53,196,737,000	281,232,674,000
79	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Morogoro Region	263,726,039,000	59,551,132,000	323,277,171,000
80	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Mtwara Region	150,761,076,000	51,822,891,000	202,583,967,000
81	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Mwanza Region	288,893,428,000	67,729,379,000	356,622,807,000
82	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Ruvuma Region	173,903,813,000	54,509,447,000	228,413,260,000
83	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Shinyanga Region	141,973,425,000	39,853,538,000	181,826,963,000
84	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Singida Region	138,568,330,000	36,553,385,000	175,121,715,000
85	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Tabora Region	181,473,717,000	53,445,063,000	234,918,780,000
86	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Tanga Region	261,221,378,000	60,344,130,000	321,565,508,000
87	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Kagera Region	215,120,922,000	48,707,839,000	263,828,761,000
88	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Dar es Salaam Region	418,106,005,000	243,500,368,000	661,606,373,000
89	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Rukwa Region	96,106,143,000	24,779,193,000	120,885,336,000
90	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Songwe Region	89,623,908,000	31,040,524,000	120,664,432,000
95	The Salaries, expenses and Development Expenditure for Manyara Region	151,168,600,000	39,724,591,000	190,893,191,000
	Total	19,712,393,612,000	11,999,592,272,000	31,711,985,884,000

OBJECTS AND REASONS

The object of this Bill is to apply the sum of Shs. 31,711,985,884,000 out of the Consolidated Fund to the service of the Financial Year 2017/2018.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Muswada huu ni kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 ya jumla ya Shilingi 31,711,985,884,000.

Dar es Salaam,
..... Juni, 2017

PHILIP ISDOR MPANGO
Waziri wa Fedha na Mipango

SPIKA: Alichofanya Katibu ni kuusoma Muswada huo kwa jina refu. Sasa naomba Katibu usome kwa Mara ya Pili.

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa mwaka 2017 [*The Appropriation Bill, 2017*].

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Naomba sasa Katibu, uusome kwa Mara ya Tatu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shillingi trillioni thelathini na moja, billioni mia saba na kumi na moja, milioni mia tisa themanini na tano, laki nane na themanini na nne elfu kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2018, kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo [*A Bill for an Act to apply a sum of thirty one trillion, seven hundred eleven billion, nine hundred eighty four thousand shillings out of the Consolidated Fund to the service of the year ending on the 30th Day of June, 2018, to appropriate the supply granted for that year, to authorize the reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes*].

(Kusomwa Mara ya Tatu)

SPIKA: Kwa hatua hizo tatu maana yake ni kwamba Muswada huu umeshapitishwa rasmi na Bunge hili. Kama ilivyo ada, Muswada huu utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya saini yake. Baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kufanya hivyo, basi sasa itakuwa Sheria iliyokamilika. Kwa jinsi hiyo ikishakuwa imekamilika tunawatakitia kila la kheri Serikali katika utekelezaji wa jambo hili la bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Bhagwanji leo ametembelewa na mke wake, sijui yuko upande gani, Mama Bhagwanji, naomba usimame. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

(Hapa Mama Bagwanji alionyesha ishara ya upendo kwa kubusu)

(Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangilia)

SPIKA: Ahsante sana mama. Sasa ndugu zangu, hata shemeji yetu akija naye hata kumpigia kofi mnanuna? Inakuwa kila jambo jamani, siyo vizuri hivyo. Hilo nawatania tu, mambo mengine tuwe tuna... (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, mwisho niwashukuru sana wenzangu ambao tumesaidiana hapa kwenye Meza kwa ajili ya shughuli nzima hii ya uendeshaji wa Mkutano huu hadi hapa tulipofika na tunaendelea. Kwa kipekee nimshukuru sana Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson; Mheshimiwa Andrew Chenge nakushukuru sana; Mheshimiwa Azzan Mussa Zungu, nakushukuru sana, siku hizi nasikia anaitwa jaza ujazwe na bila kumsahau Mheshimiwa Najma Giga, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mtaona kipindi hiki cha miezi hii mitatu ambayo tumekuwa tukiendesa mambo hapa kwa maana ya vikao hivi nya Mkutano huu, tulibadilishana sana, leo amekaa huyu, kesho amekaa yule, ile yote ni kuondoa yale mambo aliyokuwa anasema Mheshimiwa Msigwa siku ile ulinifanya hivi. Namwambia haya mimi nilifanya, haya siku ya Mheshimiwa Najma nayo, haya siku ya Mheshimiwa Chenge na yeye, haya siku ya Mheshimiwa Zungu nayo. Ningekaa mwenyewe Mkutano mzima hapo ingekuwa hoja nzito lakini kwa vile tulikuwa tunaachiana sana naamini kila mmoja, huwezi kupata yote, lazima kuna siku unafurahi siku nyingine, Mungu ndivyo alivyoumba.

Kwa ujumla wake tumeenda vizuri, naomba niwashukuruni sana wote mpaka hapa tulipofika, bado tuna

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

hatua nyingine zinafuata, *Finance Bill* bado ipo na shughuli nyingine za Bunge zipo na wengine wananiulizaauliza vipi baada ya tarehe 30 Juni?

Sasa hilo niachieni kwanza, lakini nadhani mnaweza mkabakibaki hivi, lakini tutaambiana. Uwezekano mkubwa msianze kufungasha bado shughuli ipo, si tumekubaliana hii Serikali ya Hapa Kazi Tu. (*Makofi*)

Baada ya maneno hayo, ndugu zangu niwakumbushe futari ambayo ipo kwa wale ambao wana fursa ya kuweza kufika, wale wenye udhuru, basi hakuna neno. Wazee wangu wa *Tanganyika Legion* tafadhali naomba tuwe pamoja na wageni wote ambao mmefika mko kwenye *galleries* tuungane, watumishi wa Bunge wote msiogope, Maafisa wangu wa kutoka Wizara ya Fedha wote mliopo tafadhali karibuni sana kwa futari na madereva wetu walioko nje tunawakaribisha pia waweze kuingia tushirikiane kwa pamoja, huo ndiyo Utanzania wenyewe. (*Makofi*)

Kwa hatua hiyo, naomba tusimame, sasa naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge Lillahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 21 Juni, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*